Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 1 Agosti, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):**

Majumuisho ya Mpango Mkakati wa Kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Wizara na Idara za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Majumuisho ya Mpango Mkakati wa Kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mikoa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU):**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge la Uuzwaji wa Nyumba za Serikali.

**MHE. JOB YUSTINO NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira juu ya Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji na Bei zake ambavyo muda wake Kisheria unaisha Mwaka 2009.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge Kuhusu Mchakato wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura ulioipa ushindi *Richmond Development Company LLC.* ya Houston Texas – Marekani, Mwaka 2006.

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Taarifa ya Serikali Kuhusu Ubinafsishaji wa Mgodi wa Kiwira.

## KAULI ZA MAWAZIRI

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007, Kanuni Namba 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu Matumizi ya Magunia ya Katani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe taarifa fupi kuhusiana na utaratibu wa matumizi ya magunia ya katani kwa lengo la kulinda zao la Mkonge na Viwanda vya Magunia ya Katani hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwepo hoja na maombi ya kutaka Serikali kwa nia ya kulinda Viwanda vya Katani, ilazimishe matumizi ya magunia *(Mandatory Use of Sisal Bags)*. Ili kushughulikia suala hili, mwaka 2001 Wizara iliunda Timu ya Watalaam kutafakari hoja hiyo na kuitolea maoni.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Timu hiyo, baada ya kutafakari hoja yenyewe, ilipendekeza ulazima wa kutumia magunia ya katani kuweka baadhi ya mazao yamkiwemo ya kahawa, korosho, kokoa na mahindi *(Selective Mandatory use of Sisal Bags)*.

Hata hivyo, kwa kuzingatia sera ya soko huria, Wizara ilisita na kuitaka kampuni inayozalisha magunia hapa nchini ishindane kwa kutangaza ubora wa mazao yake na pia kuangalia gharama za uzalishaji ili kuvutia wanunuzi kwa bei. Pamoja na Wizara kusita, mazao ya kahawa na mahindi ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula yaliendelea kutumia magunia ya katani kupitia katika zabuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya uamuzi huo wa Wizara, hoja hii ya kutaka kulinda viwanda vya mkonge, tarehe 29 Aprili, 2008, Wizara ya Biashara na Viwanda iliitisha

kikao cha wadau na kuamua suala hili lifanyiwe kazi na Mtalaam Mwelekezi *(TISCO). TISCO* kwa upande wake ilitoa maoni ya kutumia magunia ya katani kwa baadhi ya mazao *(focused mandatory use of sisal bags)* na mazao yaliyolengwa ni mahindi, mpunga, kahawa, korosho, kokoa na karafuu.

Mheshimiwa Spika, majadiliano ya wadau kuhusu suala hili pia yalikuwa na mgawanyiko kwa waliokubali na sababu zao na waliokataa na sababu kama ifuatavyo:-

Wadau waliokubaliana na ushauri wa kuwa na *focused mandatory use of sisal bags*, walikuwa na sababu zifuatazo:-

(i) Magunia ya plastic jute yana athari ya uharibifu wa mazingira kwa kuwa yana tabia ya kutokuoza.

(ii) Kutumia magunia ya katani kutasaidia kulinda viwanda vya ndani vya magunia ya mkonge kama ambavyo nchi za India na Bangladesh zinavyolinda viwanda vyao vya magunia ya jute.

(iii) Tutalinda na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, wadau ambao hawakukubaliana na Mtalaam Mwelekezi kuhusu *focused mandatory use of sisal bags* walikuwa na hoja zifuatazo:-

(i) Hatuna viwanda vya kuzalisha magunia ya kutosha kulingana na mahitaji. Uzalishaji kwa wakati huo ulikuwa takriban magunia milioni 1.5 wakati mahitaji yalikuwa magunia milioni 3.5 kwa mazao 6 tu yaliyolengwa.

(ii) Kampuni ya *TPM 1998 Limited* haikuwa imeionyesha jitihada za kutosha katika kutangaza magunia yale inayozaliha. Utafiti wa *TISCO* ulidhihirisha kuwa baadhi ya wadau wa magunia hayo hawakufahamu hata kampuni hiyo kama ipo, na wale waliofahamu kuwepo kwake, hawakufahamu namna ya kuyapata.

(iii) Dhana ya *focused mandatory use of sisal bags* italeta ukiritimba ambao utasababisha kupanda kwa bei za magunia ya katani.

(iv) Kulazimisha matumizi ya katani siyo njia ya kulinda viwanda vyetu.

(v) Utekelezaji wa *mandatory use of sisal bags* utaathiri ushindani wa mazao katika masoko ya Kimataifa kutokana na bei kubwa ya vifungashio (magunia).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Wizara kuhusu suala hili umebaini:-

(i) Kipo kiwanda kimoja tu cha magunia ya katani kinachofanya kazi ambacho uzalishaji wake wa sasa ni magunia milioni 1.5 ambao haukithi mahitaji ya magunia milioni 3.5 yanayohitajika kwa mwaka kwa mazao hayo yanayolengwa.

(ii) Bei ya kununulia guni la mkonge kabla ya kuondoa *VAT* ilikuwa shilingi 2880/= ukilinganisha na bei ya gunia la jute ya shilingi 1820/= ikiwa na pamoja na *VAT* na gharama nyingine.

(iii) Uchaguzi wa magunia gani yatumike wakati wa kuuza mazao nchi za nje inategemea matakwa *(Specification)* ya nchi inayoagiza zao husika. Kwa zao la kahawa kwa mfano; Shirika la Kimataifa la Kahawa *(ICO)* imeruhusu matumizi ya aina zote za magunia. Aidha, kwa ushauri wa *TBS*, Wizara ilitoa maelekezo kwa Bodi ya Kahawa kuwa magunia ya aina zote yanaweza kutumika.

(iv) Hoja ya kulinda ajira ni muhimu siyo tu kwa mkonge, bali hata kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, tarehe 27 Julai, 2009 wakati Bunge lako Tukufu likijadili hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, hoja ya kulinda viwanda vya katani ilijadiliwa na Wabunge wengi kwa kusema na kwa maandishi. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge, yalizingatia:-

(i) Umuhimu wa kulinda zao la mkonge dhidi ya ushindani usiokuwa wa haki wa magunia ya *jute* na bidhaa zake ambazo siyo zimetungiwa sheria ya *mandatory use* huko India na Bangladesh, bali pia wanafidia *(subsidized)* uzalisha wake.

(ii) Asilimia 60 ya nyuzi zinazotumika kutengeneza magunia ya katani ni *secondary grades* ambazo hazina soko nje, hivyo kusimamisha utengenezaji wa magunia hayo kutaathiri uzalishaji wa zao la mkonge, kutaathiri ajira ya wafanyakazi 500 walioajiriwa na viwanda na pia wafanyakiazi 10,000 wa mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari hoja za Waheshimiwa Wabunge na utafiti uliofanywa na watalaam mwaka 2001 na wa *TISCO 2008*, Serikali imefikia uamuzi ufuatao:-

(i) Kimsingi Serikali inakubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge juu ya umuhimu wa kulinda viwanda vya mkonge dhidi ya ushidani usiokuwa wa haki wa magunia ya *jute* ambayo yanapewa ruzuku na Serikali za nchi yanakozalishwa. *(Makofi)*

(ii) Ili kutekeleza uamuzi wa kulinda vyanda vya mkonge, Serikali inahitaji muda usiozidi wiki mbili kukutana na wadau kama vile wazalishaji wa magunia na watumiaji ili kujiridhisha kwa mambo yafuatayo:-

· Bei ya gunia la mkonge baada ya kuondoa *VAT,* ili uamuzi wetu uwape nafuu watumiaji wa magunia. Kwa taarifa tulizonazo, bei ya gunia la mkonge kwa sasa ni

shilingi 2150/= baada ya kuondoa *VAT* ukilinganisha na 1820/= kwa gunia la *jute* pamoja na kodi.

· Uwezo wa kuzalisha magunia zaidi kutoka magunia milioni 1.5 ya sasa kufikia magunia milioni 3.5 yanayohitajika kwa mazao 6 yanayopendekezwa kuingizwa katika *focused mandatory use*. Hatua hii itazingatia umuhimu wa kuanzisha uzalishaji wa magunia katika kiwanda cha Moshi. *(Makofi)*

· Ili kulinda maslahi ya wakulima wa mazao yatakayotumia mazao ya mkonge pekee, itabidi yawepo makubaliano baina ya Serikali na wazalishaji wa magunia ili kuhakikisha bei haipandishwi kiholela na kuathiri pato la mkulima wa mazao husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mara kwa mara tumekuwa tunajivunia kwamba Serikali yetu ni Serikali sikuvu! Ahsante sana. Tunashukuru sana kwa jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu na Seri kali kwa ujumla kuweza kufika hapo kwa maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

## HOJA ZA KAMATI

### Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Uteklezaji wa Azimio la Uuzwaji wa Nyumba za Serikali kma lilivyowasilishwa na Serikali

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MINDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha Azimio hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Aprili, 2008 katika Mkutano wa 11, Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio kuhusu uuzwaji wa nyumba za Serikali baada ya kuzingatia hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Bent Aloyce Kimaro, Mbunge wa Vunjo. Azimio hilo liliazimia yafuatayo:-

(i) Serikali itekeleze mara moja bila kusita agizo la Rais kurejsha nyumba zilizouzwa kinyume na utaratibu na kwa watu ambao hawakuwa watumishi wa Serikali wakati huo na vile vile nyumba ambazo hazikupaswa kuuzwa kama zile zilizopo kwenye maeneo ya utawala wa Serikali.

(ii) Serikali irejeshe kwenye umiliki wake nyumba hizo zilizouzwa kinyume na utaratibu.

(iii) Serikali itoe orodha ya nyumba zake ambazo ziliuza kwa watu ambao si watumishi wa Serikali kinyume na utaratibu na pia zile ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za watumishi wa Serikali waliostahili kutumia nyumba hizo.

(iv) Serikali ichukue hatua kwa wale ambao hawajalipa na mikataba yao ya kuuziwa nyumba irejshwe kuhakikisha kuwa malipo hayo yanalipwa mara moja ama mikataba yao kufutwa na nyumba kurejeshwa kwenye umiliki wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Azimio la Bunge: Tarehe 1 Julai, 2009, Serikali iliwasilisha Taarifa ya Utekelzaji wa Azimio la Bunge kuhusu Uuzwaji wa Nyumba za Serikali. Katika taarifa hiyo, uteklezaji wa Azimio hilo, Serikali ilibainisha makundi matano ambayo nyumba zake ziliuzwa bila kufuata utaratibu, makundi hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Nyumba zilizoko kwenye makambi.

(ii) Nyumba zilizouzwa kwa watu binafsi ambao si watumishi wa Umma.

(iii) Nyumba zaidi ya moja zilizouzwa kwa familia moja ya watumishi wa umma.

(iv) Nyumba za Taassisi mbali mbali zilizouzwa kwa watumishi wa Serikali Kuu.

(v) Nyumba ambazo ziko katika maeneo nyeti ya Serikali na ambazo ziliuzwa kwa watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa, Serikali imekiri kuwa kuna upungufu uliojitokeza katika kutekeleza zoezi hilo la uuzwaji wa nyumba za Serikali na hatua mbali mbali zimekwishachukuliwa kurekebisha hali hiyo. Aidha, Serikali katika kutekleza Azimio hilo imefanya mambo yafuatayo:-

(i) Imefuta mikataba nyumba 53 zilizokuwa katika maeneo ya makambi ya Polisi, Magereza na Hospitali.

(ii) Imefuta mikataba ya nyumba 4 ambazo ziliuzwa kwa watu wasiokuwa watumishi wa Serikali baada ya wahusika kutoa taarifa za uongo. Nyumba 3 zimerejeshwa Serikalini na moja ambayo bado ina utata katika uuzwaji wake na mhusika alifungua kesi Mahakamani na baadaye Mahakama ya Rufaa baada ya kushindwa, hukumu bado haijatolewa.

(iii) Sula la Familia moja kuuziwa nyumba mbili limepatiwa ufumbuzi baada ya kubainika kuwa wanafamilia hao wametalikiana kisheria na kila mmoja amebaki na nyumba yake.

(iv) Nyumba 27 zisizokuwa za Serikali Kuu zilizouzwa kwa watumishi wa Umma, Serikali imefuta mikataba ya nyumba 16 za Halmashauri zilizoko Mikoani na zilizobaki za Serikali za Mitaa, *SIDO*, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, Serikali imewasiliana na Taasisi husika na majadiliano yanaendelea ya namna ya kupata ufumbuzi wa tatizo hilo.

(v) Serikali imefuta mikataba ya nyumba 35 zilizokuwa katika maeneo nyeti ya Serikali na ambazo hazikupaswa kuuzwa.

(vi) Serikali imetoa orodha kama Azimio lilivyotaka kuonyesha ni akina nani waliouziwa nyumba hizo na ziko wapi.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati:-

(i) Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu imepitia na kujadili kwa kina Taarifa ya Uteklezaji wa Azimio hili na kuridhika na majibu ya Serikali hasa kwa hatua ambazo zimekwisha kuchukuliwa za kurejesha nyumba zilizouzwa bila kuuata utaratibu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizo. *(Makofi)*

(ii) Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kesi zenye utata na zilizoko mhakamani ili muafaka upatikane mapema kwani kuendelea kuwa na kesi za aina hii zitatia dosari kazi nzuri iliyokwishafanyiwa na Serikali. Aidha, Wizara ikamilishe mapema majadiliano na taasisi ambazo nyumba zake ziliuzwa kwa watumishi wa umma mapema iwezekanavyo.

(iii) Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauiri Serikali kuwa jitihada ziendelee za kuwalipa fidia mapema wale wote walioathirika na zoezi hili la uuzwaji wa nyumba za Serikali ambao nyumba walizouziwa, zimerejeshwa Serikalin. Hii itaepusha usumbufu kwa watumishi hao na familia zao.

(iv) Mheshimiwa Spika, kati ya watumishi waliouziwa nyumba za Serikali, 3131, wamemaliza kulipa madeni yao, watumishi 443 wanaendelea kulipa kulingana na mikataba yao na watumishi 75 walishindwa kulipa na kufutiwa mikataba yao. Kamati inaishauri Serikali kuwa kupitia Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)*, orodha ya wadaiwa iwe ikipitiwa mara kwa mara na kuwakumbusha wahusika kulipa madeni yao kwa wakati ili kuepusha usumbufu.

(v) Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nzuri ya ukusanyaji wa madeni na fedha za mauzo ya nyumba, Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo wa ujenzi wa nyumba hizo hasa kwa watumishi wa kada ya kati na ya chini kwani tatizo la nyumba bado ni kubwa sana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho: Napenda kukushukuru wewe binafasi kwa kunipa nafasi hii na kuwashukuru pia Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge, Katibu Mkuu Miundombinu, Mhandisi Omar Abdallah Chambo, pamoja na watalaam wote wa Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati na hasa kwa mchango wao mkubwa wa kupitia na kujadili utekelezaji wa Azimio hili hadi kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuwatambua wajumbe wanaounda Kamati ya Miundombinu kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Alhaj Mohamed H. Missanga – Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne K. Malecela – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Ali Al-Qassmy, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Dr. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Alhaj Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Sigsfrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Mwaka Abdullahman Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa na mimi Godfrey W. Zambi ninayesoma taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashilillah, Katibu wa Kamati ya Miundombinu Bi. Justina M. Shauri na Bw. Angumbwike L. Ng'wavi kwa kuandaa taarifa hii. Aidha, naomba niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa bidii na utendaji wao mzuri katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati imeridhishwa na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika kutekelza Azimio la Bunge na baada ya kutoa ushauri kama nilivyokwishaeleza, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali Taarifa hiyo kama ilivyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, mwakilishi wa Mwenyekit wa Kamati ya Miundombinu kwa kuwasilisha taarifa hiyo. Ilikuwa muiamue kwa kuijadili, lakini sikupokea ombi lolote la kuijadili. Kwa hiyo, wajibu wangu ni kuamini kwamba imepokelewa pia imekubaliwa. Namalizia tu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara hii na watendaji wote. Kwa kweli taarifa nilizokuwa nazipata wakati hadi wakati, ni jinsi gani Mheshimiwa Waziri na watendaji wake walivyokuwa wanashirikiana kwa kina. Hawakuwa wanaficha jambo lolote na ndio maana kazi imeisha vizuri kwa masikilizano mazuri. Nakupongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mzingira, Mheshimiwa Ndugai. Kabla hajaanza kusema, naomba radhi Waheshimiwa Wabunge, jana ilipotokea hitilafu ya umeme, imeunguza kifaa muhimu katika mashine yetu ya uchapaji kule *Hansard*. Kwa hiyo, imeshinidikana kupatikana nakala za kutosha kwa Wabunge, imebidi zitolewe kwa mtindo huu wa zamani na wanaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo, baadhi ya taarifa hizi pengine baadhi yenu mtakuwa hamjaziona, lakini hapa mezani ipo hii aina ya zamani. Lakini *Hansard* wanaendelea kufanya jitihada ili tuweze kuwa tunazipata wakati tunaendelea.  Naomba radhi kwa hilo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilipata fursa ya kusikiliza taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Azimio la Bunge la Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii lililowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 10 Julai, 2009 wakati wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Mwezi Aprili, 2008 katika Mkutano wa 11, Bunge lako Tukufu lilijadili namna bora ya kuboresha Tasnia ya Uwidanji wa Kitalii na ilifuatiwa na kupitishwa kwa Azimio la Bunge kuhusu ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii na bei zake lenye maagizo makuu matatu kama ifuatavyo:-

(i) Kuondoa kasoro zote zilizojitokeza ili kuongeza mapato na kuweka uwiano, uwazi na usawa katika ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji.

(ii) Serikali ianze mchakato wa kugawa upya Vitalu vyote vya Uwindaji nchini kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Bunge.

(iii) Serikali iweke mkakati maalum wa kukamilisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa 14 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano uliofanyika tarehe 30 Januari, 2009, Bunge lilipitisha Azimio kwa kutoa maamuzi yafuatayo ambayo yalilenga kuboresha Tasnia ya Uwindaji wa Kitalii:-

(i) Kuhusiana na barua ya Wizara ya Maliasili na Utalii Kumb.HD.204/401/100 ya tarehe 16 Januari, 2009 inayoongeza muda wa umiliki wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii kwa Makampuni ya Uwindaji kwa kipindi cha miaka mitatu (2010 – 2012) kwamba ifutwe mara moja barua hiyo kwa kuwa inakwenda kinyume na Azimio la Bunge.

(ii) Kwa kuzingatia hali halisi ilivyo sasa na kwa kuwa Wizara ilichelewa utekelezaji wa Azimio la Bungee, Bunge liliazimia kwamba ushauri wa kitalaam uzingatiwe ili Vitalu hivyo viwe vimekamilika na kupewa kwa wawindaji kwa maana ya ugawaji mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ilijadili kwa kina yaliyoko katika taarifa hiyo ya utekelezaji ambayo inahusu zaidi maslahi ya Taifa na uboreshaji wa Tasnia yenyewe ya Uwindaji wa Kitalii kwa kuzingatia malengo ya kuboresha ushiriki na uwezeshaji wa Watanzania katika Sekta ya Uwindaji. Uwazi na uwajibikaji, kuongeza mapato, kuweka mfumo bora wa ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii, ufuatiliaji na uthamani, usimamizi na uendeshaji wa uwindaji pamoja na ushiriki wa Tanzania katika Soko la Utalii Duniani.

Mheshimiwa Spika, Ushauri wa Kamati: Katika kutekeleza Azimio hilo la Aprili, 2008, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kamati imeridhishwa na namna Wizara inavyotathmini na kupanga vitalu katika madaraja kulingana na ubora kupitia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *(TAWIRI).* Kamati imeona suala hili ni muhimu sana kwa uhifadhi endelevu wa wanyamapori wetu. Kwa kuzingatia ukubwa wa kazi na unyeti wa suala hili, mpaka sasa *TAWIRI* wamekagua maeneo ya Vitalu kwa kiwango cha asilimia 80. Kamati inasisitiza kwamba kazi hii imalizike kwa muda uliopangwa ambao ni Desemba, 2009.

Mwezi Januari, 2009 Bunge lilipitisha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009 ambayo inatoa nafasi ya kukata rufaa kwa mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa kugawa vitalu. Kwa kuwa sheria mpya itaanza kutumika kwa makadirio, ifikapo Desemba, 2009, Kamati inasisitiza kanuni za sheria mpya zikamilishwe haraka iwezekanavyo na zilenge kuweka mfumo bora wa ugawaji wa vitalu na usimamizi thabiti wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Bunge lilipitisha Sheria ya Uhifadhi ambayo natoa nafasi ya kukata rufaa kwa mtu yoyote ambaye hataridhika na uamuzi wa kugawa vitalu. Kwa kuwa Sheria mpya itaanza kutumika ifikapo mwezi desemba mwaka 2009 Kamati inasisitiza kanuni za Sheria mpya zikamilishwe haraka iwezekanavyo na zilenge kuweka mfumo bora wa ugawaji wa vitalu na usimamizi thabiti wa wanyama pori.

(c) Kamati inakubali kuwepo kwa kipindi cha mpito ili kuwezesha mabadiliko yanayotakiwa kufanyika kwa uhakika hasa kwa upande wa Watanzania kuajiriwa kama wawindaji bingwa kwenye kampuni za uwindaji kulingana na mwongozo wa Sheria mpya ya wanyama pori ambapo *training* ya wawindaji bingwa inaanza mwaka huu kwenye chuo cha Mweka. Katika miaka miwili watakuwa tayari wamepatikana.

Mheshimiwa Spika, aidha kamati inasisitiza Wizara kuhakikisha vitalu vya uwindaji vinagawiwa kama muda ulivyopangwa si zaidi ya *October 2010.*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Azimio la Bunge la tarehe 30 Januari, 2009 Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira iliweza kupitia na kujadili kwa undani utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Bunge tarehe 30 Januari, 2009 Kamati imebaini faida na hasara za utekelezaji wa maamuzi hayo na inashauri ifuatavyo:-

(a)Kamati inashauri suala la kutekeleza uamuzi wa Bunge la kufuta barua kumbukumbu namba HD. 204/ 401/100 tarehe 16 Januari, 2009 uangalie upya na Bunge kutokana na kwamba Wizara inaweza kushtakiwa Mahakamani na kulazimika kulipa fidia kubwa takribani dola milioni 300 au zaidi. Ambayo kimsingi inaweza kuhatarisha Bajeti ya Serikali na uwezekano wa wawindaji kufungwa na hivyo Serikali kukosa mapato kutoka katika sekta hii.

(b) Kwa kuwa Serikali ilishatoa tamko kupitia kwa Waziri wake wa Maliasili na Utalii alipokuwa safarini Nchini Marekani Rhino mnamo Januari, 2009 kwa wadau wa tasnia ya uwindaji wa kitalii ambao ni *Safari Club International* kwamba

Serikali inakamilisha Sheria mpya hapa nina nukuu maneno ya Mheshimiwa Waziri: “Serikali inakamilisha Sheria mpya itakayosimamia biashara ya uwindaji na hivyo kuhahakisha Biashara haisimami Serikali imetoa kipindi cha mpito”, Mwisho wa kunukuu. Kamati inashauri uamuzi wa kufuta barua hiyo utazamwe upya ili kuinusuru Serikali na kutoheshimika Kimataifa.

(c) Utekelezaji wa Azimio la Bunge kama lilivyo haukutoa fursa kwa wawekezaji kuweka mikakati ya kuuza safari. Pia Serikali haitaweza kusimamia kikamilifu tasnia ya uwindaji ili kufikia malengo ya kukusanya zaidi ya bilioni 28 kwa mwaka ambazo ndio malengo yalivyo.

(d) Kwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii inapewa fedha kiasi za Miradi ya Maendeleo kwa sehemu kubwa uendeshaji wa Mapori ya Akiba unategemea fedha zinazotokana na uwindaji wa kitalii. Kamati imeona uamuzi huu wa kufuta barua hiyo au kufunga vitalu vya kuwinda utaiweka Serikali na Wizara katika hali ya hatari hasa kusababisha ukosefu wa fedha za kulinda maliasili zilizopo dhidi ya ujangili.

(e) Malipo ya wafanyakazi, na kuathiri kabisa utendaji wa Hifadhi zetu za Taifa hasa *Game Reserves*.

(f) Chini ya Sheria ya uhifadhi wa wanyama pori ya mwaka 2009 pamoja na kanuni zake kipindi cha mpito kitatoa fursa kwa wawekezaji wapya ambao tumesisitiza wengi wao wawe ni Watanzania na wa zamani kuweka mikakati ya kujitangaza kikamilifu kimataifa, kuajiri wafanyakazi, kutoa mafunzo kwa wawindaji bingwa kwa mujibu wa Sheria ambayo tumeweka. Kampuni mpya zitakazoingia zitakuwa na ubia wa Watanzania kwa kuzingatia asilimia isiyopungua 25%. Kwa mujibu wa Sheria tuliyopitisha Januari mwaka huu hapa Bungeni na utaratibu wa Uwiano wa Wawindaji bingwa kuwa nusu kwa nusu. Katika ya wawindaji bingwa wageni na wawindaji bingwa wa Tanzania tofauti na ilivyo sasa ambapo ni Mtanzania mmoja kwa wageni watano. Taratibu hizo za uwindaji bingwa nusu kwa nusu itahakikisha kwamba tasnia hii ya uwindaji wa kitalii siku za usoni itamilikiwa na Watanzania hivyo kuendelea kuiweka tasnia hii mikononi mwa Watanzania zaidi kama Bunge lilivyoelekeza. *(Makofi)*

(g) Kipindi cha mpito kitatoa fursa ya mabadiliko bila kuleta athari kwa Serikali na wadau kwa tasnia ya uwindaji wa kitalii kwa maneno mengine *smooth transion*. Pia kutatoa mwanya wa kuondokana na makubaliano ya mwaka 1994 kati ya Wizara na TAHOA ambayo ni Umoja wa Wawindaji wa Kitalii ambayo yalipaswa kutumika kwamba uwindaji uendelee hivihivi hadi mwaka 2014 hii itaondoa uwezekano wa makampuni kwenda mahakamani kudai fidia. Kwa kuwa sasa makubaliano ni kwamba mwaka 2012 itakuwa ndiyo mwisho na siyo mwaka 2014.

(h) Tanzania itajiweka katika Mazingira mazuri ya kurudisha Imani, kuongeza ushindani na kuimarisha tasnia ya uwindaji wa kitalii katika soko la dunia huku biashara hii ikiendelea kukua na kuendeshwa zaidi na Watanzania. Aidha usimamizi na utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kama vile *SITES* utaimarika.

Mheshimiwa Spika, hitimisho baada ya kuwasilisha taarifa hii napenda kuwatambua kwa majina wajumbe wa Kamati ya ardhi maliasili na mazingira waliohusika katiaka kusikiliza na kupitia majibu ya Azimio hili la Bunge kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wenyewe ni Mheshimiwa Job A. Ndungai - Mwenyekiti Kamati na Mheshimiwa Hassan Rajab Khatibu – Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Arch. Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa William V . Lukuvi, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Mariamu Mfaki, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Philimon Ndesamburo, Mheshimiwa Mariamu Kasembe na Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Juma S. N’hunga, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salum, Mheshimiwa Ali Hamis Seif, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Jackob Shibiliti, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Lucy Mayenga na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

Mheshimiwa Spika naomba kuwasilisha na nainaunga mkono utekelezaji wa Serikali wa Azimo la Bunge kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii.

Kwa maana hiyo naomba Bunge lako Tukufu, lipokee taarifa hiyo ya Serikali na kuikubali kama ni ushauri unaofaa. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti Mheshimiwa Job Ndugai. Waheshimiwa wabunge katika hoja hii nimepata wachangiaji wawili Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na Mheshimiwa Felix Mrema. Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Danieli Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa heshima zote nakuomba utumie kanuni zako. Mimi nina jambo ambalo limenigusa nalo ni kuhusu miundombinu. Nilikuwa naomba kwa sababu kanuni zinaruhusu kutoa fursa hiyo unipe fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba zoezi la kuuza nyumba limekwenda vizuri na mimi nalipongeza, lakini nilikuwa na ombi moja dogo.

**SPIKA:** Ameruhusiwa na Spika, mambo haya naomba tuwe na Demokrasia pana tuwe tunasikilizana. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunilinda. Zoezi hili pamoja na kwamba limekwenda vizuri lakini halikufika kabisa katika Wilaya ya Kasulu nasema hivyo kwasababu zoezi hili halikufanyika kabisa nyumba ziliuzwa kiholela kupita kiasi na katika Wilaya za Kasulu na Kibondo. Sasa mimi langu lilikuwa ni ombi tu wala sina jambo kubwa nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu utume *team* yako waende Kasulu.

Mheshimiwa Spika, Kasulu hata nyumba ya *OCD* aliuziwa Msomali anayefanya biasahara ya nyama sokoni. Ni mambo ya aibu yalitufika pale lakini kulikuwa hakuna jinsi ya kufanya lakini siyo hilo tu kwa wale mnaoifahamu Kasulu enzi za Ukoloni, Bomani ilijengwa kwenye kilima. Kwa hiyo, kuna *Police Station,* kuna Mkuu wa Wilaya na maeneo ya Utawala halafu wananchi tuliobaki tukawa tuko Bondeni kama unafahamu vizuri pale Kasulu.

Mheshimiwa Spika, sasa zile nyumba zote nyumba ya Hakimu wa Wilaya, Nyumba ya *OCD*, Nyumba ya Mkurugenzi, nyumba ya Ofisa Usalama wa Taifa, zote ziliuzwa tena kwa watu ambao ni watu wa ajabu kabisa. Nilikuwa naomba kwa ruksa yako sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu atume watu wake waende Kasulu, waende Kibondo, wafanye tathimini wajiridhishe ili jambo hili liweze kumalizika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili kwa sababu umenipa nafasi niseme hili la Maliasili. Ni kweli kwasasababu wote tunafahamu taratibu za mikataba ya Kimataifa na mimi nikubaliane na hoja ya Mwenyekiti wa Kamati kwamba jambo hili ukiliparaganyisha sasa hivi litatuondolea *Credibility* katika nchi yetu. Na mimi nilikuwa naomba tukubaliane na hoja iliyotolewa kwamba zoezi hilo waendelee kuli- *administer* vizuri lakini bila shaka huko mbele ya safari wajikite katika kutoa fursa kwa Watanzania zaidi kuliko watu wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga hoja mkono taarifa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa taarifa yako ni nzuri tu kuhusu utekelezaji wa Serikalini na ningeomba wale wote ambao kuna tatizo lina fanana na Kasulu si vibaya kufikisha taarifa Serikalini badala ya kuchangia sasa ili Serikali iweze kulifanyia kazi ipasavyo. Sasa ni Mheshimiwa Felix Mrema.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bila kupoteza wakati nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa ripoti yao, taarifa yao wameiwakilisha hapa asubuhi ya leo na kazi nzuri walioifanya katika kukamilisha taarifa yao.

Mheshimiwa Spika, la pili ni pia niishukuru Serikali kwa kuwa sikivu na kuzingatia yale yote ambayo sisi hapa Wabunge tunayatoa. Baada ya kusema hayo naomba pia nitumie nafasi hii kueleza jambo moja ambalo limetokea nafikiri linahitaji ufafanuzi au maelezo zaidi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa tunajadili mjadala wa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko alihitimisha tulipofikia lile suala la *General tyre*, alihitimisha kwa kuahidi hapa mbele yetu kwamba atahakikisha kwamba anashirikisha wadau wanaohusika na *Generla Tyre*. Ikiwa ni pamoja na wafanyakazi, *Management* pamoja na Mwenyekiti wa Bodi hiyo ya *General Tyre* aliyemteua na pia aliahidi kwamba atamshirikisha na Mbunge kwa hatua zozote zitakazofuata baada ya wao kukamilisha wanachotaka kufanya.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya jana nimepata taarifa kutoka Arusha kwamba Serikali imefika pale *General Tyre* na ikaamua kufunga kile Kiwanda, wafanyakazi wamepewa *notice* ya kusimamishwa kazi *notice* ya mwezi mmoja. Sasa mimi nilikuwa nategemea kwamba haya yote yangefanyika baada ya sisi tulioahidiwa kushirikishwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni nini kinachoendelea. Maana kama ushirikishwaji haupo wa kikamilifu ndio inatufikisha sisi mahala tukafikiria kwa nini iendeshe kwa namna hii ni kwa sasababu Serikali iliahidi kutushirikisha. Na sisi tulikuwa tunangojea kushirikishwa ili na sisi tupate nafasi ya kutoa mawazo yetu na ushauri wetu wa nini kifanyike ili tufike huko wote ambapo tunapotaka tufike kwenye suala la *General tyre* sasa inatupa wasiwasi na linatusumbua.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Serikali ilichukulie hilo na itupatie maelezo ya nini kinachoendelea na kama wanataka kupata ushauri kutoka kwetu watupe nafasi ya sisi kuwashauri kifanyike kwa ajili ya kupata muafaka kwenye suala hili la *General Tyre*. Ahsante sana Mheshimiwa Spika. *( Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na wewe naona umechomekea lakini nadhani Arusha wamesikia. Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla nadhani hakukuwa na mgogoro mkubwa kati ya yale ambayo Serikali ilipendekeza na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ndio limekuja kufikia mwisho. Wamefupisha kidogo ule muda wa mpito kuhusu leseni za uwindaji. Kwa hiyo, nadhani jambo hilo nalo limepokelewa bila mgogoro wowote.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. Naishukuru Wizara kwa kufanya kazi vizuri na Kamati yetu na mimi nasema mara kwa mara kukiwa na uwazi na kupeana taarifa mambo haya yote tunaweza kuyaamua bila migogoro. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ili atupe taarifa zake hizo mbili KIWIRA na *RICHMOND.*

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU TAARIFA YA SERIKALI ILIYOWASILISHWA BUNGENI TAREHE 25 JULAI, 2009 JUU YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU MKATABA BAINA YA TANESCO NA RICHMOND DEVELOPMENT COMPANY LLC

**MHE. WILLIMU H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Utangulizi. Awali ya yote nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Serikali iliyowasilishwa Bungeni tarehe 25 Julai, 2009 juu ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Mkataba baina ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC.*

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Serikali ilitanguliwa na Taarifa mbili zilizowasilishwa Bungeni na Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda, tarehe 28 Agosti, 2008 na tarehe 11 Februari, 2009 ambazo zililitaarifu Bunge kuwa utekelezaji wa maazimio 12 kati ya 23 yaliyotolewa na Bunge ulikuwa umekamilika. Maazimio hayo 12 ni: Nambari 4, 6, 10, 13, 15, 16, 17, 18, 19, 21, 22 na 23.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu katika maoni yake kuhusu taarifa hizo mbili za awali za Serikali, ilitamka wazi kuwa utekelezaji wa maazimio matatu kati ya hayo 12 (yaani Azimio namba 10, 15 na 18) haukukamilika ipasavyo kama ifuatavyo:-

(a) Azimio Na. 10. Mheshimiwa Spika**,** Azimio hili linatamka kwamba: “Gavana wa Benki Kuu pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wachunguze kwa makini uhalali wa malipo ya ziada (US$ 4,865,000) yaliyofanywa kwa *Dowans Holdings A.S.* iliyorithi majukumu ya *Richmond Development Company* na kuwachukulia hatua waliohusika na uzembe huo”.

Utekelezaji wa Serikali ulikuwa:- “Wizara ya Fedha na Uchumi na Benki Kuu ya Tanzania wamechunguza na kuona kuwa malipo ya US$ 4,865,000 yaliyolipwa kwa Kampuni ya *Dowans Holdings S.A.* iliyorithi majukumu ya *Richmond Development Company LLC.* ni halali. Malipo hayo yalilipwa tarehe 2 Februari, 2007 ikiwa ni gharama za ndege za usafirishaji wa mitambo ya kukodi ya umeme wa dharura, baada ya kupokea Invoice Na. EFD786675.

Uchunguzi unaonyesha kuwa, taratibu zote za malipo zilifuatwa na malipo yalifanywa baada ya kuhakikiwa na *TANESCO*, Wizara ya Nishati na Madini na HAZINA baada ya kupata ushauri wa kisheria kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba yanawiana na mkataba husika.”

Mheshimiwa Spika, maoni ya kamati**.** Uhalali wa malipo ya US$ 4,865,000 unaoongelewa na Serikali hauendani kabisa na maudhui ya Azimio hilo la Bunge. Kufuatana na barua ya tarehe 28 Desemba, 2007 ya Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Juma Reli, kwa Katibu wa Bunge, *Dowans Holdings S.A.* ilipokea malipo yafuatayo kutoka Serikalini:

(a) US$ 15,348,299.00 (tarehe 2 Januari, 2007);

(b) US$ 4,865,000.00 (tarehe 2 Februari, 2007);

(c) US$ 13,813,469.00 (tarehe 25 Mei, 2007);

(d) US$ 1,534,830.00 (tarehe 9 Julai, 2007).

Jumla ya malipo yote ni US.$ 35,561,598.00.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Azimio la Bunge ni kwamba Barua ya Dhamana ya Benki *(LC)* yenye thamani ya US$ 30,696,598.00 ilifunguliwa *CRDB Bank Ltd.* kwa ajili ya *Dowans.* Lakini *Dowans* walilipwa jumla ya US$ 35,561,598.00! Azimio la Bunge linataka wale walioidhinisha malipo ya ziada ya US$ 4,865,000.00 kwa *Dowans,* nje kabisa ya Barua ya Dhamana ya Benki, wachukuliwe hatua kwa uzembe. Hivyo basi, Kamati ya Nishati na Madini inaona kuwa Azimio hilo bado halijatekelezwa!

(b) Azimio Na. 15. Azimio hili linatamka kwamba: **"**Utaratibu wa kuteua Wakurugenzi na Makamishna katika Wizara kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara zao unazua mgongano wa kimaslahi na kudhoofisha usimamizi pamoja na uwajibikaji, hivyo Serikali iupige marufuku mara moja".

Utekelezaji wa Serikali ulikuwa: "Ni kweli kuwa huenda katika baadhi ya maeneo, mfumo huu wa uteuzi wa Wakurugenzi au Makamishna kuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma unaweza kuwa na matatizo. Hata hivyo, baada ya Serikali kuzingatia Azimio hili, imeona pia kwamba, zipo pia faida za baadhi ya Wakurugenzi au Makamishna kuwa Wajumbe wa Bodi hasa katika kusaidia kutoa msimamo na ufafanuzi wa Sera na Mipango mbalimbali ya Serikali.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali inaona ni vyema utaratibu huo uendelee lakini kila Bodi itaangaliwa kipekee. Pale itakapodhihirika kuwa ni kwa maslahi ya Taifa kuwateua baadhi ya Wakurugenzi au Makamishna kuwa Wajumbe katika baadhi ya Bodi, Serikali itafanya hivyo kwa maslahi ya Taifa letu."

Mheshimiwa Spika, maoni ya kamati. Majibu haya ya Serikali yanafungua upya mjadala na ubishi nje ya Bunge, jambo ambalo si sahihi kisheria na Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Azimio linapopitishwa Bungeni, linabeba maamuzi ya pamoja ya Wabunge na viongozi wa Serikali. Pale ambapo Azimio linazua wasiwasi wa kutotekelezeka, fursa zipo za kutosha kujenga hoja na kufanya marekebisho kabla ya kupitishwa kwake na siyo kuanzisha malumbano nje ya Bunge baada ya Azimio kupita.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Nishati na Madini katika maoni yake mwezi Februari 2009 ilitamka kuwa pale ambapo ushiriki wa Makamishna na Wakurugenzi utaonekana ni muhimu, basi washiriki kama Wajumbe *Ex-Officio.* Kamati yangu haioni sababu kwa Serikali kuingia kigugumizi kuhusu suala hili. Ushiriki wa Wabunge kwenye Taasisi za Fedha kama Wajumbe wa Bodi ulipoelezwa kuwa unaleta mgongano wa kimaslahi kwenye semina ya kimataifa ya Kamati za Bunge za usimamizi wa masuala ya fedha Jijini Dar es Salaam mapema mwaka huu, Serikali ilichukua hatua mara moja kuwaondoa Wabunge kwenye Bodi zote za Taasisi za Fedha. Kwa hiyo, Kamati inazidi

kusisitiza kuwa Azimio hili halijatekelezwa, hivyo litekelezwe bila kuvuta miguu. *(Makofi)*

(d) Azimio Na. 18"Wamiliki wa *Richmond Development Company LLC.* na *Richmond Development Company (T) Ltd.* wafunguliwe kesi ya jinai mara moja kwa udanganyifu na ujanja wa kuiibia Serikali". Utekelezaji wa Serikali ulikuwa**:**

*Naeem Gire,"* alifikishwa mahakamani Jijini Dar es Salaam tarehe 13 Januari, 2009 na kusomewa mashtaka matano.

- Kutoa hati za uongo kwa Taasisi mbalimbali za Serikali

- Kughushi hati ya wakili kuonyesha kuwa ameidhinishwa kisheria na Bwana Mohamed Gire ambaye ni mmiliki wa *Richmond Development Company LLC.* ya Texas, Marekani kufanya kazi za kampuni hiyo nchini;

- Kutoa taarifa za uongo kwa Bodi ya Zabuni ya Shirika la Umeme Tanzania na watumishi wa umma kwamba kampuni ya *Richmond* ina uwezo wa kuzalisha umeme nchini na pia kushawishi waipendekeze kampuni hiyo kupewa zabuni hiyo;

- Kutoa taarifa za uongo kwa Wajumbe wa Timu ya Majadiliano ya Serikali kwamba kampuni hiyo ina mitambo yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa Megawati 105.6 ili kuwezesha kupendekezwa kuzalisha umeme huo; na
- Kutoa Hati za uongo kuonyesha kuwa Bwana MohamedGire alimwidhinisha kufanya biashara za kampuni ya *Richmond* nchini Tanzania."

Mheshimiwa Spika, katika Maoni yake kuhusu Taarifa ya Serikali ya mwezi Februari 2009, Kamati ya Nishati na Madini ilionesha kutoridhika kwake na utekelezaji wa Azimio hili kwa kuwa Mmiliki wa Kampuni hizo mbili na ambaye alisaini Mkataba kati ya *TANESCO* na *RICHMOND*, Bwana Mohamed Gire, aishie *Houston, Texas,* Marekani hajatafutwa, hajakamatwa na wala hajafikishwa mahakamani. Aliyekamatwa na kufikishwa Mahakamani ni mdogo wake, Naeem Gire, ambaye hana hisa hata moja ndani ya *Richmond Development Company LLC.* iliyosaini mkataba na *TANESCO.* Hivyo, Azimio hili halijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya rejea hiyo ya utekelezaji uliopita wa baadhi ya maazimio ya Bunge, Kamati yangu ilielekeza macho yake kwenye taarifa ya utekelezaji iliyowasilishwa mezani tarehe 25 Julai, 2009.

**"**Maudhui ya Maazimio Namba 1 na 2 yanafanana kwa sababu yalielekeza Serikali kufanya mapitio upya ya sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kwa lengo la kuiboresha na kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* nguvu

zaidi za udhibiti na uwezo wa kuchukua hatua pale Sheria na Kanuni zinapokiukwa, badala ya kutoa ushauri tu kama ilivyo sasa. Vilevile, Maazimio haya yalitaka *PPRA* isiwajibike Wizara ya Fedha ambayo nayo ni Taasisi ya Ununuzi (*procuring entity*), badala yake iwe chombo huru".

"Mwezi Februari 2009, utekelezaji wa serikali ulikuwa: Serikali ililifahamisha Bunge kuwa Mapendekezo ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, Sura ya 410 ulikuwa umekamilika; na kinachosubiriwa sasa ni kukamilisha mchakato wa kuuwasilisha Muswada huo Bungeni"

Mheshimiwa Spika, maoni ya kamati. Kamati ya Nishati na Madini imezingatia hatua zilizochukuliwa na kuridhika na utekelezaji wa Maazimio hayo. Kutokana na umuhimu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, Kamati inahimiza Muswada huo uletwe katika Mkutano wa Bunge wa 17 kwa kupitishwa. *(Makofi)*

(e) Azimio Na. 3 "Mikataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC* (uliyorithiwa *Dowans Holdings S.A.)* na ile kati ya *TANESCO* na *IPTL, SONGAS, AGGREKO* na *Alstom Power Rentals* ipitiwe upya mapema iwezekanavyo kama ambavyo Mikataba ya Madini ilivyopitiwa upya na Serikali. Bila kufanya hivyo, mzigo mkubwa wa gharama za umeme utawaelemea Wananchi na kushindwa kufikia azma ya Serikali ya maisha bora kwa kila Mtanzania".

(i) Mikataba kati ya *TANESCO* na *AGGREKO*, Utekelezaji wa Serikali: *Alstom Power Rentals, IPTL*, na *Richmond Development Company LLC* uliorithiwa na ***DOWANS.***

Kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyoeleza katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Mikataba baina ya *TANESCO* na *AGGREKO na ALSTOM POWER RENTALS*, muda wa mikataba hiyo ulikwisha mwaka 2008 na Serikali kupitia *TANESCO* ilikataa kuongeza muda wa mikataba hiyo.

Kwa upande wa Mikataba baina ya *TANESCO* na *IPTL* na *Richmond Development Company* uliorithiwa na *Dowans Holdings S.A.*, mikataba hii bado ina mashauri mbalimbali ambayo yapo mahakamani. Kwa kuwa Kanuni ya Bunge Na.64(1)(c) inazuia Bunge kuzungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama. Taarifa ya Serikali kuhusu Mikataba hii, itatolewa baada ya mashauri hayo kukamilika.

(ii) Mkataba Baina ya *TANESCO* na *SONGAS* Kama itakavyokumbukwa mwezi Februari, *2009* Utekelezaji wa Serikali ilitoa maelezo ya kina kuhusu historia ya Mradi wa *Songo Songo. (Makofi)*

Katika maelezo hayo, Serikali ililifahamisha Bunge kuwa, mwaka 2005 kulifanyika marekebisho katika Mikataba ya Mradi wa Songo Songo kwa lengo la kuweka kipengele cha kuiruhusu Serikali/*TANESCO* kubadili mtaji uliotumika kwenye kuweka mitambo ya MW 70 kuwa mkopo, pale fursa ya *Refinancing* itakapojitokeza kwa lengo la kupunguza kiwango cha gharama ya *Capacity Charge*.

Maelewano hayo yapo katika Mikataba kati ya Serikali/*TANESCO*, Benki ya Dunia, Benki ya Wawekezaji wa Ulaya (*European Investment Bank)* na *SONGAS.*

Mheshimiwa Spika, Kutokana na Benki zilizotajwa hapo juu kuhusika katika mchakato wa upatikaji wa fedha za Mradi, ilikuwa ni muhimu kwa Serikali kuelewana na wakopeshaji hao kabla ya kujadili na *SONGAS* kuhusu urekebishaji wa Mkataba wa Mauziano ya Umeme *(Power Purchase Agreement –PPA)* kati ya *SONGAS* na *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, Hii ni kwa sababu fedha za *Refinancing* ya Mradi ni zile zinazotokana na kiasi kilichosalia kutoka kwenye Bajeti ya mkopo wa ujenzi wa Mradi wa Songo Songo ambacho ni Dola za Kimarekani Milioni 42 (takriban shilingi Bilioni 56.7). Kiasi hiki cha fedha ndicho kilichokubalika kwa ajili ya kulipia *Refinancing* kwa lengo la kupunguza *Capacity Charge.*

Mheshimiwa Spika, Chimbuko la maelewano hayo ni kufuatia uhaba wa umeme uliojitokeza mwaka 2006, ambapo *TANESCO* iliwaruhusu *SONGAS* kuweka mitambo ya MW 70 kwa njia ya dharura, wakati Serikali inafanya majadiliano na Wakopeshaji ili kupata mkopo wa masharti nafuu. Kwa kuzingatia hali hiyo, *SONGAS* walitumia fedha zao za Mtaji (*Equity)* kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 56 kuweka mitambo miwili yenye uwezo wa MW 70**.**

Maridhiano yaliyokuwepo ni kwamba, pale fursa ya *Refinancing* itakapojitokeza, mtaji huo utageuzwa na kuwa mkopo wenye masharti nafuu ili kupunguza kiwango cha *Capacity Charge*. Fedha zitakazotumika ni zilezile za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani milioni 42 ambazo Serikali ilikopeshwa kwa riba nafuu isiyozidi asilimia 0.7.

Hadi sasa, Wadau husika, ikiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, *TANESCO, SONGAS* na Serikali (Wizara ya Nisharti na Madini, Wizara ya Fedha na Uchumi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa *Power Purchase Agreement (PPA)* irekebishwe kufuatia kutekelezwa kwa Refinancing ya Mradi itakayoruhusu kupungua kwa *Capacity Charge* ya umeme wa SONGAS inayolipwa na *TANESCO* kwa Dola za Kimarekani Milioni 1.0 kwa mwezi.

Hivyo, kutokana na unafuu huo tulioupata, kwa miaka 15 iliyobaki ya muda wa *Power Purchase Agreement* unaoanzia Julai 2004, ni sawa na punguzo la Dola za Kimarekani Milioni 180 (takriban shilingi Bilioni 243 kwa kutumia kiwango cha sasa cha kubadilisha fedha za kigeni cha shilingi 1,350 kwa Dola ya Kimarekani). Hivi sasa *TANESCO* na *SONGAS* wanakamilisha maaandalizi ya nyaraka muhimu zinazohitajika

na Benki ya Dunia ili malipo hayo yaweze kufanyika. Matarajio ya Serikali ni kukamilisha zoezi hili mwezi Agosti 2009 ili unafuu wa mzigo wa kiwango cha *Capacity Charge* wa punguzo la Dola za Kimarekani milioni 1.0 kwa mwezi uanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Pia imekubalika kuwa, *Escrow Account* iliyokuwa imefunguliwa kwa ajili ya kinga kwa SONGAS kwa uwekezaji wao wa awali sasa haihitajiki. Mkataba huo wa *Escrow* utafutwa na fedha kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 4.5 zilizo katika Akaunti hiyo kurudishwa Serikalini. Wizara ya Fedha na Uchumi ipo katika mchakato wa kufunga na kuhamisha fedha hizo kutoka kwenye *Escrow Account.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, Hadidu za Rejea pana zaidi zinatayarishwa na mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA)* kwa aajili ya kuandaa *Model Power Purchase Agreemet (MPPA)* ambazo zitatumika katika majadiliano ya Mikataba ya Sekta ya Umeme itakayotekelezwa na Wazalishaji wa Umeme Binafsi Nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni ya kamati. Kamati ya Nishati na Madini inazitambua harakati hizo za Serikali na wadau husika kufanikisha "*refinancing*" ya mradi itakayoruhusu kupungua kwa "*Capacity Charge*" ya umeme wa *SONGAS* inayolipwa na *TANESCO.* Kwa kuwa matarajio ya Serikali ni kwamba zoezi hili la "*refinancing*" litakamilishwa mwezi Agosti, 2009, Kamati itaendelea kufuatilia suala hili kwa karibu ili kuhakikisha kuwa tunaipunguzia nchi mzigo mkubwa uliopo wa gharama za umeme. Aidha, Kamati yangu itaendelea kufuatilia zoezi la kuandaa *Model Purchase Agreement (MPPA)* ili mwongozo huo wa mikataba uanze kutumika mapema iwezekanavyo.

(f) Maazimio Na. 5, 7, 9 na 14. "Maudhui ya Maazimio haya yanafanana kwa sababu yaliitaka Serikali kuwawajibisha Watumishi wote wa Umma waliohusika katika Majadiliano ya Machakato mzima wa Mkataba baina ya *TANESCO* na *RICHMOND,* pamoja na wale wa TAKUKURU waliofanya uchunguzi wa suala hili".

Utekelezaji wa Serikali "Katika kushughulikia suala hili, Watumishi wa Umma waliohusika katika Majadiliano ya Mchakato mzima wa Mkataba baina ya *TANESCO* na *RICHMOND,* wakiwemo Maafisa Waandamizi 3, yaani Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati na Madini na aliyekuwa Katibu Mkuu,

Wizara ya Fedha na Uchumi walifunguliwa Mashtaka ya Nidhamu kwa mujibu wa Kanuni Namba 49 (1) ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002.

Vile vile, Watumishi wa TAKUKURU waliofanya Uchunguzi kuhusu suala hili nao walifunguliwa Mashtaka ya Nidhamu kwa Mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002. Watumishi wote hao waliwasilisha utetezi wao kwa Mamlaka zao za Nidhamu.

Katika Taarifa ya Serikali iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Februari, 2009 ilielezwa kuwa, Mamlaka za Nidhamu zilizokuwa zinashughulikia hatua za Nidhamu dhidi ya Watumishi wa Umma waliohusika katika mchakato mzima wa Mkataba baina ya *TANESCO* na *RICHMOND*, pamoja na wale wa TAKUKURU, waliofanya uchunguzi wa suala hili zilikuwa zimekamilisha uchambuzi wa maelezo binafsi ya utetezi yaliyotolewa na kila Mtumishi aliyeshiriki. Hadi sasa Mamlaka zao za Nidhamu zimekwishatoa Maamuzi kwa kila Mtumishi wa Umma kama ifuatavyo:

(i) Kwa mujibu wa mchanganuo wa Mashtaka, utetezi na maamuzi dhidi ya Mashtaka ya Nidhamu, imebainika kuwa wapo Watumishi watano (5) ambao walifunguliwa Mashtaka ya Nidhamu yasiyowahusu. Watumishi hao wamefutiwa mashtaka hayo kwa sababu hawakuhusika moja kwa moja kwenye mchakato wa Zabuni hii.

(ii) Watumishi 16 wa Umma waliohusika katika mchakato wa Zabuni hii, wakiwemo wale waliokuwa kwenye Kamati ya Wataalam na Majadiliano *(GNT),* pamoja na wale wa TAKUKURU, baada ya Mamlaka zao za Nidhamu kupitia utetezi walioutoa kwa kuzingatia Kanuni Na. 49 (1) ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma, imebainika kuwa, hakuna ushahidi wa wazi uliopatikana ambao unadhihirisha kuwa Watumishi hao wa Umma hawakutumia utaalam na uzoefu wao kuishauri vizuri Serikali kwenye Mchakato mzima wa Zabuni ya umeme wa dharura.

Kwa mantiki hiyo, Mamlaka zao za Nidhamu zimeridhika na utetezi uliotolewa na Watumishi hao na kuwaondolea Mashtaka. Hata hivyo, Watumishi hao wamekumbushwa kuhusu umuhimu wa kuwa makini na thabiti zaidi katika utaekelezaji wa majukumu wanayopewa na Serikali.

(iii) Aidha, Mamlaka za Nidhamu zimetoa onyo kwa Watumishi Wawili (2) ambao baada ya kupitia utetezi wao ilibainika kuwa, hapakuwepo na umakini wa kutosha katika kushughulikia suala hili. Watumishi hao ni aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Majadiliano ya Wataalam, Bw. Singi Madata na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU), Bw. Edward Hosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Bwana Singi Madata, katika utetezi wake, Mamlaka yake ya Nidhamu imeona kuwa, kwa mujibu wa maelekezo ya kazi waliyopewa ya kusaili Makampuni nane (8) yaliyoomba Zabuni ya kufufua Umeme wa dharura alieleza kuwa kazi hiyo ilifanyika kwa muda wa siku mbili.

Pamoja na utetezi huo, Mamlaka yake ya Nidhamu imeona kuwa muda huo ni mfupi na usingewezesha Kamati husika kukamilisha kazi hiyo kwa umakini na ufanisi, pamoja na kuwepo kwa hali ya dharura ya upungufu wa Umeme Nchini.

Hata hivyo, hapakuonekana dalili za mazingira ya rushwa wakati wa kufanya kazi hiyo**.** Hivyo, Mamlaka yake ya Nidhamu imetoa onyo kwake kwa kutokuwa mwangalifu katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Bw. Edward Hosea, Mamlaka yake ya Nidhamu imeona kuwa ni kweli kwamba Sheria ya TAKUKURU kwa wakati huo ilikuwa na mapungufu katika kubaini viashiria vya rushwa kwenye mchakato wa Zabuni, ambavyo ndivyo Wataalam wa TAKUKURU walijikita kufanya uchunguzi wao.

Hata hivyo, ingawa Sheria ilikuwa na mapungufu kwa upande mmoja, Mamlaka yake ya Nidhamu, imebaini kuwa, wakati wa kupitia Taarifa ya uchunguzi iliyofanywa na Wataalam wake wa TAKUKURU na kabla ya kuitoa kwa Umma, alipaswa kujirishidha kwamba, kweli Kampuni ya *Richmond Development Company* LLC. ilikuwa imeandikishwa hapa Nchini au hapana**.**

Mheshimiwa Spika, aidha, Taarifa yake haikuonyesha bayana tofauti baina ya Makampuni ya *Richmond Develoment Company* LLC, *RDEVCO,* na *Richmond Development Company (RDC),* jambo ambalo lilijitokeza baadaye wakati Kamati Teule ya Bunge ilipofanya uchunguzi wake.

Hivyo Mamlaka yake ya Nidhamu imeamua apewe onyo kwa kutokuwa makini katika uchambuzi wa Taarifa zinazowasilishwa kwake na Wataalam wake, ili kuleta usimamizi wenye tija ndani ya TAKUKURU.

(iv) Kuhusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye Mamlaka yake ya Nidhamu ni Mheshimiwa Rais, kwa maelezo tuliyonayo ni kuwa, hakuna kosa lolote la Kisheria au Kinidhamu ambalo alilifanya katika nafasi yake kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mchakato mzima ulioipa ushindi Kampuni ya *Richmond Develoopment Company LLC* katika Zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura.

(v) Kwa ujumla, hadi sasa, uchunguzi wa vyombo vya Dola kuhusu Watumishi wate wa Umma waliohusika na suala hili, unaonyesha kuwa, hakuna Mtumishi yeyote aliyeonekana kutenda kosa la Jinai lenye kuhitaji kuchukuliwa hatua za Kisheria.

Hata hivyo, kwa kuwa yapo Mashauri mbalimbali yanayoonedelea Mahakamani dhidi ya Wamiliki na Wawakilishi wa Kampuni ya *RICHMOND*, iwapo Mtumishi yeyote wa Umma atatajwa na Watuhumiwa hao, kwamba alihusika, katika Makosa ya Jinai, Serikali haitasita kumfikisha Mahakamani*”*.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati, katika Maoni yake mwezi Februari 2009 Kamati yangu iliishauri Serikali kutumia Taratibu na Kanuni zilizopo zinazo ruhusu mtuhumiwa kupewa likizo maalum, kusimamishwa kazi katika kipindi cha uchunguzi au kubadilishiwa sehemu ya kazi, ili kufanikisha zoezi la kuwawajibisha watumishi wote wa

umma waliohusika na kashfa ya *RICHMOND*. Kamati yangu ilisisitiza kuwa hatua hizo siyo adhabu bali mbinu za kiutawala na kiutumishi katika kushughulikia matukio ya ukosaji kiutendaji. Kwa maneno mengine, Kamati ya Nishati na Madini haikufurahishwa na uendeshaji wa zoezi hilo huku watumishi wanaokabiliwa na tuhuma mbalimbali wakiendelea na nyadhifa zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ushauri wa Kamati haukuzingatiwa, utekelezaji wa maamuzi haya ya Bunge umegubikwa na udhaifu wa aina tatu:-

(1) Kwanza, umekiuka Kanuni muhimu ya haki ya asili inayozuia mtu kuwa Hakimu kwenye suala linalomhusu.

(2) Pili, utaratibu huu umetawaliwa na upendeleo wa bayana kwa kuwasafisha watendaji wote bila kuwatofautisha. Hivyo kuzua maswali, mfano: Kwa maelezo ya Serikali ni kwamba hakuna Mtendaji aliyekosa, sasa kwanini wanapewa onyo?

(3) Tatu, Mamlaka za Nidhamu zinawekwa juu ya chombo cha Kikatiba cha kuisimamia Serikali, yaani Bunge, hivyo kuruhusu Mamlaka hizo za kiutendaji kukosoa na kubadilisha maamuzi halali ya Bunge kinyume cha misingi ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Wanasheria waliobobea katika masuala ya Mikataba ya Kimataifa wa Kampuni ya *REX ATTORNEYS*, Wanasheria ambao walitafutwa na Serikali yenyewe wamegundua mapungufu yafuatayo:-

(i) Utaratibu mzima wa manunuzi ya huduma ya umeme na kuingia Mkataba na *Richmond Development Company LLC* ulikiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004;

(ii) Kutokana na ukiukwaji huo, Mkataba baina ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC* haukuwa halali na hauna nguvu ya Kisheria; na,

(iii) Vile vile, hata kama Mkataba husika ungekuwa halali, uhamishaji (*assignment*) wa Mkataba huo kutoka *RDEVCO* badala ya Richmond *Development Company LLC* kwenda *DOWANS HOLDINGS S.A.* na hatimaye *Dowans Tanzania Limited* haukuwa halali. Je, ni kitu gani kinaifanya Serikali leo ipuuzie ushauri na maoni ya wataalam na kushindwa kuona kosa wala wakosaji kwenye suala hili?

(iv) Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Taarifa yake kwa Bunge ya tarehe 28 Agosti, 2008 alimwelezea Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa ni (nanukuu); “Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala yote ya Sheria za Nchi. Hivyo, ana wajibu mkubwa wa kuishauri Serikali

katika maeneo ambayo anaona yanakiuka Sheria, Taratibu na Kanuni za Nchi.”

(v) Vile vile katika taarifa hiyo, Waziri Mkuu anamwelezea Wakili wa Serikali Bwana Donald Chidowu ambaye alikuwa ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Majadiliano (*GNT*) kuwa Mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(vi) Kwa Serikali kugeuka na kuona Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kutohusika kabisa na suala hili, ni kuendekeza kutowajibika katika Ofisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na mapungufu yote haya tuliyoyaainisha, Kamati ya Nishati na Madini inayarejesha tena Serikalini Maazimio Na. 5, 7, 9, Na 14 kwa utekelezaji unaozingatia misingi ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 8 na 14 “Maudhui ya Maazimio haya yanafanana kwa sababu yaliitaka Serikali iwawajibishe Viongozi wenye dhamana ya kisiasa waliokuwa Mawaziri wa Wizara ya Nishati na Madini ambao ni Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha Mbunge na Mheshimiwa Nazir Karamagi Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Serikali; “Kama ilivyoelezwa katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge kwamba vyombo vya dola vilikuwa vinaendelea na uchunguzi wake kuhusu suala hili. Hadi sasa, suala hilo halijafikia tamati kwa kuwa linashughulikiwa zaidi na Taasisi ya Kuzuia na Kudhibiti Rushwa (TAKUKURU) pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini”.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati; Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji wa maazimio haya mawili.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 11 “Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 1995 *(The Public Leadership Code of Ethics Act)* ifanyiwe marekebisho makubwa ili kudhibiti utaratibu unaoonekana wa kawaida sasa wa Viongozi Waandamizi wenye dhamana ya kisiasa kuendelea na biasharaza zao binafsi wakiwa madarakani, jambo ambalo lina mgongano wa kimaslahi. Serikali ianze rasmi maandalizi ya majadiliano ya kina kuhusu suala hili ndani na nje ya Bunge kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali.”

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Serikali: “Kikundi Kazi (*Task Force)* kilichoundwa na Serikali kushughulikia Azimio hili, kimefanya Utafiti na kupitia upya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995, ili kubaini upungufu uliopo na kuainisha mapendekezo yatakayowasilishwa Serikalini. Vile vile, Kikundi Kazi hicho kimepokea maoni ya Wananchi yatakayosaidia kuweka utaratibu wa Viongozi Waandamizi wenye dhamana ya Kisiasa na Watendaji wa ngazi ya juu katika Utumishi wa Umma kutenganisha shughuli zao za Biashara na Uongozi ili kuondoa mgongano wa Kimaslahi katika utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, Hivi sasa, Kikundi Kazi kimeanza zoezi la kuandaa mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995, kwa madhumuni ya kuwezesha Viongozi na Watendaji Waandamizi kutenganisha shughuli za Biashara na Uongozi wa Umma. Zoezi hili likikamilika, mapendekezo ya Kikundi Kazi yatawasilishwa Serikalini kwa uamuzi na hatimaye Muswada wa Sheria husika kuwasilishwa Bungeni".

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati; Serikali iendelee na mchakato huo na kwamba Kamati inasubiri utekelezaji wa Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 12: "Serikali ijiepushe kadri inavyowezekana na utaratibu wa kutumia Mawakala katika ununuzi wa Umma na kuhakikisha kuwa Wizara zote zina taarifa za bei halisi za mahitaji yao kila wakati ili kujiepusha na mchezo wa kawaida wa Mawakala kupandisha bei mara mbili au zaidi ya bei halisi."

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Serikali: "Kama Serikali ilivyoahidi tarehe 17 Februari 2009, Kikao cha Kazi cha Makatibu Wakuu kilifanyika ili kupitia Taarifa kuhusu Mapendekezo ya Mtaalam Mwelekezi aliyepewa kazi na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*) ya kuandaa Mfumo wa ununuzi wa pamoja (*Common Used Items*) pamoja na kuandaa utaratibu wa kupata takwimu za Bei Dira za bidhaa mbalimbali (*Indicative Price)* kutoka kwa Wazalishaji wa bidhaa na mitambo na huduma.

Mheshimiwa Spika, Katika kikao hicho, utaratibu mpya wa Ununuzi wa Pamoja utakaotumiwa na Taasisi za Umma katika Manunuzi ya Bidhaa na Huduma ulijadiliwa na kukubalika uanze kutumika mara moja. Kutokana na maelekezo hayo, *PPRA* imekamilisha maandalizi ya utaratibu utakaotumiwa na Taasisi za Umma katika ununuzi wa pamoja wa bidhaa na huduma; na vile vile, takwimu za Bei Dira za bidhaa na huduma zimeandaliwa**.** Hivi sasa *PPRA* inaendelea na zoezi la kuandaa Bei Dira za kazi za Kandarasi za Ujenzi na Huduma za ushauri ili ziende sambamba na utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma mara Marekebisho hayo ya Sheria yatakapokamilika na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na hatua hiyo, *PPRA* imeagizwa kuwajengea uwezo Wataalam wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Manunuzi Nchini (*GPSA*) ili kuwawezesha kusimamia na kutekeleza kwa ufanisi utaratibu mpya wa Manunuzi ya Umma. Tayari *PPRA* imeshaanza zoezi hilo kwa kutoa mafunzo kwa Wakuu wa Taasisi za Umma kuhusu matumizi ya utarabu huo mpya. Mafunzo hayo yalifanyika Mjini Morogoro tarehe 16 na 17 Aprili, 2009 ambapo Washiriki kutoka Taasisi za Umma 52 walishiriki.

Mafunzo ya aina hayo yataendelea kufanyika katika mwaka 2009/2010 kwa Taasisi za Ununuzi zilizobaki".

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati; Kamati imeridhika na utekelezaji unaoendelea wa Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 13: “Serikali izihusishe Kamati za Kudumu za Bunge kwenye hatua za awali za maandalizi ya Mikataba mikubwa ya muda mrefu ya kibiashara ili kuondokana na utaratibu uliopitwa na wakati kwamba Mikataba ya Kibiashara ni siri hata kwa walipa kodi wenyewe. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa, Kamati zote za Bunge zinapitia Mikataba mikubwa ya muda mrefu ya kibiashara chini ya sekta zao ili kuliondolea Taifa mizigo isiyo ya lazima”.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Serikali: “Katika Taarifa za awali, Bunge lilifahamishwa kuwa Serikali imekubali kimsingi kuwa Mikataba Mikubwa ya Kibiashara na ya Muda Mrefu baina ya Serikali na wawekezaji au wafanyabiashara itakuwa inawekwa kwenye Maktaba Maalum ya Bunge illi Waheshimiwa Wabunge watakapotaka kuiona Mikataba hiyo, wapewe kwa utaratibu utakaokubalika.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Serikali kuhusisha Kamati za Bunge kupitia Mikataba Mikubwa ya Kibiashara na ya Muda Mrefu. Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge, imeunda Timu ya wataalam ambao wanaandaa utarabu muafaka wa kufanya utafiti katika Mabunge ya Nchi za Jumuiya za Madola ili kupata uzoefu zaidi utakaosaidia katika utekelezaji wa suala hili. Pindi Wataalam watakapokamilisha kazi hii, Bunge litaarifiwa”.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati; Kamati imeshindwa kuelewa ni utafiti gani ambao Serikali inaendelea kuufanya mpaka sasa, kwani katika utafiti uliofanywa na Kamati kwa kipindi kifupi utaratibu huu upo katika nchi nyingi kama Ghana, Nigeria, Norway na Afrika ya Kusini.

Kwa mfano, Nchini Afrika Kusini kazi ya kujadili mikataba mikubwa ya kibishara, kimsingi ni kazi ya Serikali, lakini Mikataba hiyo haipati nguvu ya kisheria na kuanza kutumika bila kuridhiwa na Bunge na Baraza la Majimbo (*National Council of Provinces*). *(Makofi)*

Hivyo basi, ili mchakato wa kuridhia uwe rahisi Waziri mhusika huzieleza Kamati husika za Bunge na Baraza juu ya lengo, maudhui, faida na changamoto zilizopo kabla ya kuanza mazungumzo/majadiliano *(negotiations)* ili kupata maoni ya jumla ya Kamati ya kuzingatiwa katika majadiliano hayo. Kabla ya majadiliano kufika mwisho, Serikali hurudi tena kwenye Kamati hizo kutoa picha halisi ya majadiliano na kupata ushauri wa mwisho wa Kamati hizo. Kamati hukaribisha wadau wa sekta husika, katika hatua hiyo. Aidha, Kamati zinaweza kushauri, kuukubali au kuukataa Mkataba kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia mfano tajwa hapo juu, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utekelezaji wa azimio hili katika muda muafaka ili kuepuka madhara tuliyoshuhudia katika mikataba iliyoingiwa kati ya Mashirika ya Serikali na Kampuni za Nje ya Nchi. Suala la msingi hapa ni kuweka utaratibu mzuri wa mawasiliano na ushiriki wa Kamati husika ambao hauingilii maeneo ya utendaji.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 20 “Serikali iendeshe uchunguzi maalum ili kubaini ukweli kama Taarifa rasmi ya TAKUKURU iliyotoa matokeo ya uchunguzi kuhusu mchakato wa *Richmond* ilikataliwa na kuharibiwa na kutolewa nyingine na kama jalada halisi linalohusu Kampuni ya *Richmond* lililokuwa *BRELA* liliharibiwa na kuwekwa lingine kwa lengo la kuficha ukweli.”

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Serikali: “Kamati ya Vyombo vya Dola imekamilisha uchunguzi wake kuhusiana na suala hili; na imebainika kuwa, sikweli kuwa Taarifa rasmi ya TAKUKURU iliyotoa matokea ya uchunguzi kuhusu mchakato wa suala la Richmond ilikataliwa na kuharibiwa na kutolewa nyingine kwa lengo la kuficha ukweli.

Vile vile, Taarifa ya Kamati ya Vyombo vya Dola inaonyesha baada ya upelelezi na uchunguzi wa kina kufanyika wameridhaka kuwa jalada halisi la *Richmond* lililokuwa *BRELA* halikuharibiwa na wala hakukuwa na jalada lingine lililowekwa kuficha ukweli wa jambo hili”.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati; Kamati inaridhika na taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho, Kamati inapenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mbunge, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora na Mheshimiwa Adam K. Malima, Mbunge, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa kushirikiana na Kamati katika kujadili suala hili na hivyo kuweka msingi mzuri katika ripoti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na Wabunge wengine ambao walikuja kwenye vikao vya Kamati kutuunga mkono. Michango yao imewezesha kutoa Taarifa katika muda mfupi. Naomba niwataje Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William H. Shellukindo - Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe - Maakamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Faida M. Bakar Mjumbe, Mheshimiwa Asha M. Jecha Mjumbe, Mheshimiwa Yahya K. Issa Mjumbe, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mjumbe, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya Mjumbe, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa Mjumbe na Mheshimiwa Rita Louis Mlaki Mjumbe.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Mohammed H. J. Mnyaa Mjumbe, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi Mjumbe, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela Mjumbe, Mheshimiwa Omar Shekha Mussa Mjumbe, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe Mjumbe, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa Mjumbe, Mheshimiwa Charles N. Mwera Mjumbe, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko Mjumbe, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa Mjumbe, Mheshimiwa Christopher O. Ole Sendeka Mjumbe, Mheshimiwa

Mohammed S. Sinani Mjumbe, Mheshimiwa Lolensia J.M. Bukwimba Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwisho namshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashillilah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Vile vile nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Stella Bwimbo, kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, mimi nachanganyikiwa nataka mwongozo wako, moja ya majukumu ya Wabunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali, inapofikia hatua Wabunge wanaweka Azimio, lakini moja ya jukumu lake ni kuishauri Serikali na wameishauri Serikali haikuuchukua ushauri ule, naomba unisaidie maana yake hapa kuna *contradicting statements* Ahsante.

**SPIKA**: Mheshimiwa malizia sasa. (*Kicheko*)

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, *contradiction* ninayoipata mimi ni kwamba sisi tunaishauri tu Serikali, tukiweka Azimio bado kazi yetu ni kuishauri siyo kuiamuru, Je, inapofikia hatua Serikali imeshauriwa kama Katiba inavyosema haikukubali.

Mheshimiwa Spika, naomba unisaidie ni kipengele kipi tutawabana na sisi tunawashauri tu.

**SPIKA**: Ahsante sana ni swali la maana sana. Mchakato wenyewe ndiyo huu huu, kilichoanza ni kwamba, kuna mambo fulani yalitendeka Serikalini ikaundwa Kamati Teule ya Bunge, ikachunguza na ikatoa ushauri wake kwa maazimio yale yenye vipengele 23. Kwa hiyo, ushauri ulijikita katika mambo 23 kuhusu *Richmond*, yalipopelekwa Serikalini tumeendelea kuwa tunapata taarifa za utekelezaji kama *progress report* ambayo ni haki yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa imefika hatua Kamati ya Uongozi iliamua kwamba suala hili la *RICHMOND* tulimalize mwaka huu lisiwe linaendelea kama mengine. Kwa hiyo, nilimwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu nikiweka wazi kwamba tunahitaji kwa faida ya Taifa letu jambo hili tuliweke mwisho. Serikali ilete maelezo kwamba mmefikia wapi sasa na hayo mnayotujibu yaturidhishe kwamba ndiyo utekelezaji wa yale tuliyoazimia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilipoyapata kwa mujibu wa Kanuni nikayapeleka kwenye Kamati zinazohusika. Kwa mfano hili la *RICHMOND*. Uwindaji likaenda Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Uuzwaji wa nyumba likaenda Kamati ya Miundombinu.

Utaona kwenye yale mawili ya kwanza, Miundombinu kuhusu Uuzwaji wa Nyumba za Serikali na Ugawaji wa Vitalu Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kiasi kikubwa wameridhika. Kwa hiyo, hayo mawili yamefungwa ukiacha haya mambo ya kufuatilia kiutendaji tu kama kule Kasulu na sehemu zingine ambazo labda bado kuna mambo ambayo hayakukaa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, katika hili Bunge kupitia Kamati yake ya Nishati na Madini imegundua kwamba utekelezaji wa baadhi ya mambo haukuwa wa dhati, ni haki yetu kusema kama Bunge kwamba, utekelezaji huo siyo wa dhati, sasa hilo ndilo tunaliamua leo. Kwa hiyo, kutakuwa na wachangiaji, Mwenyekiti amewasilisha taarifa ya Kamati akikosoa baadhi ya vile vipengele 23 namna vilivyotekelezwa na hususani kinachoelekea kuwa ni ulegevu katika kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi mbali mbali.

Waheshimiwa Wabunge, tafsiri ya Kamati ambayo ndiyo nitaomba muiamue ni kwamba bado kuna kazi ya kufanywa, na hilo ndiyo tunawaambia Serikali na wengine mtachangia hapa. Baada ya hapo nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini afafanue ama wengine wote walioko Serikalini wanaopenda kuchangia lakini tayari nina jina la Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa ufafanuzi.

Hatima yake sisi tutaamua na baadhi ya maamuzi yanaweza kuwa ni magumu sana hatuna ukomo wa kitu cha kuamua hapa, tukiendelea kuridhika kwamba Serikali tu haitaki kufanya yanayoazimiwa na Bunge ambayo mtu yeyote mwenye busara analiona ni jambo la haki kutendeka, tunaweza tukafika mbali zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mnanielewa, kwa sababu Serikali inawajibika kwa Bunge kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hilo siyo tatizo kubwa sana, sidhani kama tutafika huko. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani sasa mmeelewa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, ninao wachangiaji 12, kwa suala la *RICHMOND* kabla ya kuwataja naomba niwatambue wageni waliopo hapa, wapo wageni wangu wanaotoka Jimbo la Peramiho kwa rafiki yangu mpendwa sana Askofu Mkuu Nobert Mtega wa Jimbo la Songea, tunasaidiana na tunaziunga mkono jitihada za kanisa Katoliki kujenga hospitali Kitunda Dar es Salaam, nadhani ni Jimbo la Mheshimiwa Naibu Waziri Mahanga. Wageni hawa ambao ni wageni wangu na wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge wa Peramiho ni kama ifuatavyo, Sister Josee Chiwinga karibu sana Sister. Ndugu Lwembu Henjewele na Vitalis Aloyce nadhani wamesindikizwa na wenyeji Masista kutoka hapa Dodoma naomba nao wasimame, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Dar es Salaam inapata bahati kubwa, mimi nazungumza kwa sababu nitakuwa mgeni rasmi wa kwanza katika kuzindua uchangishaji wa mfuko ambao utaunga mkono jitihada za marafiki walioko nje wanaotaka kujenga hospitali kubwa sana pale Jimbo la Ukonga Kijiji cha Kitunda.

*Fund rising* ya kwanza itafanyika mwezi wa tisa kule Peramiho na baadhi yenu ninao wafahamu nitawaandikieni barua kwa sababu najua moyo wenu wa kuchangia mambo haya, tutakwenda pamoja Peramiho tukaziunge mkono jitihada hizi kwa sababu hospitali kubwa ikijengwa Dar es Salaam inakuwa kama hospitali nyingine ya Rufaa tena na kwa sababu inaungwa mkono na taasisi ambayo ina uwezo basi hili ni jambo zuri. Nawashukuru sana wageni wetu tupo pamoja katika kutekeleza hilo na msalimieni sana Baba Askofu Mkuu, Mheshimiwa Nobert Mtega.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Capt. Mstaafu John Chiligati ni Ndugu Thadeous Mwakilema, Msajili wa Hati Kanda ya Kati, karibu sana, Ndugu Grace Mwagimba Afisa Usajili na Ndugu Grace Paschal, Afisa Ardhi Msaidizi. Karibuni sana naomba wote msimame ili Wabunge waweze kuwaona.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama Hati zenu zinakwama kwama hawa hapa, sasa ndiyo wakati wa kuwaona karibuni sana. Yupo mgeni wa Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kindondoni, ambaye ni Mwanamuziki na Mwanaharakati Bwana Mrisho Mpoto.

Mjomba karibu sana, ahsante sana kijana una kipaji maalum na nashukuru unakuwa Balozi mwema mpaka nje ya nchi nakutakia mema na tutakuwa nawe katika kueneza Sanaa ya Tanzania. Anazo kanda zake zinauzwa hapo nje na moja maarufu sana ambayo mimi nimeinunua jana na nimeisikiliza asubuhi inasema, nikipata nauli Mjomba. Hii ni moto kweli, nadhani Waheshimiwa mjitahidi kuinunua. (*Makofi/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wanafunzi 40 kutoka Chuo cha Ualimu cha Don Bosco Selesian Seminari, Dodoma nadhani na viongozi wao, karibuni sana. Tunashukuru sana mmejitolea leo siku ya jumamosi, vijana wengine wanafanya mambo ya kipuuzi tu, lakini ninyi mmekuja kujifunza mambo ya Bunge. Mungu awaongoze katika shughuli zenu, tunawahitaji sana na tunawatakia mema katika masomo yenu.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni na huo ndiyo mwisho wa matangazo kwa sasa ili wageni wapate fursa ya kuweza kama wakihitaji kufanya shughuli zingine.

Wachangiaji wa hoja ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Willibroad Peter Slaa, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii,

Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Mtangi na sasa hivi nimepata wawili, Mheshimiwa Magalle John Shibuda na Mheshimiwa John Cheyo.

Waheshimiwa Wabunge, nitaanza kumwita Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, nitawachanganya si katika mpangilio huu nilioutaja.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii ya mwanzo kabisa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Kamati ya Nishati na Madini, au kuchangia taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Mkataba baina ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC*, sambamba na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa sana kusema ni kuridhika kwangu kwa kazi nzuri sana inayofanywa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Mara tu baada ya kuchanguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake ya kufungua Bunge hili, Rais alielezea pamoja na mambo mengine mambo makubwa mawili ambayo nitayagusia.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala zima la mgawanyo wa madaraka kwa mihimili yetu mitatu, lakini jambo linalohusiana na haya ya leo aligusia suala la mikataba na kusema kwamba Serikali ya awamu ya nne itajitahidi kupitia mikataba hiyo na kuona kwamba mikataba yote inayoingiwa na iliyokwisha ingiwa inakuwa ni kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mikataba iliyoingiwa na ambayo imezua mazungumzo mengi na umeingiwa na Serikali ya awamu ya nne ni huu mkataba wa *RICHMOND*. Lakini ninachotaka kulihakikishia Bunge lako, Watanzania na dunia ni juu ya imani yangu kuhusu kauli ya Rais katika suala zima la kuona kwamba mikataba hii inakuwa ni kwa manufaa ya nchi na si kwa manufaa ya wachache.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu ni mtu mwadilifu kwa kiwango cha kupigiwa mfano na bahati nzuri mwenyezi Mungu amemjalia Mke wake ambaye ni mama yetu Salma, ambaye siyo mtu wa makuu, ni mwadilifu na siyo mtu anayezunguka zunguka kutafuta vijisenti. Unapokuwa na Rais ambaye ni mwadilifu na mchapakazi na anayeipenda nchi yake kwa dhati na Mungu akamjalia Mwenzake ambaye yuko hivyo hivyo. Haiwezekani katika kinywa cha mtu yeyote makini eti tu kwa sababu ya propaganda za kisiasa, akataka kusema hata haya yanayoendelea leo yana mkono wa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba hakuna mkono wa Rais katika kashfa hii ya *Richmond*, tumeichunguza, waliohusika, walitajwa na namna yeyote Rais hahusiki na angehusika asingeruhusu Tume iundwe, asingeweka mambo bayana, asingechukua hatua na kuridhia Waziri Mkuu kujiuzulu na kuvunja Baraza lake la Mawaziri. Kwa hiyo, tunapolijadili jambo hili tujadili wazi tukijua kwamba tunaendelea na mkakati wa kutekeleza maelekezo ya Rais ya kupambana na vita dhidi ya ufisadi na yeye akiwa ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa vita hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwamba sasa suala la *RICHMOND* makosa yalifanyika au hayakufanyika si jambo la kubishaniwa tena, katika taarifa ya Waziri Mkuu ya Agosti, Serikali ilitafuta mabingwa wa mikataba ya kimataifa kampuni ya *REX ATTONEYS* ili kuchunguza kama kulikuwa na ukiukwaji wa sheria na uvunjaji wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda, alisema kwamba kampuni ya *REX ATTONNEYS* ilibaini pamoja na mambo mengine kwa ruhusa yako naomba kunukuu:

"Kwamba utaratibu mzima wa manunuzi ya huduma ya umeme na kuingia mkataba na *RICHMOND Development LLC* ulikiuka sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004. Hii ni kampuni ya watalaamu ambao ni mambingwa wa mikataba ya kimataifa iliyotafutwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya (B) inasema kutokana na ukiukwaji huo Mkataba baina ya *TANESCO, RICHMOND Development LLC* haukuwa halali na hauna nguvu ya kisheria, wanasema hawa mabingwa wa mikataba ya kimataifa ambao wamelipwa kwa fedha ya walipa kodi wa Tanzania na wakaleta taarifa na Waziri Mkuu wetu kwa kuwa ni mtu mwadilifu na muwazi akaja kuisoma hapa mwezi Agosti, 2008.

Mheshimiwa Spika, (C) Hata kama mkataba huo husika ungekuwa halali uhamishaji wa mkataba huo kutoka *RDEVCO* badala ya *Richmond Development Company* kwenda *Dowans Holding SA* na hatimaye *Dowans Tanzania Ltd.* haukuwa halali. Inasema, kwa kuzingatia mapungufu hayo yaliyobainishwa katika mkataba huo, Serikali iliamua kusitisha huduma za *Dowans Tanzania Ltd.* kuanzia Agosti Mosi, 2008".

Mheshimiwa Spika, kwamba Mkataba wa *RICHMOND* ulikuwa ni mkataba halali uliofuata taratibu au haukufuata hili si jambo la kubishaniwa tena, ni jambo dhahiri kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Waziri Mkuu mwezi Agosti, 2008 akirejea ushauri wa watalaamu mabingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali ya tarehe 24 Julai ambayo ndiyo iliyopelekea Kamati ya Nishati na Madini kutoa maoni pamoja na Serikali kukiri kufanyika kwa makosa, kuwepo kwa mapungufu hayo, bado Serikali haisemi wakosaji ni akina nani inakwepa. Kuwa na kosa bila mkosaji huwezi kusema mkataba huu umeingiwa ni batili halafu unasema hakuna mkosaji. Kwa utaratibu tu wa kiutumishi mamlaka zao za nidhamu ziliwachaji wale wahusika 16 japokuwa mchakato wenyewe wa kuwachaji mimi mwenyewe naona una utata, utata wake uko wapi?

Mamlaka ya Nidhamu ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini ni Katibu Mkuu Kiongozi. Mamlaka ya Nidhamu ya Mkurugenzi Mkuu wa *PCCB* tunatarajia

yataandikiwa barua na Katibu Kiongozi kuwa Mteule wa Rais. Sasa na yeye Katibu Mkuu wa Nishati na Madini anawaandikia hawa wengine ambao wako chini yake. Wewe mwenyewe mtuhumiwa halafu unawatuhumu na hawa wengine, bado wote mko Ofisini. Wewe Mkurugenzi wa *PCCB* unashitakiwa na Katibu Mkuu Kiongozi ujibu tuhuma na wewe unamwandikia Mkurugenzi wa Upelelezi pamoja na wengine wa *PCCB* walioko chini yako na wote mko kazini. Halafu hatimaye ripoti inayokuja ni kama ifuatavyo:- kwamba watumishi hawa wa umma hawakutumia utalaam na uzoefu wao wa kuishauri vizuri Serikali kwenye mchakato mzima wa zabuni ya umeme. Wanasema hakuna ushahidi wa wazi kwa mujibu wa taarifa hiyo ukurasa wa sita.

Lakini wanaendelea kusema kwamba kwa mantiki hiyo, mamlaka zao za nidhamu zimeridhika na utetezi uliotolewa na watumishi hao na kuwaondolea mashitaka. Hata hivyo, watumishi hao wamekumbushwa kuhusu umuhimu wa kuwa makini na thabiti zaidi katika utekelezaji wa majukumu waliyopewa na Serikali. Sasa hapo ndipo taabu inapotokea. Nataka niseme tu Kamati yetu ya Nishati na Madini inachoshauri ni Serikali iwe wazi juu ya jinsi walivyofikia hatua hizi.

Najua Mawaziri wale wawili wanaendelea kuchunguzwa kwa mujibu wa ripoti iliyoko hapa. Lakini sasa kama hao wote watendaji hawakukosea maeneo yake namna peke katika akili za kawaida ukiona kwamba hawa watendaji wanaonekana hawakukosea kama walitoa ushauri wao wa kitalaam maana yake unachokipata wameshauri kwa mujibu wa talaaluma zao lakini kuna mamlaka fulani hapa juu katikati hapa imekataa ushauri wa watalaam. Sasa hapo ndipo Serikali inapotakiwa kuwa wazi. Kama ni Mawaziri wenye dhamana tuambieni, kama kulikuwa na shinikizo kutoka juu kwa Waziri Mkuu tuambieni. Maana mkiendelea kunyamaza hapa inaonekana kama hatuko wawazi kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili halijawahi kumwonea mtu na hatarajii kumwonea mtu. Tulipitisha azimio hapa na maazimio tulipitisha kwenye Bunge hili tukiwepo Wabunge na upande wa Serikali ukiwakilisha. Sasa baada ya kuona yale yote tuliyoyaona leo mkirudi mkakiri makosa yamefanyika, lakini wakosaji hamtaki kusema, tunachotaka Serikali iendelee kuwa wazi, nendeni hatua moja mbele msiwaonee haya maana mkionea haya hawa maana yake mnatafuta mtu wa kumtwisha mzigo. Sasa mtu wa kumtwisha mzigo Bunge limeridhika kuna makosa yamefanyika na ninyi hapa mmeridhika, hatua hamchukui mnaendelea kuwaonea haya watu hao. Hivi mnataka tena tuseme nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachosema, mimi sifikii hatua ya kusema Serikali imekataa, ninachosema kuweni wazi kidogo, chukueni hatua zaidi. Niseme katika jambo linalotutesa wengine tuliochangia jambo hili katika kipindi kilichopita ni kubainisha kwamba jamani watu hawa wachukuliwe hatua. Ndiyo kero inayotugusa wengine huko, kana kwamba sisi tulikuwa tuna mkono tofauti, hili lilikuwa ni Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachotaka kuishauri Serikali ya Chama changu ni kwamba twende mbele zaidi kidogo, tueleze bayana tuwaridhishe Watanzania juu ya

hatua tulizozichukua, tusifunike. Kama kuna watu hawakuhusika, njooni hadharani semeni fulani hajahusika, kama wamehusika watajeni hao.

Mheshimiwa Spika, hii itaweza kutusaidia sana na namna pekee ya kufunga hoja hii ni kuchukuliwa kwa hatua kwa watuhumiwa waliohusika kwenye jambo hili vinginevyo tutaonekana kama hatuko makini kwenye mchakato huu mzima. Mchakato huu umebainisha mambo haya kigugumizi ni kuwawajibisha hao. Sawa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pengine hakuwepo kule, alikuweko mwakilishi wake na mimi namjua Mwanyika ni mtu mwadilifu Mwanyika kama Mwanyika. Lakini hawa aliowatuma huko wakaenda kuboronga na kutuingiza kwenye mikataba hiyo, kwa nini hawachuliwi hatua? Mnapata taabu gani? *(Makofi)*

Mkurugenzi wa *PCCB* aliyefikia hadharini kuitakasa Richmond na kusema mkataba huu ulikuwa ni halali, imebainika si halali, anaendelea kufanya nini hapo? Amerudi hadharani ameitakasa *Richmond Rex Atone* imethibitisha mkataba ulikuwa batili, *PPRA* wametoa ushauri haukuzingatiwa. Mkurugenzi wa *PCCB* anawatakasa, Bunge linasema Mkurugenzi achukuliwe hatua, mnasema amepewa onyo. Amepewa onyo! Umadhubuti, umakini wa kupambana na ufisadi utatiliwa mashaka, chukueni hatua sasa. Msiwaonee haya.

Mheshimiwa Spika, mimi sina lingine, mimi nitaendelea na hili katika kipindi cha uhai wangu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpangilio wangu wasemaji sasa ni kama ifuatavyo:- Atafuatia Mheshimiwa Said Nkumba, Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru, lakini vile vile kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati kwa maelekezo mazuri. Kamati kwa kweli imefanya kazi yake vizuri. Kwanza napenda niungane mkono na mwenzangu aliyetangulia.

Lakini vile vile napenda nimwombe Mwenyezi Mungu aniongoze vile vile katika misingi ya haki na bila kumwonea mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipomaliza hoja hii katika vipindi vilivyopita, mimi nilikuwa najua kwamba jambo lile lilikuwa limekwisha na nilikuwa nina hakika kabisa kwamba Serikali itachukua hatua kama jinsi ambavyo Bunge lilivyokuwa limetoa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona ni ajabu sana nilivyosoma magazeti kupokea taarifa mbalimbali na ushawishi wa baadhi ya watu kusafisha watu ambao kwa kweli walidhihirika kabisa kwamba wana makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makosa yako dhahiri, hutakiwi kwenda kwenye Chuo cha Mahakama kubaini makosa ambayo kwa kweli yalijitokeza dhahiri. Haya ndio ambayo

yalipelekea baada ya maamuzi kuchukuliwa kwa mfano kama hakukuwa na makosa, kwa nini Serikali ilichukua hatua ya kuvunja mkataba na *Richmond* na *Dowans*? Lakini kama haitoshi Serikali vile vile ikachukua hatua ya kufuta ile Kampuni ya *Richmond Development Company* ya Tanzania. Haya yote yanadhihirisha kwamba kulikuwa na mushkeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Christopher Ole - Sendeka, taarifa ya Serikali inaonyesha kuwasafisha watumishi, lakini vile vile haishii kuwasafisha watumishi tu, inaelekea kuwasafisha wale wote ambao walituhumiwa juu ya sakata hili la *Richmond*. Hii ni aibu, wananchi wanatusikiliza huko, Watanzania wamefuatilia sana suala hili kuanzia mwanzo mpaka mwisho na mimi nasema Wabunge ambao wako makini hawataweza kurudi nyuma katika jambo la namna hii. Hakuna makosa ambayo yanaweza yakafanyika kama wakosaji hawapo. Wakosaji wapo ndiyo sababu makosa haya yakafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu alijiuzulu hapa wote tukiwa mashahidi na Mawaziri wawili walijiuzulu hapa. Sasa hizi za mwisho za Serikali zinaonyesha kwamba watumishi hawa waliohusika ni safi. Maana yake mnataka kulishawishi Bunge, mnataka kuwashawishi Watanzania kwamba waliohusika ni Waziri na wale Mawaziri Wawili na kwa sababu hiyo sasa inajidhihirisha kwamba hawakuwa na makosa sijui sasa tumshawishi Mheshimiwa Rais afanye maamuzi gani. Jambo hili ni la aibu, haliwezi likajirudia sisi Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tuko makini katika jambo la namna hii.

Lakini vile vile Rais anavyo vyombo vyake vya kuangalia jambo lolote ambalo kwa kweli linasemwa na hasa katika chombo kama hiki cha Bunge. Nina hakika baada tu ya jambo hili kuzungumzwa vyombo hivi vilifanya kazi. Sasa isingekuwa rahisi Mheshimiwa Rais kupokea barua ya Waziri Mkuu, kupokea barua za Mawaziri akakubali haraka. Mimi nina hakika alijiridhisha kwamba yako matatizo. *(Makofi)*

Sasa kama Mheshimiwa Rais alichukua hatua hizo, kwa nini sasa Serikali kwa maana ya ngazi zinazohusika zisiwachukulie hatua wale wote ambao walihusika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie na mambo mawili ya mwisho, la kwanza zimeanza kujitokeza jitihada za kupotosha ukweli, kupotosha hoja, kumchanganya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumesoma baadhi ya magazeti hapa, lakini sisi wote tuko humu. Tunaona baadhi ya watu wakianza kuhamasisha wakianza kusema maneno ambayo kwa kweli yanatupelekea kwa watu ambao hawako makini kuanza kuwa na uhakika kwamba labda kuna watu wengine walihusika ambao hawakutajwa. Napenda nitumie fursa hii kuendelea kusema kwamba mchezo huu hautavumiliwa. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ni mtu safi. Watanzania tunamwamini na Waheshimiwa Wabunge tunamwamini. Huu mzigo ni kwenu mliohusika msimbebeshe mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho habari ya kusafishana. Huwezi kumsafirisha mtu alikwishachafuka. Ukishachafuka umechafuta na huwezi ukatumia maji ya matope unamsafisha mtu, bado huyu akitembea mtaani ataonekana mchafu tu. Hebu tufike mahali sasa tuache. Watanzania hawa hawajafika mahali wakawa ni watu ambao hawaelewi kiasi hicho. Hakuna watu mbumbumbu katika karne hii sasa hivi watu wanafahamu mambo yanavyokwenda.

Sasa tusijidanganye hapa tunaokaa katika hili jumba tukafikiri watu huko nje hawaelewi mambo, wanaelewa! Napenda niwaombeni ndugu zangu ikifika mahali umechafuka kaa utulie. Kutulia na kukaa kimya ni namna nzuri sana ya kujisafisha. Lakini ukiendelea kupigapiga kelele uchafu unaendelea kuwepo na utaendelea kujipaka matope zaidi kuliko pale mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ukishakuwa umechafuka, usiamue kuwachafua na wenzako, hiyo ni dhambi. Mwenyezi Mungu hawezi kukubali! Kwa hiyo, napenda niseme kwamba taarifa hii ya Serikali ya kuwasafisha watu hawa waliohusika mimi siungi mkono na naomba Bunge kwa kweli liseme kabisa katika maazimio yake kwamba haliwezi kuendelea kuunga mkono mambo haya ya kusafishana. *(Makofi)*

Huko nje kuna viongozi wetu watendaji wengi katika ngazi ya Vitongaji, ngazi ya Kata na Wilaya wakifanya makosa tunawachukua hatua: kwa nini katika nafasi hizi za juu hatuchukui hatua? Mimi naomba tutende haki. Mwenye makosa ni mtendaji wa makosa tu, haangaliwi huyu ana cheo kiasi gani, huyu ana nafasi gani, huyu ana mali kiasi gani. Kwa Mungu wote ni sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutokuunga mkono maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Niwakumbushe hoja ni ya Kamati. Nadhani Kamati imejieleza vizuri kwenye hilo. Kwa hiyo, hoja hii siyo ya Serikali. Kwa hiyo, unapounga mkono unaiunga mkono ile ya Kamati.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nianze kwa kuunga mkono hoja ya Kamati. Ninakubaliana na mapendekezo yao na ninapenda kuyaboresha kama nitakavyoeleza huko mbele.

Mheshimiwa Spika, kama ni wakati mgumu katika historia ya Bunge letu nadhani sasa tumeingia kwenye wakati mgumu. Wote tunafahamu nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa Katiba, inafuata sheria zitafuatwa kanuni, zinafuatwa taratibu mbalimbali yaani *decrease* yanafuata maazimio na maazimio ni zaidi ya *decrease* za Serikali. Kwa sababu Bunge ndiyo chombo cha kutunga sheria. Wote tunafahamu kwamba pale ambapo Serikali inaona azimio haliwezi kutekelezeka kama vile ambavyo sheria imepitishwa na Bunge katika hatua ya utekelezaji Serikali inaona haitekelezeki, wanarudi Bungeni kwenda kuleta *amendment* ya sheria ile. Kama ilikuwa maazimio haya hayatekelezeki walipaswa kurejea Bungeni na kueleza kwamba kwa sababu moja, mbili, tatu hayatekelezeki hawakufanya hivyo. Hii ni hatua nzito sana ni hatua ya Serikali kukataa kutekeleza maazimio ya Bunge au kulidhalilisha Bunge.

Mheshimiwa Spika, mambo haya ni mazito. Kwa nini ni mazito? Kwa sababu ndani ya kitabu hiki cha Kamati imeonyeshwa katika maeneo mbalimbali jinsi ambavyo Serikali imeona kwamba kuna ambao hawakutekeleza kwa sababu hawakuweza kufuatilia mambo yao kwa sababu hawakuwa makini. Sasa ukishakubali kwamba Mheshimiwa Hosea hakuwa makini, lakini wakati huo huo Serikali yenyewe inakubali kwamba imeanguka kwenye mtego ule ule wa Hosea wakati anachunguza hakuweza kuchunguza *Richmond* kikamilifu, Serikali yenyewe inaelezwa hapa na Kamati kwamba imempeleka Mahakamani Bwana Naem Gile lakini haikumchunguza yule mwingine ambaye ndiye aliyesaini mikataba.

Serikali yenyewe ndiyo haikuwa makini. Yule ameonywa, nani anaionya Serikali leo? Maana ameonywa Bwana TAKUKURU lakini Serikali ambayo imeanguka kwenye mtego ule ule haijionyi yenyewe na hakuna mamlaka ya kuionya. Hilo ni swali litahitaji kujibiwa huko mbele ya safari.

Lakini imeelezwa na wenzangu kwamba hapa inawezekana ni makusudi ameshtakiwa huyu mmoja na mwingine anaachwa makusudi kwa sababu ya kusafisha ule mtandao wote wa *Richmond*. Sitaki kuingia kwenye hilo kwa hatua hii ya sasa.

Mheshimiwa Spika, nieleze tena kitu kidogo ambacho kimenistua sana, ukishakubali kwamba huyu bwana TAKUKURU aliyechunguza na hakuwa makini unakubali kwamba tatizo ni kubwa na tatizo hilo kubwa kutokana na umakini linaongezewa pia na *Rex Attorney's* ambao waliishauri Serikali kwamba mkataba huu ni batili. Katika utekelezaji Serikali inapata kigugumizi kuwachukulia hatua ni suala zito kabisa kwa sababu siyo Bunge tu limesema lingekuwa Bunge tungesema Bunge limeangalia kwa sababu ni wanasiasa hawakuwa na utalaam. Lakini Serikali imekwenda kuajiri watalaam *Rex Attorney's* wameishauri na hata ushauri wa kitalaam wa *Rex Attorney's* umewekwa pembeni. Suala hilo ni zito kuliko unavyoweza kulieleza.

Mheshimiwa Spika, suala la mikataba ameeleza Mheshimiwa Ole Sendeka na waliotangulia. Mikataba haina uwazi, Serikali siku zote imejaribu kuchenga. Lakini Serikali inapokosa uwazi hata katika majibu yake tatizo linabaki pale pale. Serikali kumbe kwa makudi inakuwa siyo wazi katika mikataba na tumeuliza mara kadhaa hapa. Kwa mfano, Mkataba kwa mfano, ambao dalili zote zinaonyesha taarifa zote zilizoko zinaonyesha ina *20 years time* mradi ule ni mali ya Serikali kwa sababu Watanzania walioko kule ndiyo waliokuwa wamechangia sehemu kubwa na Serikali ndiyo iliyotoa dhamana wawekezaji wameweka kidogo. Rais amesema tutau-*review* tutautazama upya, hautazamwi upya, hautazamwi upya. Lakini Serikali katika majibu haya inazidi kurudi nyuma. Tunashindwa kuelewa katika sura hii tunatakiwa twende namna gani.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wameeleza wakati tunajadili suala la Richmond Serikali ilijiuzulu kwanza kwa mujibu wa katiba na kwa sababu Waziri Mkuu amejiuzulu kwa sababu ya uwajibikaji, lakini leo ukifika mahali kwamba nchi imekosa Serikali kwa siku tatu kwa sababu Serikali yote imejiuzulu kwa sababu ya tatizo hilo, leo wahusika wote wale wanashindwa kuchukuliwa hatua wanasafishwa, wanapewa maonyo

inahitajika sababu ambayo ni lazima ielezwe wazi kwa nini Serikali ilijiuzulu wakati ule? *(Makofi)*

Kuna maswali Kamati inauliza hapa kwamba ni kweli kwamba mkataba umekiuka kanuni, au taratibu hizi zimekiuka kanuni muhimu ya haki ya asili inazuia mtu kuwa hakimu kwenye suala muhimu. Wamejisafisha kwa sababu wamekwenda kujihukumu wenyewe. Wamejihukumu wenyewe kwa sababu kwa kweli hatuna *mechanism* nyingine.

Lakini *mechanism* hakuna, tuna taratibu za kawaida za kuunda *panel* ambazo zingetoa mapendekezo Serikali wamesafishwa na mamlaka ambazo hapa hatuijui na kwa bahati mbaya *process* iliyotumika, utaratibu wa Bunge lako, taratibu zile zingewasilishwa Bungeni leo tungeziona hatuna *details* za namna gani kazi hii ilifanyika.  Ni siri labda ya Serikali au ni nini, lakini Bunge halina siri. Kwa sababu kama tungeweza kujibu hii tungeweza kuangalia *process* iliyofanyika tungesema Serikali imetumia taratibu za haki hatuwezi kuziona kwa sababu hawakuziwasilisha. Kama inasema umetawaliwa na upendeleo wa bayana kwa kuwasafisha watendaji wake.

Mamlaka za Nidhamu zinawekwa juu ya chombo cha kikatiba cha kusimamia Serikali. Sasa ukishafika hapo huna mahali pengine. Labda hapa nieleze kitu ambacho wenzangu labda hawakutaka tu kulifikisha. Au hapa tusijadili na wengine huwa tunapenda kuita *spade a spade*. Rais wa Jamhuri ya Muungano ndio Mkuu wa Serikali. Kiongozi Mkuu anayesimamia *cabinet* ni Rais, aliyekuwa anapitisha haya maamuzi ni Rais wa Jamhuri ya Muungano *(Executive President)* tofauti na nchi nyingine ambapo Waziri Mkuu labda ndiye *President*.

Sasa ukishasema kuna tatizo kwa hawa watendaji na kwa Serikali ni vigumu kumweka Rais nje ya *system* hii kwamba kuanzia kwa Rais hapakuwa namna ya kuweza kusimamia. Sasa mimi sizungumzii Rais kama Rais, namzungumzia Rais kama Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri ambalo limesimamia maamuzi haya. Kwa hiyo, tunapozungumza kwamba Rais ni safi na mimi nakubali Rais kama Rais ni safi kama Mheshimiwa Kikwete. Lakini kama Mwenyekiti wa Baraza ni kwa nini maamuzi haya yametufikisha hapa tulipo? Azimio la Bunge linaachwa Rais na Waziri wake Mkuu wako kwenye *cabinet* wameshindwa kusimamia haya maamuzi? Je, ni kweli kwamba leo tutasema kuna Serikali, Serikali ni nani? Tukienda huko ni lazima tufanye tafsiri ya Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali ni Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri pamoja na watendaji wake wote, hiyo ndiyo *executive*. Hawa kwa pamoja ndio wametufikisha hapa tulipo ambapo maazimio ya Bunge hayakutekelezwa.

*There is no way* kwamba leo hapa kuna mtu atasimama na kuanza kutenga kwamba fulani mzuri, fulani safi, sio safi. Wote katika *system* hii ambao hawakutekeleza kama tulivyomhukumu Waziri Mkuu tunahukumu wote kwamba hawakutekeleza kazi yao. Hapa tusianze kulumbana na kuwayumbisha watu ambao hawajui Katiba ya Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba katika taratibu za kawaida tunapofika mahali kusema kwamba haikutekelezwa, aidha kuna uzembe ndani ya Serikali ndiyo hawakusimamia mambo haya au kuna kulindana kwa wazi ndani ya Serikali jambo linaloathiri Taifa letu na tumeona hapa ni athari ya fedha, sio athari ya kwamba maamuzi hayakutekelezwa, sio athari tu kwamba sheria zimevunjwa, sio athari ya kwamba sheria za manunuzi hazikufuatiliwa. Lakini athari ambayo inatokana na maamuzi kutokusimamiwa kutokutekelezwa Taifa zima linapata athari ya kifedha. Athari moja ni hii Kamati inasema Shilingi bilioni nne ambayo haikupaswa kulipwa, Serikali haikuona hilo?

Lakini la pili ambalo ni lazima tulikubali, unapofikisha Serikali katika sura hiyo na Taifa linapofika sura hiyo, ni nini kinatakiwa kufanyika? Ingekuwa nchi ya wenzetu leo hii Serikali inajiuzulu hapa, Serikali unapoongea maana yake ni Serikali nzima inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, tunarudi kwenye uchaguzi. Huu ndiyo utaratibu wa kidemokrasia. Unapofika Serikali inashindwa kutimiza Azimio la Bunge huna namna tena ya kuanza kugawagawa, Serikali imeshindwa kwa hiyo, tunarudi kwenye uchaguzi wananchi wanaolitupa ridhaa watupe ridhaa upya tutekeleze yale ambayo tuliwaahidi. Huu ndiyo utaratibu wa kawaida wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Bunge lako katika hili lisiyumbe. Tunaweza kwenda kwa ustaarabu mzuri kwamba labda tuombe Serikali iyatekeleze maazimio haya tuletewe utekelezaji *by November. Short of that,* tunakwenda kwenye uchaguzi. Huu ndiyo utaratibu katika nchi nyingine kwamba tunapeana *time*. Juzi G. Brown anapewa muda kwa sababu tu ya posho ya Wabunge, anaambiwa ajiuzulu na yule Bwana akatoa ahadi alizozitoa na wote tunajua kwamba yuko njiani anajiondoa.

Sasa katika taratibu za namna hiyo Serikali yetu tutajenga heshima katika Taifa *unless* leo tupate majibu ya Serikali ni kwa nini Serikali imeshindwa kuchukua hatua kwa wale watu? Hosea unampa onyo, TAKUKURU inatuhumiwa nchi nzima, huyu Bwana ameonekana sio makini. Kama mtu sio makini na umekiri sio makini anaongoza chombo nchi nzima cha kupiga vita rushwa, itapigwaje vita rushwa kiongozi wake sio makini na Serikali imemwacha hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *this is a serious matter*. Tuna malalamiko nchi nzima, fedha za nchi zinalalamikiwa, kuna rushwa lakini kiongozi sio makini. Tunashindwa kuona ni namna gani chombo hiki kitaondoa rushwa. Serikali itupe majibu na ikishindwa kutupa majibu tuipe muda mpaka Novemba. Kama Novemba, hakutakuwa na majibu, watu hawa hawakuchukuliwa hatua, Serikali ikubali iseme *bye bye* twende kwa wananchi tena tukafanye uchaguzi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naam! Hadithi inazidi kuwa tamu tu! *(Kicheko)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nami kwanza niseme naunga mkono taarifa ya Kamati yangu. Tanzania

ni nchi inayoeleweka kuwa na utamaduni wake wa kuzingatia heshima na utawala bora. Tanzania siyo nchi ya wababaishaji.  Ni nchi inayoheshimika duniani kote. Ni nchi iliyosaidia hata kuleta ukombozi katika bara hili la Afrika. Tunaomba tusiyumbishwe.

Mheshimiwa Spika, niliisoma taarifa ile ambayo ililetwa na Serikali ambayo kiukweli kwanza siku ya kwanza mimi nilifikiria siyo taarifa ya Serikali kwa sababu ya kukosa mtiririko. Mwanzo ilikuwa inawasilishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini ilipotoka katika lugha nyingine nikafikiria labda kulikuwa kuna tatizo. Lakini baadaye tukasema tunaweza kuendelea kuijadili.

Mheshimiwa Spika, naomba nifahamu, Tanzania leo hii kupitia Serikali yetu tunataka kujenga utamaduni wa aina gani kwa Watanzania? Tunataka kuwafahamisha nini Watanzania? Tunataka kuwaambia kwamba Serikali yenyewe ina uhuru wa kufanya chochote inachotaka hata kama  hakina maslahi kwa Watanzania na kikapewa kipaumbele? Ni kweli ndio tunavyotaka kuwaambia Watanzania?

Tunataka kuwaambia Watanzania kwamba mtu akishachaguliwa kuwa Waziri hata akikosea, akifanya jambo zito hakuna chombo kinachoweza kumchukulia hatua? Ndiyo tunayotaka kuwaambia Watanzania! Tunataka kuwaambia Watanzania kwamba mtu aliyekaa kwenye madaraka akifanikiwa kufanya kazi zake anavyotaka yeye, akaharibu kama ambavyo anakusudia, basi huo ndiyo uwe ni utamaduni wa kuigwa na mtu yeyote yule anapokuwa kwenye nafasi yake ya kazi kwamba anaweza akajifanyia anavyotaka na asichukuliwe hatua? Ndiyo hilo tunataka kuwaambia leo Watanzania?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naongea nikiwa naguswa sana, naguswa na hali ya Taifa la kesho la Watanzania. Ndiyo maana hata wakati umeanza kuita majina wengine wakasema ni hao hao na mimi nasema ndiyo watabaki hao hao. Watabaki hao hao kwa sababu wamedhamiria kuisaidia nchi yao. Kwa sisi tunaoamini katika imani zetu, hata Yesu hakuwa na mitume wengi, alikuwa nao wachache sana, 12 tu. Kwa hiyo, lazima tuwe *clear*.  Tunataka ku-*archive* nini? Mimi sioni tatizo la mtu muadilifu kutambua makosa yaliyojitokeza, kukiri makosa na kuangalia njia ya kujirekebisha, sioni tatizo. Lakini inapotokea mtu hata kutambua lile kosa, ni ngumu, yaani haoni kabisa kwamba kuna tatizo, hapo ndiyo inaponigusa.  Tunaishi vipi? Tunaendesha vyombo vyetu na watu wa haina gani wasioweza kutambua hili ni kosa? Lakini kikubwa zaidi, ni pale niliposemwa hakuna kithibitisho kwamba wataalamu hawakutumia utaalamu wao au uzoefu wao.

Mheshimiwa Spika, jamani, kwenye ile Kamati kulikuwa kumekusanywa watu wa aina mbalimbali kwa nyadhifa mbalimbali, kwa taaluma mbalimbali, kwa hiyo, ukiacha uwajibikaji wa pamoja kama Mwenyekiti, kama alivyotajwa hapa Bwana Madata bado mtu alikwenda kwa taaluma yake alistahili kushauri kama yeye na kama alionekana kwamba ushauri wake haukukubalika, basi tulitakiwa tupewe vithibitisho kwamba mimi sikukubaliana isipokuwa kwa sababu kikao kiliamua, kama ambavyo tuliona taarifa za *TANESCO*, hakuna hizo taarifa.

Tulitarajia ripoti ya Serikali ituambie bayana kwamba hao tunasema hawana hatia kwa sababu a, b, c tunaambiwa tu hakuna. Tunakwenda vipi? Ndiyo maana unakuta sasa watu wanapata mwanya, uchaguzi unakaribia anajua nikipitapita humu labda fulani atanisaidia chochote kitu, anajitosa mpaka gazetini, njoga niongee, *statement* hii itanisaidia kupata chochote kwa ajili ya uchaguzi yawezekana. Si ndiyo jamani!

Kwa hiyo, hatutakubali hata kama kiongozi wa nchi wakati huo ndiyo anaonekana alihusika, basi tulipoitisha zile Kamati tungeambiwa, kwa sababu tulishafunga ushaidi, hakufanya hivyo mtu, hakulalamika, hivyo sana sana sasa hivi kupitia magazeti ndiyo mtu anatafuta kujiosha, sijui kujiogesha.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi naomba sana, mtu hawezi kujiogesha kienyeji kienyeji, tunaomba kabisa suala la kujiogesha kienyejienyeji halipo! Tutasimama mpaka dakika ya mwisho na Watanzania wanatuelewa. Kwa hiyo, mimi sitaki kwenda kiundani sana kwa sababu wenzangu wamezungumza, lakini niseme tu kwamba ndugu zangu nadhani mnakumbuka, hata wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anahitimisha taarifa, akizungumzia habari ya mgodi wa Kiwira, nadhani iko kwenye taarifa zilizowasilishwa sijui kama itajadiliwa, lakini mimi nasema ule ni mfano wa kuigwa, mtu unapoona kwamba wale wamiliki kweli hawana uwezo tena wa kuendesha na wafanyakazi wana matatizo angalau basi kubali kurudisha ili watu wachukue hatua nyingine.

Mimi nadhani ni utaratibu mzuri, ingekuwa tunafanya hivyo, leo tusingekuwa na malalamiko kama haya yanayoendelea. Hebu tazama siku ya bajeti ya Nishati na Madini watu wangapi walisimama humu kushika vifungu? Ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko makubwa ambayo hayashughulikiwi kwa wakati. Jana tu tumekataa kifungu hapa Mezani, wote sisi mashahidi, tumekataa kifungu kilichopita kinyemelanyemela. Hii nchi tunaipeleka wapi? Nami nasema, kama huu utaratibu wa kutuleta vitu vya ajabu ajabu, tusiwe tunatoa vile vifungu peke yake, viwe vinasindikizwa na yule aliyevileta. Hivyo tutajiwekea azimio kwamba mtu akituletea kitu ambacho hakieleweki kwa sababu zisizojiridhisha, kwa kweli kile kifungu tunapokiondoa hapa Mezani kisitoke peke yake, kiwe kinasindikizwa na aliyekileta. Huo ndiyo ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja taarifa ya Mwenyekiti wa Nishati na Madini.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua fursa hii kukupongeza kwa kunipa nafasi hii ili nichangie hoja iliyopo mbele yetu na mimi ni mmoja wa waumini kwamba Bunge letu hili na jinsi ninavyolifahamu na ninavyolijua na kwa miaka kama sita ambayo nimekaa kwenye Bunge hili, haliwezi hata siku moja kumwonea mtu. Si kazi ya Bunge kumwonea mtu! Bunge linaangalia sera, linatunga Sheria, linasimamia Serikali, kuishauri Serikali na maamuzi mbalimbali yanatokea kwenye Bunge hili na kama ilivyo kwenye taasisi zote, maamuzi huwa yanatokana na taarifa ambayo mtu anayo ndiyo inakuongoza kufanya maamuzi mpaka hapo, unakuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile naamini kwamba unapopata taarifa ya ziada ambayo ikikuonyesha kwamba maamuzi yako ya awali hayakuwa sahihi, muungwana usiwe na kigugumizi kusema hapa nilikuwa nimekosea, hili ndilo sahihi. Hapa Bungeni tunapotoa maazimio kwa kawaida nafikiri huwa hatuiagizi Serikali; kuna kipengele kinasema Bunge hushauri Serikali na maana yake kubwa ni kwamba baada ya Serikali kupata hizo taarifa, ina vyombo vya kwenda kuchunguza ili kupata uhakika na baadaye ni kazi ya Serikali kurudi hapa kututolea taarifa.

Kwa hiyo, ningeishauri Serikali kwamba wakati inafanya uchunguzi na kupata taarifa, isiwe na wasiwasi, isiwe na uwoga hata kama kile ilichokipata kinaendana tofauti na yaliyozungumzwa hapa ije utuambie hapa Bungeni hata kama ni tofauti na Waheshimiwa Wabunge walichosema. Kama azimio haliwezi kutekelezeka kwa sababu 1,2,3 ama kunahitajika taarifa za ziada, irudi hapa ituambie kuliko kukaa kimya.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini kwamba *justice delayed is justice denied.* Suala hili limekaa miaka mitatu, bahati mbaya sitazungumzia juu yangu, maana yake ingebidi niseme niko *interested party,* lakini kila siku unaandikwa, unaandikwa, haina furaha! Kitu gani? Kama Karamagi amekula hela, usimwambie! Usimchukue Mahakamani akafungwa! Mchukue akafungwe kama amekula hizo pesa, amezimeza mpaka haziwezi kupatikana! Si umuendee kwenye *account* zake mumshike, mumfunge! Lakini kama linakwenda tu, ina maana unataka ungoje mpaka mfikie uchaguzi bado, unasema hili, na hili; maana yake humtendei haki. Kwa hiyo, nafikiri sio sahihi juu ya hilo.

Sasa niende kwenye *point.* Nimepata hapa kwenye *note*, sijui nani kanitumia *message*, kaniandikia, naweza kunukuu: “*Mheshimiwa Spika, binafsi nakuheshimu sana, nakupenda sana. Kwa hili la leo nakuomba usiongee, acha! Muungwana akivuliwa nguo huchuchumaa. Acha kaka watakushangaa.*” *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hakuandika jina lake, lakini najua ananipenda. Lakini nami naweza kumpa ushauri, naamini kwamba hapa sote tumechafuliwa kwenye magezeti hata wewe Mheshimiwa Spika umechafuliwa, mimi naamini mtu anaweza akakutupia madongo, uchafu,yakakuchafua nguo, lakini kama roho yako ni safi, itabaki safi tu.

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kwenye hoja yenyewe. Kuna hoja ambayo imetolewa kwamba watendaji wa Serikali, watumishi mbalimbali wamesafishwa na inaweza kuwa kweli ama sio kweli. Lakini hili Bunge ninaamini ndio tunatunga Sheria lakini kama hatuvisomi vipengele vya sheria hizo, tutajilaumu sisi wenyewe.

Mimi nilikuwa nasoma kuwa, analaumiwa yule mtumishi wa TAKUKURU, Hosea; lakini ninaposoma, hii *prevention and combating of corruption act*, kifungu Na.50 naomba kukinukuu, kinasema:“*general immunity for members* kile kifungu cha 50 mnawapa kinga. Kinasema: “ *no act or thing done or omitted to be done by an officer of the bureau shall if the act or omission was done or omitted on a field in exercise of his function under this act render the officer or personally liable for the act or omission* “.

Umekwishamlinda, ukimfukuza akimpeleka Mahakamni anakuondoa kwa hiki kifungu. Hii ndio Sheria isemavyo kama tulikiweka tukiwa tumefunga macho, shauri zetu. Lakini hatuwezi kuilaumu Serikali kama iliona badala ya kumfukuza impe tu onyo kwamba angeona hili na hili, lakini isifanye kama tulivyoshauri kikubwa wangetuambia tumeshindwa kufanya hivi kwa sababu ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naamini kwamba watumishi wana mamlaka za nidhamu ambazo wanafuata. Leo asubuhi nilikuwa nasikiliza kwenye televisheni *DT DOBIE* wafanyakazi waliwafukuza sina uhakika 2002, au 2000 sasa wamerudishwa na Mahakama na wanalipwa stahili zao zote. Hizi ni Sheria tumezitunga sisi wenyewe, kwa hiyo, inabidi kuziangalia kabla hatujafanya maamuzi na ningeomba tu Serikali labda iwe wazi. Isiliweke jambo hili kijumla jumla iseme kwamba hili limekuwa hivi tumeshindwa kwa sababu 1,2,3; kwa njia hiyo itabidi kuliondoa. Na sisi Wabunge tusiwe na jazba, tulitoa ushauri kwa Serikali mahali ambapo panakuwa pagumu, tusilazimishe hata sisi tukavunja Sheria ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nisaidie tu kisheria, kipengele alichokisoma Mheshimiwa Karamagi kina neno la kilatini *Bonafide*, lazima idhihirike kuna nia njema. Sasa kama Kamati imeona hakuna nia njema, hiyo kinga haipo. Ni wajibu wangu kufafanua mambo, maana yake isije ikachukuliwa hoja hapa eti Sheria inasema watumishi wote wa umma wana kinga hata kwa mambo yanayodhihirika ameyafanya kwa nia mbaya. Hiyo haipo!

**MHE. HERBERT J. MTANGI:** Mheshimiwa Spika, nitazungumza kwa ufupi sana. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nitazungumza katika maeneo maalum sana ya kiufundi na nitaanza na hili ambalo limeonekana linaleta utata. *Letter of credit* au ile inayoitwa barua ya dhamana, hii barua ya dhamana Sheria yake ni kwamba, ikishafunguliwa lazima ilipwe kwa kiasi kile kile kilichopo pale. Taarifa zimeonyesha kwamba, kiasi cha dola 4,865,000,000 zimelipwa zaidi ya ile thamani ya barua ya dhamana.

Tunachojibu ambacho tumeambiwa ni kwamba, imekuja ankara ya madai ya kiasi hicho, ikapita *TANESCO* ikaenda katika maeneo mengine yote ikalipwa. Kiutaratibu inaonekana kama utaratibu umefuatwa, lakini kimsingi gharama hizo zilikuwa ni za nini? Kimsingi gharama hizo zilikuwa ni sehemu ya gharama ambazo Wazungu wanaita *mobilisation* maandalizi ya uwekaji wa vifaa ili uanze kufanya kazi na haya maandalizi yalijadiliwa katika mpango ule katika Kamati maalum, kwamba yatakuwepo maandalizi na kwa hiyo, ifunguliwe barua ya dhamana ili kazi hizi ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa imekuja ankara dola 4,865,000,000, wewe unaipitisha unalipa eti kwa sababu *TANESCO* wameipitisha. Kwa sababu Wizara ya Nishati na Madini imeipitisha, kwa hiyo, Benki Kuu unalipa. Lazima ujiulize, unalipa kwa madhumuni gani? Hii gharama ni ya kuuchukua mzigo ule wa mashine kwa ndege kutoka huko ulikotoka kuifikisha Dar es Salaam. Sasa hebu tutazame hiyo gharama ya ndege.

Mheshimiwa Spika, kukodisha ndege kubeba mzigo huo kwa Dola za Marekani 4000, Dola za Marekani 4,865,000 kweli ndiyo gharama halisi! Mimi nilikuwa nafanya mahesabu hapa ya dharura kwamba ndege inatoka Amsterdam, *Boeing* inachukua abiria 200, tiketi ya kwenda na kurudi kwa ndege hiyo Dola 4000 kwa kila *passenger*, kwenda na kurudi ndege hiyo itarudi itakuja Dar es Salaam na itarudi tena Amsterdam kwa kiasi hicho ni Dola 800,000 peke yake. Hizi  Dola 4,865,000 kwa kusafirisha mzigo kutoka huko ulikotoka mpaka Dar es Salaam ni gharama halali? Hapo ndiyo mahali pa kujiuliza na sisi tulisema liangaliwe hilo. Sasa watu wanasema utaratibu wa kupitisha imepitishwa, ni sawasawa, lakini: Je, ile barua ya dhamana!

Mheshimiwa Spika, kwa nini tumevuka kiwango bila kufuata taratibu? Hilo bado kama ambavyo Kamati imesema hairidhiki na mimi nasema bado siridhiki na naomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kutoridhika kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini nije katika lingine ambalo nimelisikia likisemwasemwa sana, watu wanazungumza tu hapa kwamba hivi RICHMOND amekosa nini wakati RICHMOND hakulipwa hata senti tano? Hizo lugha za ubabaishaji tu, RICHMOND ameingia mkataba na *TANESCO*, RICHMOND akatoa ridhaa ya kuhuisha mkataba wake kwa DOWANS. Sasa amejitoaje? Mkataba ameomba kwamba yeye hawezi anamwambia ndugu yangu, hebu fanya kazi hii, hebu turudi nyuma, hivi DOWANS alipatikana kwa utaratibu ule tunaoufahamu wa *procurement*? Hapana. RICHMOND alihuisha mkataba kwa hiyo majukumu na dhamana bado iko pale pale. Leo mnasema ooh, RICHMOND kakosa nini? RICHMOND hajalipwa fedha yoyote, hizo ndiyo lugha tunazosema za kutaka kuwasafisha RICHMOND hapa!

Mheshimiwa Spika, si kweli RICHMOND bado ana hatia na mkataba umedhibitishwa si tu na Kamati, umedhibitishwa hata na hao mliyowaleta, wameuthibitisha kwamba mkataba ule haukuwa halali. Kwa hiyo, yupo pale pale kwa sababu yeye alimkabidhi majukumu yake *DOWANS* na *DOWANS* amechukua fedha tena kachukua zaidi ya fedha zile zilizoidhinishwa katika barua yake ya dhamana. Yeye ndiyo kachukua hizi fedha Dola za Kimarekani 4,865,000 *DOWANS*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nilisema nitakwenda haraka, basi nitakwenda katika mambo mengine. Niende katika *DOWANS* sasa. Mkataba umesitishwa, mkataba uliokuwa si halali umesitishwa, *TANESCO* wameipeleka *DOWANS* Mahakamani, mashine asiziondoe na nina taarifa kwamba Mahakamani *TANESCO* wameshindwa. Lakini mashine ile iko kwenye eneo la Ubungo pale Dar es Salaam mali ya *TANESCO.* Hivi kweli mashine itakaa pale inakaribia sasa muda wa miaka miwili, bure tu! Lazima *TANESCO* watuhakikishie kwamba *DOWANS* analipia *rent* ya kuweka mashine ile pale katika maeneo ya Ubungo na si kuondoa tu mashine hivi hivi bila kulipa *rent*. Hatuwezi kumlindia *DOWANS* mashine zake, hatuwezi kumuwekea *DOWANS* mashine zile bure! Hilo ni muhimu, lakini vile vile lazima taarifa iletwe hapa Bungeni, taratibu za ile barua ya dhamana zilikuwa zinasema tunampa fedha huyu lakini atazilipa wakati tukimlipa madai yake.

Mheshimiwa Spika, lakini watuletee taarifa za kudhibitisha kwamba zimelipwa na sio zile milioni 30 tu, zilipwe pamoja na hizo milioni 4.8 kwa sababu zilikuwa ni sehemu ya gharama ya *mobilisation*, zote lazima zirejeshwe. Sasa lazima watuambie turidhike kwamba kweli zimerejeshwa hizo fedha. Kweli *DOWANS* amerejesha fedha zote au amerejesha tu zile milioni 30 na hizi 4,865,000 amezichukua kienyeji tu. Hatujui hilo! Watanzania hatujui hata mahesabu! Watanzania hatujui hata tafsiri ya mikataba! Kama wapo wasiojua, wengine tunafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la nidhamu, mimi ni Mkuu wa Taasisi na wako walioko chini yangu, wao ndiyo niliyowatuma kwenda kutafuta ripoti, wakaileta kwangu. Ripoti hii imeonekana ina kasoro, mimi Mkuu wa Taasisi ninaendelea kubaki katika nafasi yangu wakati uchunguzi unafanywa. Hivi hawa waliokwenda kuandika taarifa wakahisi kama tulivyohisi sisi kwamba yapo mambo yaliobadilishwa katika taarifa na wao bado wanaendelea kuwa chini yangu na mimi naendelea kufanya kazi, hivi kweli tuna imani kabisa hawa wataendelea kusema kweli wakati mimi bado nipo kwenye kiti? Hapana utaratibu na upo katika Kanuni hizo za watumishi. Unamsimamisha kazi wakati uchunguzi unaendelea, akionekana hana hatia anarudi katika nafasi yake. Hicho kifungu kilichozungumzwa hapo nashukuru umekifafanua vizuri, lakini katika Kanuni kusimamishwa kupo katika Kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa wewe unamweka pale unawanyima hawa haki na uhuru wa kusema ukweli na ndivyo ilivyotokea, unawatisha hawa. Nami nasema, laiti angekaa pembeni wale walioko chini ambao walikuwa na uhakika wa ile taarifa kwamba ilibadilishwa wangetoa nakala halisi. Lakini mnawatisha! Kwa nini Serikali inafanya vitu vya namna hiyo? Kwa hiyo, lazima hilo limeleta kasoro. Huwezi ukamwachia fisi mzoga aulinde halafu unarudi hakuna kitu, unamwamini fisi maneno anayokwambia kwamba simba alirudi akauchukua, amekula nyama pamoja na mifupa yote! Wewe umemwachia dhamana yule mtu ambaye...! Kwa hiyo hivi ndivyo walivyofanya hawa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ili na wenzangu nao wapate nafasi ya kusema, naomba niishie hapa. Nasema naiunga mkono taarifa ya Kamati lakini pamoja na hayo niliyoyaongezea yawe sehemu ya taarifa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kadiri tunavyoendelea, linanijia wazo kwamba ipo kazi ya kufanywa na Serikali katika hoja hizi, labda wakisimama wakisema hakuna, wamebaki hivyo hivyo, lakini mimi nadhani tukiendelea na zoezi hili, kasoro zinazidi kuonekana za dhahiri tu za mtu unaziona sasa. Labda ningetoa nafasi, mimi nitafurahi sana kama Serikali wakisema na niko tayari kuwapa muda huo kwamba kwenye Mkutano wa Kumi na Saba sasa ndiyo tulifunge hili kuliko kuendelea kuzidi kuzionyesha tofauti, matatizo na hivi na muda wenyewe ni mgumu. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini aweze kutusaidia katika hilo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa fursa hii kwa niaba ya Serikali kusema kauli ya Serikali kuhusu mwongozo wako. Awali ya yote nakushukuru wewe, nawashukuru pia Kamati ya Nishati na Madini, Kamati ya Bunge ya Kudumu, lakini pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa

ushauri ambao wameutoa. Sisi kama Serikali tumeliongea hili kwenye hatua ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini chini ya Mheshimiwa William Shellukindo baada ya kukaa na kupitia. Kimsingi tumekubalina kwamba kuna kazi ya kufanya zaidi na kuna mambo ya kutolea ufafanuzi zaidi. Kama utaniruhusu kwamba niishie hapa bila ya kusema kidogo ambacho nilikuwa nataka niseme kwa kutoa ufafanuzi kwenye hoja uliyoitoa kwa Serikali ni kwamba bado tuna kazi, tuko tayari, lakini sema tu kwamba kuna mambo ambayo nataka niyaweke wazi mawili matatu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, limejitokeza suala hapa, kulikuwa na utata kwa nini...

**SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa Waziri ukishasema hivyo, tuliamue tu hili kwa sababu hata hayo unayotaka kujibu pengine yatakuwa bora zaidi mnamo mwezi Novemba. Waheshimiwa Wabunge nawasihi sana, sisi wote tunaiona hali hii na hatungeendelea kusema na kurejea katika mambo mbalimbali, nashauri yale yote ambayo Kamati ya Nishati na Madini inastahili kuyazingatia wanaweza wakapelekewa hata kwa maandishi halafu Kamati ya Nishati na Madini ikawasilisha sasa kazi iliyosalia kwa uhakika kabisa, nini kinatarajiwa na Bunge, hiyo ikapelekwa rasmi kwa Serikali, halafu uamuzi wetu sasa mwezi Novemba katika Mkutano wa Kumi na Saba ndiyo tutaweza kulizingatia hilo kwa vizuri.

Mimi nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi iliyopo mbele yetu hili litakuwa ni jambo zuri zaidi kuliko kuendelea kuzungumza, kurejea mambo ambayo mnaunga mkono hii Kamati yetu na kadhalika. Nadhani tunakubaliana kwa hilo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, napenda sasa nitoe Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira *(Kiwira Coal Mines Ltd).*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ilifanya ziara Mkoani Mbeya kuanzia tarehe 15 hadi 18 Januari, 2009. Wakati wa ziara hiyo, Kamati ilipata fursa ya kukutana na uongozi wa Wilaya za Rungwe, Kyela na Ileje. Mgodi huo uko mpakani mwa Wilaya hizo tatu za Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya ziara hii yalikuwa ni kutembelea Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira ili kujionea hali halisi ya mgodi na uzalishaji umeme. Katika ziara hiyo, Kamati iliweza kujifunza mambo mengi kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya historia ya Mgodi wa Makaa ya Mawe – Kiwira ni kwamba mgodi huu ulianzishwa kwa msaada wa fedha na ufundi kutoka Jamhuri ya Watu wa China. Mradi huu ulizinduliwa rasmi na aliyekuwa Rais wa Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Ali Hassan Mwinyi na kuanza uzalishaji mnamo mwezi Novemba, 1988.

Mheshimiwa Spika, mgodi huu upo katika Wilaya tatu ambazo ni Rungwe, Ileje na Kyela. Hivyo hata usimamizi wake unahusisha Wilaya hizi kama ifuatavyo:- Kwanza, Wilaya ya Kyela husimamia masuala ya Kiutawala; pili, Wilaya ya Ileje husimamia masuala ya mapato kama vile ulipaji wa tozo ya Halmashauri zitokanazo na uzalishaji wa makaa na kodi za wafanyakazi. Hii ni kutokana na kwamba eneo la uchimbaji wa makaa ambapo uzalishaji hufanyika liko Ileje. Lakini eneo la Utawala na makazi ya wafanyakazi lipo Kyela; tatu, Wilaya ya Rungwe ndiyo iliyokuwa Wilaya Mama ya Wilaya ya Ileje na Kyela.

Mheshimiwa Spika, mgodi una uwezo wa kiusanifu wa kuzalisha makaa ghafi tani 50,000 kwa mwaka. Hata hivyo, uzalishaji unaweza kupanuliwa kufikia zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka. Kabla ya kubinafsishwa mgodi huo ulikuwa unalizalisha makaa ya mawe ambayo yalikuwa yanatumika kuzalisha umeme wa megawati sita ambazo ziliunganishwa kwenye njia kuu ya msongo wa umeme - *National Grid* kupitia Mji wa Tukuyu.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa ubinafsishaji wa *Kiwira Coal Mine Limited CSM Limited* ulianza mwaka 2004 chini ya Tume ya Rais ya Ubinafsishaji ya Mashirika ya Umma *PRSC.* Mgodi huu ulibinafusishwa rasmi kwa kampuni ya *Tan Power Resources Limited* mwaka 2005 na sasa unajulikana kama *Kiwira Coal and Power Limited*. Baada ya Shirika hili kubinafsishwa Uongozi wa *KSM Limited* uliamuliwa na *PSRC* kuandaa mafao ya mwisho kwa wafanyakazi, yaani *teminal benefits.*

Wilaya ya Rungwe ilipewa jukumu la kusimamia jukumu la kusimamia zoezi la ulipaji wa mafao ya wafanyakazi na jumla ya wafanyakazi 1,632 walilipwa kiasi cha Sh. 686,999,000.40 fedha ambazo zilitoka *PSRC.* Pamoja na wafanyakazi kulipwa mafao hayo, bado wafanyakazi hao wanadai kuwa malipo hayo hayakuzingatia madai halisi kwani wengi wao walipunjwa. Aidha, shilingi milioni 50 kati ya fedha hizo zilipotea na tayari Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inapambana na tatizo hilo kama tulivyoelezwa na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe. Aidha, wakati tulipokuwa ziarani, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Maafisa wa TAKUKURU na *CHC* walikuwa huko wakifuatilia suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Kamati ilipokea malalamiko kutoka kwa wafanyakazi kuwa hawajalipwa mishahara kwa kipindi cha miezi saba hadi wakati Kamati ilipokuwa mgodini mwezi Januari mwaka huu. Hali hii imejenga chuki kati ya wafanyakazi na wawekezaji na kusababisha watumishi hao kushindwa kuendesha maisha yao pamoja na familia zao kwa ujumla. Hali ya watumishi hao ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu thamani ya mgodi wenyewe na ubinafsishaji wake ulivyofanyika ni kwamba tathmini ya mwaka 1988 ilionyesha kwamba kwa wakati huo mgodi ulikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 4.2 lakini tathmini ya mwaka 1991 iliyofanywa na Taasisi ya Ardhi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilionyesha kuwa mgodi huo ulikuwa na thamani ya Shilingi bilioni saba. Pamoja na uthamini huo kufanyika miaka mitano kabla ya kubinafsishwa mgodi huo Kamati ya Nishati na Madini

imeshindwa kuelewa ni vigezo gani vilitumika kutupilia mbali uthamani huo wa awali na kuamua kuuza hisa za mgodi wote kwa asilimia 70 kwa gharama ya Shilingi milioni 700 tu.

Umuhimu wa mgodi, baada ya kutembelea mgodi huo, Kamati ilibaini umuhimu wake hasa katika malighafi ya makaa ya mawe ambayo hutumika sehemu mbalimbali kama nishati mbadala kwa kuendesha mitambo kwenye hospitali, viwanda, Magereza na kadhalika. Makaa haya pia kama ilivyoelezwa awali hutumika kuzalisha umeme. Kwa mfano, kabla ya kubinafsishwa, mgodi ulikuwa ukizalisha Megawati sita zilizokuwa zimeingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya *Tan Power Resources Limited* kupewa mgodi walitakiwa wazalishe Megawati 200 katika awamu mbili. Awamu ya kwanza, ilikuwa izalishe Megawati 50 ifikapo mwezi Julai, 2007 na Megawati nyingine 150 zingekamilika ifikapo mwezi Machi, 2009. Kamati imeshangazwa kuona kuwa hakuna chochote kilichofanyika katika kutekeleza mpango huo hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, hapo awali umeme huo ulikuwa ukisambazwa na kutumika katika wilaya ya Kyela na Rungwe. Kwa kuwa uzalishaji umeshuka kutoka Megawati sita mpaka sifuri kwa sasa maeneo hayo yana matatizo ya kupata umeme kwani chanzo hicho hakizalishi tena umeme. Kamati ilipofika mgodini hapo tarehe 17 Januari, 2009 ilishangazwa na aina hii ya uwekezaji. Kamati iliona kitendo hiki kama hujuma ya aina fulani. Kiwira iliyokuwa ikizalisha Megawati sita leo kuzalisha Megawati sifuri.

Umiliki wa hisa, hisa za *Kiwira Coal Mine Limited* zinamilikiwa na Serikali pamoja na Kampuni ya *Tan Power Resources Limited* kampuni ya *Tan Power Resources Limited* ni Muungano wa Kampuni nne zenye wanahisa kama ifuatavyo:-

Kampuni ya kwanza ni *Force Mick Limited* na ina wanahisa watatu, ambao ni Nick Mkapa, Fostam Mkapa na Bi. Mahembe. Kampuni ya pili ni *Choice Industries* na ina wanahisa wawili, Joe Mbuna, Godfrey Francis na Goodyear Francis. Kampuni ya tatu ni *Devo Consult Limited* ina wanahisa wawili. D. Yona and Dani Yona Junior na kampuni ya nne ni *Universial Technologies Limited,* ina wanahisa wawili, Wilfred Malkia na Evance Mapundi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ilipokea taarifa mbili tofauti zinazogongana kuhusu umiliki wa hisa za mgodi huu. Taarifa ya uwekezaji inaeleza kuwa wawekezaji wamenunua hisa asilimia 70, Serikali imenunua asilimia 12 na nyingine asilimia 12 hazijanunuliwa, wakati wa taarifa ya wafanyakazi inasema, wawekezaji wana asilimia 85 na Serikali asilimia 15. Kamati inashindwa kuelewa juu ya utata wa umiliki huu wa hisa na hivyo kuiomba Serikali ieleze wazi wazi kuwa inamiliki hisa asilimia ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifahamishwa kuwa kabla ya kubinafsishwa, mgodi huo mitambo yote ya uzalishaji ilikuwa imechakaa hivyo ilihitaji matengenezo makubwa ili iweze kuzalisha ipasavyo. Hata hivyo taarifa ya uwekezaji inaonyesha

kuwa Serikali ilitenga Shilingi billioni 17 kwa ajili ya ukarabati wa mitambo hiyo. Je, ikiwa Serikali ilitenga kiasi hicho mwekezaji mwenye hisa naye alitenga kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishangazwa kuambiwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa wamiliki wapya kuwa kiasi hicho cha fedha kilitumika kukarabati mitambo wakati wafanyakazi walisema kuwa hakuna ukarabati wowote uliofanyika. Kwa sasa jenereta mbili za kuzalisha umeme zimechakaa kabisa na hazifanyi kazi wakati jenereta ya tatu ina uwezo wa kuzalisha si zaidi ya Megawati moja tu kwa ajili ya kutunza mitambo, yaani *service*.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa kawaida, Bodi ya Wakurugenzi ya *Kiwira Coal Power Limited* hutakiwa kukutana si chini ya mara nne kwa mwaka kujadili masuala yanayohusu kampuni au shirika husika. Kamati ilishuhudia hali tofauti kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Kiwira ambayo toka imeingia madarakani haijawahi kukutana na wafanyakazi kuzungumzia masuala yanayohusu wafanyakazi wa mgodi kwa ujumla na mgodi kwa ujumla na vile vile Kamati imeona upungufu kwamba Bodi hiyo yenye Wajumbe ambao baadhi yao wanatoka Serikali na huingia kwenye Bodi hiyo kwa nafasi zao kushindwa kushiriki katika vikao na hivyo kutokuwa na Taarifa zozote kuhusiana na mgodi. Wawakilishi au Wajumbe hao wa Serikali hawakuwa na utaratibu wa kutoa za mabadiliko ya nyadhifa zao. Hivyo kubaki kwenye orodha ya Wajumbe wa Bodi huku walioshika nafasi zao kwa sasa kutoshiriki kwenye shughuli za kampuni. Hali hii imesababisha kukosekana kwa taarifa zinazohusiana na mgodi huu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili, Kamati inashauri kuwa ni vyema Wajumbe wanaoteuliwa kuwa Wajumbe katika Bodi kwa nyadhifa zao wanapokoma kuwa Wajumbe basi waache taarifa kwa maandishi ili yeyote atakayeteuliwa badala yao apate taarifa za hali ya Kampuni au shirika husika kuliko ilivyofanyika Kiwira. Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya *Kiwira ya Coal and Power* ni kama ifuatavyo:-

Moja, ni Joe Mbuna ambaye kwa sasa ni Marehemu kutoka *Tan Power Resources*, aliyekuwa Mwenyekiti; wa pili, Wilfred Malkia - *Tan Power Resouces;* wa tatu, Evance Mapundi, samahani yale maandishi ya kule chini yasomeke kwamba bado anaendelea kuwa Mjumbe wa Kamati hiyo; wa nne, Lutenge kutoka *Tan Power Resources* – mjumbe; wa tano Kamishna wa Madini ambaye anawakilisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa sita *RAS* - Mbeya ambaye pia anawakilisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha uzalishaji wa makaa ya mawe kwa sasa kimeshuka sana ukilinganisha na kipindi kabla ya ubinafsishaji. Hali hii imetokana na kuchakaa kwa miundombinu ambayo haifanyiwi ukarabati wa mara kwa mara. Aidha, wawekazaji wa sasa wameuza baadhi ya vifaa na mitambo kama vyuma chakavu na vyuma hivyo kutumika kwenye shughuli nyingine nje ya uchimbaji ya makaa. Kwa mfano, krasha la mawe la kutengeneza barabara. Maelezo haya yametolewa na wafanyakazi 500 waliokutana na Kamati. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya uchunguzi na ikibainika ni kweli, basi hatua za sheria zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wawekezaji wana mpango wa kuanzisha mgodi mwingine wa uchimbaji wa makaa, Kamati ina mashaka na uwezo wao, itakuwaje washindwe kuendeleza uzalishaji wa Megawati sita halafu warukie kuzalisha Megawati 200 hadi 400?

Mheshimiwa Spika, hali hii ni dhahiri kuwa uwezo wa wawekezaji kifedha ni wa mashaka kutokana na ukweli uliodhihirika na dalili zinazoonekana hususan katika kutekeleza mipango mbalimbali ya kuendeleza mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, ni zaidi ya miaka minne sasa imepita tangu wakabidhiwe mgodi huo, lakini hakuna maendeleo yoyote yaliyofanyika ikiwa ni pamoja na kutokulipa mishahara ya watumishi wake kama ilivyoelezwa katika vifungu vilivyotangulia.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa ule wa saba kuna jedwali ambalo linaonyesha ni kiasi gani cha makaa ya mawe yalipatikana kuanzia mwaka 1989 hadi mwaka 2008, kwa kuwa WaheshimiwaWabunge wanayo nakala hii wataona wao wenyewe. Maoni na ushauri wa Kamati, baada ya kutembelea mgodi na kwenye maeneo ya uzalishaji pamoja na kuingia kwenye mitaro *tunnels* ndani ya mgodi na kukagua miundombinu ndani ya mgodi Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Moja, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote wanalipwa mafao yao, stahili walioyotakiwa kulipwa wakati wa kubinafsisha mgodi huo mapema iwezekanavyo ili kuepuka migogoro inayoweza kuleta madhara makubwa mgodini hapo.

Pili, kwa kuwa wawekezaji wameonyesha wazi wazi kuwa wameshindwa kutekeleza mpango wa uendelezaji wa mgodi wa Kiwira kutokana na kutokuwa na uwezo wa kifedha Kamati inashauri kuwa mgodi huo urudishwe Serikalini na uendeshwe na *STAMICO* ikishirikiana na *TANESCO* na uendelee kuzalisha umeme ili kuliepusha Taifa siyo tu kulipia *capacity charge* ambayo wawekezaji walikuwa wamelenga kulipwa, bali pia kuweza kuingiza kiasi kikubwa cha umeme kwenye gridi ya Taifa. Vile vile wawekezaji hao warejeshe Serikalini gharama zote pamoja na Shilingi bilioni 17 zilizotolewa kwa ajili ya kukarabati. Aidha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *CAG* awezeshwe ili aweze kufanya ukaguzi wa kina kuhusu mapato na matumizi wa mgodi huo ambao una hisa za Serikali.

Tatu, Kamati inashauri kuwa Serikali ishughulikie mgogoro wa wafanyakazi kama ilivyofanywa kwa Shirika la Reli *TRC* endapo itakubali ushauri wa kuvunja mkataba na wawekezaji na kuukabidhi mgodi huo kwa *STAMICO* na *TANESCO*. Mgodi wa Kiwira ni chanzo mbadala cha kuzalisha umeme na utasaidia kuondokana na utaratibu wa kulipa *capacity charges* kwa wawekezaji wanaozalisha umeme wa kujitegemea.

Nne, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini wakati wa kuteua wawakilishi wake kwenye Kampuni ambazo zina hisa ili kuepukana na udhaifu mkubwa uliojionyesha kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya Kiwira *Coal and Power Limited.*

Mheshimiwa Spika, mwisho, itakumbukwa kuwa taarifa hii iliwasilishwa kwako mapema mwezi Februari, 2009 ambapo Serikali pia ilipata na kuanza kufanyia kazi baadhi ya maoni yaliyokwishatolewa kabla ya taarifa hii kuwasilishwa Bungeni. Hivyo, mambo yote ambayo Kamati imewasilisha na ambayo Serikali imeanza kuyafanyia kazi utekelezaji wake ufanywe kwa wakati kama tulivyokwisha shauri hapo juu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati imefarijika na Taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ambayo kwa kiasi kikubwa imezingatia zaidi kuurejesha mgodi huu Serikalini chini ya Mkataba wa uendeshaji utakaotolewa kwa Mkandarasi ambaye atapewa jukumu la kujenga uwezo wa Mashirika ya *STAMICO* na *TANESCO* ili kuyawezesha kumiliki na kusimamia mradi huu.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa mgodi wa Kiwira wamekuwa wavumilivu sana kwa kuishi bila mishahara kwa miezi 12 sasa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ichukue hatua za haraka ili wafanyakazi hao walipwe mishahara yao na kuwaonyesha wazi kwamba Serikali yao inawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Kamati yangu imepokea taarifa ya wizi mkubwa uliofanyika kwenye miundombinu ya Kiwira ambapo vifaa vifuatavyo vimeibiwa au kuhamishwa. Vifaa hivyo ni viberenge sita vya kusafirishia mkaa mgodini.

Mheshimiwa Spika, *tone crasher* tatu, *wheel loader* tatu, *deep driller* zenye mita 70 kila moja. Injini za *Fiat* ya *tone* 30 tatu, Mashine za kuzoa makaa nane, *duper* moja, tanki za kutunzia mafuta mbili pamoja na *compressor* nne. Kamati inaishauri Serikali kuweka ulinzi wa kutosha ili kuhakikisha kuwa mali zilizopo haziendelei kuhujimiwa na iwapo zitakuwa zimehamishwa, basi zirudishwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwa kushiriki kwenye ziara ya kutembelea mgodi wa Kiwira na kwa uvumilivu na michango yao wakati walipokuwa kwenye ziara. Wajumbe hao ni kama wafuatavyo:-

Mheshimiwa William H. Shellukindo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe - Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Faida Bakar - Mjumbe, Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa - Mjumbe, Mheshimiwa Asha Jecha – Mjumbe, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa – Mjumbe, Mheshimiwa Mohamed H. Mnyaa - Mjumbe, Mheshimiwa Halima Mamuya – Mjumbe, Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya – Mjumbe, Mheshimiwa Dr. James Musekela – Mjumbe, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka – Mjumbe, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko – Mjumbe, Mheshimiwa Fredi Tungu Mpendazoe –Mjumbe, Mheshimiwa Charles Mwera – Mjumbe, Mheshimiwa Esther Nyawazwa – Mjumbe, Mheshimiwa Mohamedi Sinani – Mjumbe, Mheshimiwa Omari Sheha Mussa – Mjumbe, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa – Mjumbe, Mheshimiwa Rita Mlaki – Mjumbe, Mheshimiwa Klontsi Mporogomyi – Mjumbe na Mheshimiwa Lolensia Bukwimba – Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati inaamini kwamba Serikali yetu ni sikivu, itapima, itachambua na kudadisi taarifa muhimu kuhusiana na uuzaji wa hisa za Kiwira kwa wanahisa wa Kampuni ya *Tan Power Resources* na hivyo kufanya maamuzi sahihi kama Kamati ilivyoshauri hapo juu.

Aidha, napenda kusisitiza kwamba Kamati ya Nishati na Madini ilitembelea mgodi wa makaa ya Kiwira kwenda kuona jinsi unavyochangia katika kuzalisha nishati ya umeme ambayo inahitajika sana katika uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma mbalimbali na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdul Marombwa kwa niaba ya Mwenyekiti. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia hili la Kiwira, nimezinduliwa hapa kwamba ili lile la kwanza ambalo mlilikubali liishe vizuri, ni vyema kikanuni Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Shellukindo aje kwa sababu hii ni hoja ya Kamati, atamke kwamba ni vizuri kwamba lihitimishwe Mkutano wa Kumi na Saba. Tukiafiki hilo, basi tunaendelea na hili la Kiwira. Sasa namwita Mheshimiwa Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena hii ili nihitimishe hoja hii ya Kamati ya Nishati na Madini, kuhusu Mkataba wa *TANESCO* na *Richmond Development Company Limited (LLC).*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna wenzetu ambao walichangia, ningependa niwatambue kwa mujibu wa taratibu zetu. Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Saidi Nkumba, Mheshimiwa Dr. Slaa, Mheshimiwa Eng. Manyanya, Mheshimiwa Karamagi na Mheshimiwa Mntangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wote waliozungumza wamezidi kuimarisha maoni ya Kamati. Kwa hiyo, nawashukuru sana. Kuna machache ambayo yamezungumzwa yataweza kuboresha maoni yetu na nikifika hapa ningependa sasa Bunge lako Tukufu lipokee maoni ya Kamati na maoni haya yabadilike sasa kuwa ni Maazimio ya Bunge ya kwenda kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kazi hii iweze kwisha mwaka huu kama tulivyoazimia, naomba kupendekeza kwa Bunge lako kwamba sasa tuwape muda Serikali kwa kipindi kuanzia sasa mpaka Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge lako Tukufu tupate taarifa ya mwisho na kama kuna hoja nyingine ambazo zinaweza kutolewa hoja za kutengua Maazimio hao, basi wakati huo huo zifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Nakushukuru Mwenyekiti wa Nishati na Madini - Mheshimiwa William Shellukindo kwa hoja hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni ya kuongeza muda ili majibu yanayohusu hoja zile 23 za Bunge hili katika Azimio yashughulikiwe na Seriakali na Taarifa ya mwisho iweze kupatikana katika katika Mkutano wa Kumi na Saba mwezi Novemba mwaka huu. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

*(Hoja iliafikiwa na kupitishwa na Kamati ya Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru. Kwenye suala hili la Kiwira ninao wachangiaji watatu, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Fred Mpendazoe na Mheshimiwa Magalle Shibuda. Kwa sababu Mheshimiwa Shellukindo, nadhani itasaidia kama yeye atatangulia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Willliam Shellukindo atafuatiwa na Mheshimiwa Mpendazoe na tutamalizia na Mheshimiwa Shibuda. Kwa tahadhari kwa Mheshimiwa Shibuda kwamba achukue muda mfupi kadri inavyowezekana. Mheshimiwa William Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii.

**SPIKA:** Kuhusu Utaratibu. Tulia kwanza Mheshimiwa Shellukindo. Mheshimiwa Dr. Salaa, utaratibu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Kuhusu utaratibu Kanuni ya 68.

**SPIKA:** Naam! Endelea.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa taratibu ambazo tulikuwa tumejipangia siku ya leo ilikuwa ni ya kupokea taarifa ya Kamati ambao inachukua na inaifanyia kazi taarifa ya utekelezaji ya Serikali. Sasa kwa bahati mbaya taarifa tuliyosomewa sasa hivi ni Taarifa ya Kamati ambao ni ya mwezi Februari, 2009. Tuligegemea katika taarifa hiyo Kamati itatupa pia picha nini imefanywa na Serikali. Sasa kwa kuwa haipo: Je, tunaijadili taarifa hii ili iwe nini? Kwa sababu lengo ilikuwa ni kuhitimisha mjadala huu wa Kiwira pia na ndivyo ulivyopangwa kwenye *Order Paper* na tungetegemea tungepata hii taarifa sasa naomba kuhusu utaratibu niombe mwongozo wako: Je, tuna sababu ya kuendelea kujadili taarifa hii au tuipeleke kwa sababu bila taarifa ya Serikali tutakuwa tunajadili taarifa ya Kamati ambayo tulishaijadili wakati Kamati ilipotugawia taarifa zake huko nyuma. Nakumbukuka ilishagawiwa hii taarifa ya Kamati pia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiitazama vizuri taarifa ya Kamati siyo ile iliyotolewa mwezi wa pili. Taarifa hii ilivyosomwa leo, mwezi wa Pili nilimsikia Mheshimiwa Marombwa akizungumzia, lakini nilielewa kwamba ana maana aliyoipokea, Kamati iliipokea kutoka Serikalini ile ya mwezi wa Pili. Lakini ili kuhitimisha, wao wamekaa vikao, maana yake nimeidhinisha vikao na moja ya agenda ilikuwa ni taarifa kuhusu Kiwira. Kwa hiyo, hata taarifa yenyewe ya Serikali ni ya zamani na haina mapya

kwa msingi ule niliousema kwamba tunahitaji mambo yote haya. Basi Kamati ya Nishati na Madini katika vikao vyake ilikuwa inazingatia yote mawili Richmond na Kiwira. Kwa maana hiyo iko katika mtiririko sahihi tu na tunaweza kuijadili. Mheshimiwa Shellukindo endelea!

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe mchangu wangu kidogo kama Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Nilikuwa nasimama kufafanua kitu kimoja. Serikali ilitoa taarifa kama Kauli. Ilitoa Kauli kwenye Bunge hapa na Kauli hiyo hasa imesimama kwenye kitu kimoja zaidi kuuresha mgodi huo.

Lakini Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba mwezi Februari tulipoleta taarifa yetu tulikuwa na pendekezo kwa Serikali kwamba mgodi huo urejeshwe Serikalini. Kwa hiyo, tulipata tatizo kidogo kutosoma ile taarifa, kwa sababu taarifa ya Kamati ina mambo mengi zaidi kuliko ile hoja ya kurudisha mgodi tu.

Kwa hiyo, kwa ajili ya ufanisi wakati tumejadiliana na Mheshimiwa Waziri, tumesema kwamba tumepokea taarifa ile na taarifa ile ina eneo moja ambalo na sisi tumeliunga mkono na tumelipongeza katika hitimisho letu. Lakini kuna mambo ya maana kwa mfano, ule wizi ambao umetokea tarehe 30 tumeletewa mwezi jana. Tuliona haya mambo tuyaunganisha mahali pamoja.

Kwa hiyo, halijaharibika jambo lolote. Taarifa yetu imeunganisha mambo mengi zaidi, kwa mfano watumishi wale, wizi unaotokea na fedha ambazo zinaonekana kwamba zilikwenda kule zifanyiwe kazi, zichekiwe ijulikane kama kweli zimekwenda huku, zimefanya kazi gani. Hii tumeitoa kwa sababu ripoti ya Serikali wanasema kwamba kuna uwezekano wa kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, sisi tunasema kuna uwezekano wa kulipa fidia. Sisi tunasema kuna uwezekano wa kurudisha fedha. Kwa hiyo, haya mambo mawili yaende yakatazamwe. Nimesimama zaidi kutoa ufafanuzi huu. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Shellukindo na huo unatusaidia sana. Sasa napata tatizo kidogo, maana yake haya mambo yaliyotamkwa hapa, Serikali inasema mwekezaji aliyeshindwa alipwe fidia. Kamati inasema, huyu mwekezaji arejeshe fedha alizokabidhiwa ambazo zinaelekea kama zilipotea. Sasa ingekuwa vizuri tupate taarifa ya Serikali hivi sasa kabla hata haujaendelea na haya mengine. Kwa sababu inapingana kabisa. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika hili kama ulivyoongoza ni vyema tulifafanue. Tulisema wakati tunawasilisha Kauli ya Serikali na hatiamaye taarifa ya Serikali kulingana na taratibu zilivyokuwa zimepangwa wakati tunawasilisha hotuba yetu ya Makadirio na Matumizi ya Mwaka 2009/2010. Tumesema pale kwamba baada ya kukubaliana kwamba mgodi umerudishwa Serikalini, tukasema kwamba Serikali itafanya tathmini kwa yale madai yaliyokuwepo kama kuna fedha ambazo zimetumika, wametumia hao wawekezaji wa sasa, lakini nje ya yale

yanayosemekana kuwa ni madeni ambayo Serikali inaweza kubeba majukumu yake, baada ya kuyazingatia yote hayo kuna fedha ambayo imejitokeza kwenye taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini hapa.

Tukisha-*verify* vitu hivyo na Kamati imetushauri kwamba vyombo vyote vinavyohusika ikiwemo Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali *CAG* ahusishwe. Tukishajiridhisha, endapo kutakuwa na *balance* hata kama ni shilingi moja ambayo inaonekana dhahiri inastahili kurudishwa irudishwe. Hilo ndilo angalizo ambalo tuliweka, lakini hatuna maana ya kwamba sasa hivi tumeshathibitisha kwamba Serikali turudishe kiasi chochote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuliweka kwa namna ile kwa kuzingatia mambo yote ambayo yapo ndani ya huu mgodi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimwa Waziri, limekaa vizuri. Namwita sasa Mheshimiwa Fred Mpendazoe.

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nadhani nitachangia kwa kifupi Taarifa hii ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza kabisa naomba niunge mkono taarifa hii na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati na mimi nadhani nitaongezea jambo, nadhani litakuwa jambo moja na zaidi nitazungumzia suala la miiko ya uongozi na kumomonyoka kwa maadili katika nchi yetu. Nadhani ni jambo ambalo litakuwa siyo rahisi sana kulizungumza. Nirudie kusema, kwa kawaida ni rahisi sana kuuzunguka mbuyu, lakini ni vigumu sana kuukumbatia. Lakini leo nataka kuthubutu kuukumbatia. Lakini nadhani siwezi kuukumbatia peke yangu. Naomba kwa kuanza nimnukuu Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kitabu chake cha Nyufa cha mwaka 1995, alisema hivi, nanukuu kwa ridha yako:

*"Sasa Tanzania inanuka rushwa, tunataka kiongozi anayejua hivyo, ambaye atasema rushwa kwangu mwiko. Mwaminifu kabisa kabisa, hawezi kugusa rushwa na wanamjua watu wa rushwa watamjua hivyo. Lakini hatutaki aishie hapo tu, maana haitoshi wewe mwenyewe uwe mwaminifu. Unaweza wewe mwenyewe ukawa mwaminifu kabisa kabisa lakini una shinikizo la ndugu zako, jamaa zako na marafiki zako. Kwa hiyo, sio inatosha wewe kuwa mwaminifu tu, lakini uwe na uwezo wa kuwaambia jamaa zako kwa kauli ambayo wataiheshimu na hawatarudia tena. Utawaambia jamaa na rafiki zako kwa dhati kabisa, Ikulu ni mahali patakatifu. Mimi sikuchaguliwa na wananchi wa Tanzania kuja kupageuza kuwa pango la wahalifu, walanguzi. Na hakuna Serikali mahali popote duniani inayoendeshwa bila miiko."*

Ndio kitu ambacho ninaomba nikiongezee katika yale ambayo yamezungumzwa katika Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, katika Isaya 1:1-10 inaeleza, wakati huo wana wa Israeli, walishuhudia nchi yao ilikuwa inaporwa, utajiri wao unaporwa na wageni. Lakini cha ajabu kabisa walikuwa wakishangilia uporaji wa rasilimali zao wenyewe; ni jambo la kushangaza sana. Lakini katika Isaya 24:1-2, inasema hivi...

**SPIKA:** Uende kwenye Kiwira, eeh!

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Spika, naenda kwenye Kiwira. Kama alivyo Kuhani, ndivyo waumini watakavyokuwa. Nchi yoyote hapa duniani wananchi watakuwa waadilifu na waaminifu kama viongozi wao ni waadilifu na waaminifu. Katika ubinafsishaji wa mgodi wa Kiwira, katika ukurasa wa nne wa Ripoti ya Kamati, umeonyesha wamiliki makampuni manne na wanaohusika pale wameonyeshwa. Lakini kauli ya Serikali iliongezea mmiliki mwingine na alikuwa ameonyeshwa wa kwanza pale katika Kauli ya Serikali. Mmiliki huyo ni Anbern.

Mheshimiwa Spika, naomba nikukabidhi, kama utakubali, nyaraka zinazoonyesha mmiliki huyo Anbern ni nani na mlolongo mzima unaoonyesha jinsi ubinafsishaji ulivyofanyika na ninaomba Watanzania wafahamu na ndugu zangu wengine ambao wameniona mimi labda nina sababu zangu binafsi katika suala hili. Lakini ninataka nizungumze, hoja yangu ni kutaka kuwa na utaratibu wa kuwajibishana wakati, kama mtu aliyepewa dhamana kubwa na wananchi, akienda kinyume na maadili na miiko ya uongozi, tusimwonee haya. Hiyo ndio hoja yangu.

Ukurasa wa nne wa Taarifa ya Kamati, umeonyesha wale wamiliki, kwa kifupi hao wote ni ndugu na marafiki. Ndio nilisema katika kuukumbatia huu mbuyu, nimeomba ninukuu maneno ya Hayati Mwalimu Julius kambarage Nyerere, inawezekana ikawa rahisi kuukumbatia. Lakini ninachotaka kusema, kama hatutazingatia maadili, viongozi tunaopewa dhamana kubwa, ninakuhakikishia nchi yetu miaka mitano, kumi ijayo, tutakuwa na maadili ya ajabu sana, kitu ambacho ni kibaya tutasema ni kizuri na tutakitetea kwa sababu maadili yamemomonyoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaonaje Israel? Utajiri wao unachukuliwa lakini wao wanashangilia! Unaonaje leo Tanzania, Viongozi tuliowapa dhamana kubwa ya kuongoza wanapoamua kujitajirisha wao wenyewe na tunasema wasiguswe! Wakisemwa, wanakejeliwa; hapana! Hayati Mwalimu, alisema tujali miiko ya uongozi na tukijali miiko ya uongozi tutafika mahali ambapo nchi yetu kweli na rasilimali zetu kweli zitawanufaisha Watanzania.

Haiwezekani anapatikana mtu tunampa dhamana, anaanza kugawa utajiri wa nchi yetu kwa rafiki na familia yake, haiwezekani. Tufike hapo tukubali kwamba hilo nalo tuliangalie na sisi Watanzania tubadilike. Kama hatutabadilika na tabia hii hatutakuwa tofauti na enzi za Israel, wakati uchumi wao unachukuliwa wao wanashangilia. Ni afadhali kwamba Kuhani alivyo ni sawa na Waumini ni afadhali kidogo, kuliko waumini wawe sawa na Kuhani. Ni afadhali Kuhani awe sawa na Waumini, lakini ni vibaya sana Waumini kuwa sawa na Kuhani. Kuhani alivyo ndivyo waumini walivyo. Kama Kuhani akianza kuwa mbadhirifu na wengine wataanza kufuata hivyo hivyo, ni afadhali hiyo,

kuna wengine watakataa; kuna kikundi ambacho walikuwa wanasema ni wale wale wanaotaka kusema leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wanaweza wakakataa lakini hatari iliyokubwa ni kwamba, akipatikana Kuhani kutokana na jinsi waumini walivyo, ambapo kama waumini wakawa wameharibika, tunapata Kuhani aliyeharibika, nchi itakwisha kabisa.

Kama Watanzania leo hatutajali maadili ya kuwawajibisha viongozi wanaokiuka miiko na tukasema hakuna tatizo lolote, nchi yote itaoza. Wananchi watasema jambo lolote ni sawa. Nchi nzima ikianza kuliona jambo lolote la uovu ni sawa, atapatikana Kuhani kutokana na jinsi waumini walivyo, itakuwa ni hatari zaidi. Kwa hiyo, tuzuie hilo. Hilo tulizuwie na ombi langu, Viongozi wa Awamu ya III najua walifanya mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi wakati tunakwenda kwenye uchaguzi, nilitaka hata kusema kwamba Rais Mkapa aendelee na wengine ambao walikuwa humo waendelee kwa sababu wamefanya mambo makubwa, hakuna cha ajabu hapo, ni kweli kabisa! Lakini ndani ya pazia hilo kuna matatizo ambayo tunayaona hapa na ni lazima tuyarekebishe na tuyaweke wazi watu wajue na tujue kwamba haya hatuyataki tena. Tukiyaficha kama watu wengine wanavyosema kwamba tusioneshe hiki kitu, hapana! Ni lazima kitu kifahamike, *where there is no pain there is no gain.* Ni jambo linaloumiza, lakini tukilikubali litaleta faida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba waliohusika, waliokuwa Viongozi wa Awamu ya III, tuliyoiheshimu sana wajitokeze wawaombe msamaha Watanzania. Vinginevyo Serikali ya Awamu ya IV ambayo iliapa kuilinda Katiba, haikuapa kulinda Serikali ya Awamu ya III, isiwaonee haya wote waliohusika katika tatizo hili, waliokuwa viongozi. Ninarudia, Serikali ya Awamu ya IV ambayo ina heshima kubwa sana sasa hivi, haikuapa kuilinda Serikali ya Awamu ya III na Serikali ya Awamu ya III haikuapa kuilinda Serikali ya Awamu ya II, waliapa kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, Serikali ya Awamu ya IV iliyo na heshima kubwa sana isione haya kuwaonea haya wale waliohusika na ubadhirifu au na ubinafsishaji ulio holela wa Mgodi wa Kiwira, waliokuwa Viongozi wa Awamu ya III. Kama hawatataka kujitokeza na kuwaomba msamaha Watanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, tafadhali kaa chini. Nikukumbushe tu kuhusu Kanuni ya 64(1)(b), inasema hivi: "*Wakati wa kuchangia Mbunge, hataruhusiwa kuzungumza jambo ambalo haliko kwenye mjadala.*" Sasa suala la Awamu ya IV kuidhibiti ya III, halipo kwenye mjadala, tunazungumzia suala la Kiwira. Nilikuwa ninakuomba uende hapo na kama umemaliza basi.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, ngoja nimalizie basi. Ninashukuru kwa kunikumbusha nirudi pale, basi nilichokuwa ninaomba ni kuhitimisha

mchango wangu. Basi nilikuwa ninaomba wale waliohusika katika ubinafsishaji holela wa Mgodi wa Kiwira ambao walikuwa ni Viongozi, itakuwa ni heshima kubwa sana hata kwao wakisimama wakieleza na ikiwezekana wakawaomba msamaha Watanzania na itatusaidia sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hali ya mjadala uliopo, hicho unachokifanya ni kama kufunga zizi baada ya ng'ombe wote kutoroka. Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa, msemaji wa mwisho ni Mheshimiwa Magalle Shibuda. *(Makofi/Makofi)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia tafakari na maoni kuhusu masuala ya rasilimali zetu za Tanzania. Leo hapa tumekuwa na ajenda kuhusu rasilimali zetu za Kiwira, palikuwa na *Richmond.*

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya hapo, naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni mwana *CCM* asilia ambaye ninaweza kutetea Ujamaa na Kujitegemea, Azimio la Arusha, kwa hiyo, kauli yangu itakuwa ni msisitizo kwa rasilimali zetu na azma yangu ni kwamba ninataka kutoa maoni ya mwelekeo wa kutekeleza ushauri kwa Serikali. Kwa hiyo, unapotoa ushauri kwa Serikali, ni kuinufaisha Serikali iweze kujihami ama kujikosoa katika makosa ambayo imekuwa ikiyafanya kwa uhitaji wa mustakabali wa mema kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Kikwete kwa juhudi zake za kuhakikisha anarejesha uwajibikaji na ndio maana amekuwa akitoa fursa ya masuala mbalimbali kusemwa hadharani ambayo yalikuwa ni ya makosa. Hii ni watu wajikosoe na Taifa letu lirejee kwenye maadili.

Mheshimiwa Spika, Bunge halimwonei mtu, lakini Wahenga husema uchafu hausafishi uchafu na sabuni ya mkaa haiwezi kufulia kanzu nyeupe. Hapa tuna jambo moja muhimu sana. Tuna mihimili mitatu; tuna Bunge, tuna Serikali na Mahakama. Hapa tunazungumzia matatizo yaliyotokea Kiwira na leo tumeanza kuelekea katika fursa njema ya kujisahihisha. Lakini ninaomba kutoa ushauri kwamba, makosa ya mtu binafsi yasitumike kufichwa kwa jina la Serikali. Serikali nayo isihami makosa ya mtu binafsi kusema kwamba ni kudhalilisha Serikali.

Dhamiri ya mantiki ya kuiita Serikali ni mfumo, lakini udhaifu wa Askofu sio udhaifu wa Biblia, udhaifu wa Sheikh sio udhaifu wa Msahafu. Sasa inakuwaje mtu binafsi akifanya makosa, akikosolewa au akisutwa au akizomewa uambiwe unaiaibisha Serikali! Unaiabishaje Serikali? Serikali haina makosa, udhaifu binafsi usilindwe na hivi sasa panataka kuzuka tabia ya kuhami uovu wa watu binafsi kwa jina la kwamba unaaibisha Serikali. Naomba hilo liondolewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hatujengi ufanisi wa kuisadikisha Serikali kwa wananchi, hatujengi uadilifu wa kuisadikisha *CCM* panapokuwa na makosa ya watendaji binafsi, haya yote ni kupunguza kura za *CCM.* Kwa hiyo, ninaomba haya yaliyotufikisha ikazaliwa Kiwira, ikazaliwa *Richmond,* haya yote ni maovu kuhusu rasilimali za

Tanzania. Kiwira, ni jina kwa maslahi ya Tanzania. Naomba Serikali ithibitishie Watanzania inachukua hatua gani kwa wale wote waliozua mgogoro na hatimaye pakazaliwa tatizo la Kiwira? Ithibitishieni Tanzania uadilifu enyi mliopewa dhamana ya kuitwa Serikali, kama hamwezi kuithibitishia Tanzania, ina maana na nyie ni wateja wa dhamana hizo za dhuluma.

Naomba Kitengo cha Sheria cha Bunge, kiandae Muswada uletwe hapa hivyo Serikali tunapoishauri jambo ikawa haitaki kutekeleza, sasa pawe na sheria ya kuwawajibisha. Wanataaluma wa Bunge, Wanasheria walete hapa Muswada. Utatusaidia sisi kuisimamia Serikali, huwezi ukasimamia mtu, huna wajibu wa kumuwajibisha. Kwa hiyo, haya ya zamani yaliyokuwepo basi na sasa tubadilike, kwa sababu pana viburi vya uhondo wa madaraka, hivi viburi sasa ni lazima viondolewe. *(Makofi/Kicheko)*

Hivi tunaposimama hapa tunawasema Mawaziri: Je, Makatibu Wakuu, wana uzalendo wa kuisadia *CCM* ishinde? Wana uzalendo gani? Maana hapa tusiwaseme Mawaziri tu, lakini Makatibu Wakuu na wasaidizi wao, kwa sababu Washauri wa Mawaziri ni Makatibu Wakuu, *garbage in, garbage out.* Uongo ndani, uongo nje! Kwa hiyo, niliona hili niliseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanawajua watu wao ambao wanazungumzia maslahi ya Taifa. Ninakupongeza wewe na ninaiomba CCM ikuunge mkono na ninaiomba CCM irejeshe jina lako kugombea tena Uspika, pamoja na vimeta ambao hivi sasa wapo. Naomba kwa sababu umegeuza Bunge, sasa linazungumzia maslahi ya umma sio Baraza la Kutunga Sheria peke yake, naiomba Serikali na Wajumbe wa Kamati Kuu mnapokaa huko, aidha, hata siku mkijadili jina lake, mpeni *A*, japo anaweza kupewa alama za ajabu ajabu eti *C* ajaribiwe, ajaribiwe kitu gani na huyu ni hodari! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukaidi wa kukataa ukweli, haubadilishi hadhi ya ukweli, bali unachelewesha ukweli kutekelezwa. Toka tumeanza kujadili masuala ya *Richmond* na Kiwira, ni muda gani? Mnachelewesha nini? Mnajihami kitu gani? Hii Serikali ya CCM, Mawaziri wa CCM, Baraza la Mawaziri la CCM, Makatibu Wakuu si wa CCM*!* Ndio! Kwa hiyo, tufike mahali mjiulize. Naomba kutoa angalizo na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alichukue kwa haja kubwa sana ya tafakari zake.

KANU imeondolewa madarakani na nani? KANU imeondolewa madarakani na watumishi wa Serikali waliokuwa na machukizo hatimaye KANU ikaonekana ni chama kibovu kikaondolewa madarakani. *UNIP* imeondolewa madarakani. KANU ilipokuwa madarakani ilikuwa na viongozi wa chama na ilikuwa na watumishi wa Serikali na Viongozi wa Serikali, sasa machukizo yenu yatapunguza kura za CCM. Mnataka kutung’oa, mnataka kutung’oa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wasimamie waambie hatung’ooki, tutawang’oa wao!

Mheshimiwa Spika, lete sheria tuwaadabishe hawa! Kitengo chako cha Sheria, kiandae Muswada na kilete hapa tupate jinsi ya kuwaadabisha watu. Ninaomba sana hilo lifanyike. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, dhamiri ya Serikali iwe kwa maslahi ya umma. Kuna maonevu mengi yanafanyika, lakini kasi ya kutoa maamuzi na kuchukuliwa hatua kwa aliyesababisha maonevu na machukizo, ni dhaifu, ni dhaifu! Tumesikia maonevu ya wafugaji, katika uamuzi upo udhaifu, lakini hakuna hatua. Tumesikia masuala ya *Richmond,* napo udhaifu upo, masuala ya Kiwira, yamechukua muda wote huu! Ndugu zangu, hivi tunakwenda wapi? Tunasema tunataka kushika hatamu za uchumi, tunasema *TANU* imepigania uhuru ni maendeleo, mapinduzi matukufu ya Zanzibar yamefanyika, uhuru ni maendeleo kwa Watanzania, leo tuko wapi? Tunashika hatamu? Hatukutafuta uhuru huu Watanzania wawe masikini.

Mheshimiwa Spika, sina ugomvi na Watanzania kuwa na hisa katika makampuni, lakini wafuate taratibu, sheria na kanuni. Sio tunajenga wajanja wachache ambao wanakuwa mawakala wa mirija ya ukoloni mamboleo; mirija ya ukoloni mamboleo ipo. Je, mabaki ya ukoloni mamboleo yamekwisha? Ninaomba sana hilo suala lisimamiwe. Serikali itoe huduma kwa maslahi ya kuendeleza uhuru wa Mtanzania wa kushika hatamu. Lakini ikiwa Mwekezaji atalalamika mtaleta Muswada haraka, lakini tukizungumzia maslahi ya Tanzania kwamba kuna dhuluma, ugoigoi unatokea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukweli ameyakuta lakini ndivyo hivyo ukiamua kuwa baba wa kufikia ni lazima uyakubali yote. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwasababu ni baba wa kufikia basi atoe malezi. Chapa bakora kama watoto walikuwa wanarudi saa 9.00 basi warejee saa 4.00. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ajenge kumbukumbu kwamba alifanya kazi na Baba wa Taifa. Najua anaelewa mengi, anapata kigugumizi gani? Lete hapa Bungeni tukusaidie! Lete Bungeni tuwashughulikie hao! Kama utaona unashindwa, ni bora ujiuzulu ulinde heshima yako na uadilifu wako kuliko kuendelea kukaa Uwaziri Mkuu, lakini je, hao unaowaambia wana viburi, wana jeuri, wanasingizia kwamba ni marafiki wa watu wakubwa! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Bunge ni kwa maslahi ya nchi. Ninaomba sana walioko Serikalini mwelewe ya kwamba Wabunge ndio wanaosimama kwenye majukwaa kuitetea *CCM.* Katibu Mkuu wa Wizara haendi kwenye jukwaa, Mkuu wa Mkoa haendi kwenye jukwaa, *DC* au Mkurugenzi, hawendi kwenye jukwaa, sasa mtusikilize sisi ndio tunaosimama kwenye majukwaa. Je, *CCM* ikianguka Makatibu Wakuu watachekelea ama watasikitika? Watasema sisi ni *Public Officers any Government in power,* kila Serikali iliyoko madarakani sisi watwana wake, alaah! Tokeni hivi sasa kabla ya *CCM* haijaondoka.

Mheshimiwa Spika, kiwira tusingekuwa tunaijadili hapa leo. Ninakupongeza kwa ujasiri wako wa kuhakikisha kwamba rasilimali za Tanzania zinalindwa. Binadamu unaweza kumpa ushauri, lakini huwezi kumpa tabia njema. Wapo Makatibu Wakuu hata ukifanya nini, unageuza huku na huku kuwahamisha, hawabadiliki tabia zao! Hulka na silka zao ni dhalimu! Waondoeni wapumzisheni. Wako watu mnawapa dhamana za

Uwaziri, mmewaonea kuwapa madaraka hayo, wapumzisheni! Wawawezi wakasema hawawezi! Hata mtoto si riziki, hupeleka posa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, asiye kinyume na binadamu, yuko na Mwenyezi Mungu. Nashukuru, naunga mkono hoja ya Kamati. Kengele ya mwisho hiyo? *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE:** Eeh!

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, ahsanteni. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilimtahadharisha Mheshimiwa Shibuda, lakini kama kawaida amechukua muda wote wa robo saa.

Bila kutaja jina, nilipokea hapa ushauri ambao nauona ni mzuri tu kwamba suala hili halijaiva, Serikali imetakiwa na Kamati kutekeleza mambo kadhaa, hayajatekelezwa. Kwa hiyo, linafanana fanana na lile tulililoliacha lile, tulilolisogeza mbele. Lakini natoa nafasi kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ili pengine kama ana majibu sasa, lakini mimi nilikuwa naliona kama bado, kwa sababu baada ya tamko lake ndio Kamati imetoa maelekezo haya.

Kwa hiyo, tamko lilihusu tu suala la Serikali kuchukua hisa zote za Kiwira, lakini yale mambo mengine ya fidia na nini, mengine yote yale bado, mali zilizoibiwa bado. Sasa sijui kwa maoni yangu itakuwa ni ahueni na kama Kamati itakubali, Mwenyekiti atakubali, hili nalo liweze kusogea mbele ya Mkutano wa 17.

Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninakushukuru wewe binafsi, ninaishukuru Kamati ya Nishati na Madini chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Shellukindo. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao, maoni na ushauri mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu umetoa Mwongozo, ni kweli kuna mambo ambayo baada ya sisi kutoa Kauli ya Serikali na hatimaye kutoa Taarifa wakati wa hotuba yetu, yamejitokeza kwa mfano yale mambo ya wizi wa baadhi ya vifaa. Lakini Serikali imeshaanza kuchukua hatua kwa kuzishirikisha mamlaka na ngazi zote za Kiserikali kuanzia ngazi ya Wilaya na sisi Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, mambo mengi ambayo yamejitokeza hapa kwa ngazi ya Kamati, tumeshayajadili lakini kama ilivyojitokeza, yapo mambo mengine ambayo ni ya utekelezaji. Kwa mfano, ufuatiliaji wa mali, tathmini ya mali iliyoibiwa, kwa kweli haya ni masuala ya utekelezaji, lakini mambo ya msingi makubwa tulishayajadili kwenye Kamati. Nachelea kusema kwamba tulikubaliana, lakini kwa sababu taarifa imekuja hapa kwenye Bunge lako Tukufu, ni vyema na tunashukuru tunaendelea kupokea ushauri.

Mhweshimiwa Spika, niseme machache. Moja limejitokeza hapa wakati Taarifa inawasilishwa, nifafanue kuhusu umiliki wa hisa. Kamati yetu ilipotembelea Mgodi wa Kiwira, ilipata taarifa ambazo ukiziangalia kwenye taarifa iliyowasilishwa zinaonyesha kama mgongano wa umiliki wa hisa: Je, Serikali ina asilimia 18, 12, 30 ama 15?

Mheshimiwa Spika, suala la Mgodi wa Kiwira lina sura mbili. Kwanza kuna umiliki kuhusu Mgodi wenyewe na katika huo umiliki kuna mpangilio wa hisa. Kwenye Mgodi wa Kiwira, wawekezaji wana hisa asilimia 70 ambazo ndio Taarifa ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ametoa hapa. Huo umiliki wa hisa hizo asilimia 70 ulifanyika kwa utaratibu wa *subscription*, wataalamu wa mambo ya Sheria mnajua. Unaweza kuongeza hisa za Kampuni kwa aina mbili, kwa kuzizalisha ama ukanunue kwa makampuni mengine na kuziunganisha na kampuni ambayo inaendelea, utaratibu uliotumika kwenye mgodi huu mpaka wakati ambapo mgodi ulipokuwa unabinafsishwa. Mgodi wa Kiwira ulikuwa na hisa 120 zenye thamani ya Shilingi milioni 120 kwa sababu kila hisa ilikuwa na thamani ya Sh. 1,000/=.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati mazungumzo yanaendelea, nimesema kabla ya kuhitimisha mikataba ya ubinafsishaji wa ule mgodi, Serikali na wawekezaji wakaona ni busara kwa sababu mtaji ulikuwa ni Shilingi milioni 120 tu, ulikuwa hautoshi. Wakasema sasa watumie utaratibu wa kuongeza hisa, ile *subscription.* Wakaziongeza hisa hizo ziwe nyingi zifikie milioni moja na kwa sababu kila hisa ina thamani ya Sh. 1,000/= maana yake sasa ni kwamba mtaji ulipanda kutoka Shilingi milioni 120 hadi Shilingi bilioni moja. Hivyo wakati mwekezaji anakuja na kwa sababu mazungumzo yalikuwa ni kwamba yeye atakuwa na hisa asilimia 70, ukichukulia zile hisa 120 zilizokuwepo zenye thamani ya Shilingi milioni 120, walitengeneza sasa hisa nyingine kufikisha hisa milioni moja. Hisa 880,000 ili sasa iwe hisa zinazopatikana ni milioni moja zenye thamani ya Sh. 1,000/= na hivyo unapata thamani ya Shilingi bilioni moja kama mtaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu makusudio ya kuwakaribisha wawekezaji ilikuwa ni wamiliki asilimia 70, wao waliuziwa hisa 700,000. Hivyo kwa sababu kila hisa ilikuwa na thamani ya Sh. 1,000/= ndio yale malipo ambayo tumekuwa tukiyasikia wakawa wamenunua zile hisa ambazo zilitengenezwa kwa makusudi ya kufanya kampuni ionekane ina mtaji mkubwa, iweze kukopesheka na kujiendesha kibiashara. Ni utaratibu wa kawaida katika biashara. Hivyo wakauziwa hisa 700,000 zilizotengenezwa, zilizoongezwa; sio ambazo zilikuwa zinamilikiwa na Serikali. Serikali ikabaki na umiliki wake wa hisa 120 zenye thamani ya Sh. 1,000/= kama ambavyo ilikuwa kabla. Sasa baada ya kujumlisha hizo hisa 700,000 ukajumlisha na hisa 120 ambazo ni za Serikali, unapata hisa 820,000. Lakini kwa sababu mtaji umefikia Shilingi bilioni moja kwa maana ya hisa milioni moja, kuna *balance* ya hisa 180.

Baada ya kujumlisha hizo hisa laki saba ukajumlisha na hisa mia moja na ishirini ambazo ni za Serikali, unapata hisa laki nane na ishirini elfu. Lakini kwa sababu mtaji umefikia bilioni moja kwa maana ya hisa milioni moja kuna *balance* ya hisa 180. Kwa sababu makusudio ya kumkaribisha mwekezaji ilikuwa ni kuchukua asilimia sabini kwa mazingira yale, tusingesema zile hisa 180 zimebaki hazina mtu kwa sababu ni za Serikali,

ndiyo maana tunasema Serikali ilibaki na asilimia 30 kwa maana ya kwamba hisa ilizokuwa nazo 120 ukijumlisha na 180 ambazo baada ya mtaji kufikishwa hisa milioni moja kwa hisa bilioni moja haziwezi kubaki zina-*hang* ndiyo maana kuna Serikali, ndiyo maana kukawa na mgawanyo.

Mheshimiwa Spika, sasa kumekuja mkanganyiko, kuna taarifa ilitoka kwamba hisa za Serikali ni asilimia kumi na tano, kwenye mgodi Serikali asilimia thelathini na wawekezaji wanamiliki asilimia sabini kwa mgawanyo huo niliouelezea.

Mheshimiwa Spika, kwenye mkataba wa umeme na wawekezaji ambao shirika la umeme liliingia pale, ndiko ambako Serikali ina asilimia kumi na tano lakini wawekezaji walikuwa na asilimia 85, hapo kulikuwa na mambo mawili ambayo napenda niyafafanue kama ambavyo nimefanya.

Mheshimiwa Spika, kuna swali limejitokeza kwamba kampuni hizi wanahisa walikuwa vipi. Tulitoa kwenye kauli yetu na baadaye kwenye taarifa wakati tunawasilisha bajeti yetu, kampuni ya wawekezaji iliyokuja kumiliki hizi asilimia sabini ilisajiliwa tarehe 29 Desemba 2004. Tarehe 10 Januari siku 13 baada ya kampuni hiyo kusajiliwa, kampuni mojawapo ambayo walikuwa waanzilishi wa hiyo kampuni ya *TANPOWER Resources* walijiondoa kwa kushindwa kulipia hisa zao.

Mheshimiwa Spika, naamini watalaam wa mambo ya fedha na mambo ya makampuni akina Mheshimiwa Kaboyonga, Mheshimiwa Dokta Mwakyembe mnafahamu. Ukianzisha kampuni ni jambo la kawaida wale waanzilishi au wale *promoters*, wanaweza hata kuchukua hisa moja moja tu lakini mnataka kufanya shughuli ya mabilioni ya fedha kwa minajili ya usajili. Katika sheria za makampuni ni mambo ya kawaida, lakini ili mhalalishe umiliki wenu na mpate ile hati ya usajili inayoita *certificate of shares*, ile hati ya umiliki wa hisa ni lazima kama mmetaja kwamba kila hisa itakuwa na thamani fulani lazima mzilipie na huwa kuna *certificate* ambazo zinajulikana kwa wale wanaofahamu mambo ya makampuni. Lakini huwezi kuwa na *certificate* ile kama hujalipia. Hii kampuni pia ilishindwa, hivyo ikajitoa.

Mheshimiwa Spika, nataka niendelee kuweka wazi kwamba wakati inajitoa tarehe 10 mwezi Januari mwaka 2005 mkataba wa kuuza hizo hisa asilimia 70 kwenye mgodi wa Kiwira ulikuwa haujafungwa. Mkataba wa makusudio wa kufunga ulifungwa mwezi wa tatu tarehe 24 mwaka 2006. Kulikuwa na mchakato wa mazungumzo pale.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kusema baada ya hapo mkataba wa makusudio au *agreement of intent* haukuhalalisha umiliki wa asilimia sabini kwa kampuni ya *TANPOWER Resources* kwenye mgodi wa Kiwira hadi mkataba wa mauzo ya mkataba wa hisa zile sabini ulipofanyika mwezi wa Sita. Mkataba sasa wa kuuza hisa asilimia sabini ulikamilika mwezi wa Sita 2006.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa kuingia kwa ajili ya uzalishaji umeme ulifungwa, ilikuwa na mikataba mingi, tulitoa taarifa pale zikiwepo *EXCO ACCOUNT*

*implementation agreement* na vitu vingine. Mkataba ule ulifungwa mwezi wa Nane mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niliweke wazi hili kuhusu kampuni iliyokuwa inaitwa *ANIBEN* na kutokuwepo, kwa hivyo, baada ya kulifafanua hilo niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri mliotupa. Kamati yetu imetupa ushauri mzito sana na tunajadiliana sana kwenye vikao vyetu na tumekubaliana mambo ya msingi ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hao wachangiaji ambao wamechangia namshukuru sana Mheshimiwa Marombwa kwa kuwasilisha taarifa ya Mheshimiwa Shellukindo kama Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mpendazoe na Mheshimiwa John Shibuda, tunauchukua na tunauzingatia lakini kimsingi mambo ya msingi tulishayafanya na Serikali inachukua ule mgodi sasa, tunachofanya sasa hivi ni kuzihusisha mamlaka zote za kitendaji za Serikali kuhakikisha kwamba inafanyika tathmini ya kuona kinachostahili kurudi Serikalini ni pamoja na mambo yapi na kama endapo itajitokeza kukawa na kitu ambacho kinastahili kwenda kwa mwekezaji niseme kwa nia njema kabisa, kama kitakuwepo kitu tutafanya hivyo, lakini baada ya kuzingatia mambo yote yakiwemo madeni ya wafanyakazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba niliahidi Bunge lako kwa niaba ya Serikali kwamba tupo makini tunalifanyia kazi jambo hili vizuri, tumeshaongea na Serikali ya Wachina, ule mkopo wa milioni mia nne Dola za Kimarekani ambao vinginevyo ulikuwa unajadiliwa na kampuni hii ya uwekezaji. Serikali tulishaji- *commit* na Serikali ya China iko tayari kushirikiana na sisi kutupatia fedha za kuendeleza ule mgodi.

Mheshimiwa Spika, habari njema ni kwamba katika mradi huu Serikali haitaanza kuanzia mwanzo kufanya tathmini ya upembuzi yakinifu. Jambo hili lilishafanyika na hayo sisi tunayachukua kwa sababu lengo letu ni kuzalisha umeme na tunaambiwa inawezekana tukazalisha umeme ndani ya miezi 18, tukichelewa sana miezi 20.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA**: Nashukuru sana kwa ufafanuzi huo, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ili aweze kutusaidia namna ya kwenda mbele kwa sababu kwa maoni yangu linafanana na lile tulilokwishalimaliza.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya mwasilishaji ningependa kuliomba Bunge lako Tukufu kwamba sasa ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini uchukuliwe na Serikali na kwamba ufanyiwe kazi na Wizara ya Nishati na Madini na kwenye Bunge la Mkutano wa Bunge wa Kumi na Saba tupate taarifa ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja hii.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki Utekelezaji wa Hoja ya Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini Kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu mchakato wa Zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura ulioipa ushindi Richmond Development Company LLC ya Houston Texas - Marekani Mwaka 2006)*

*(Bunge liliafiki Utekelezaji wa Hoja ya Taarifaya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Taarifa ya Serikali kuhusu Ubinafsishaji wa Mgodi wa Kiwira)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda na kwa hiyo tunaliacha hili mikononi mwa Serikali nalo ili tuweze kupata kitu kilicho kamili kwenye Mkutano wetu wa Kumi na Saba. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu leo kutakuwa na hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na muda sasa umekaa vibaya namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano aweze kutoa hoja ili shughuli za Bunge ziendelee hadi hapo hoja ya kuahirisha Bunge itakapotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

## HOJA YA KUONGEZA MUDA WA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kutoa hoja kwamba, muda wa leo uongezwe hadi hapo hotuba itakapomalizika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge hoja ya kuongeza muda wa shughuli za Bunge imetolewa hadi hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapomaliza hoja yake ya kuliahirisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge sasa ili nimpe nafasi Mheshimiwa Waziri kukamilisha hoja yake bila tena kuwa na mambo mengine, naomba nimalizie viporo viwili, kimoja ni taarifa ya awali ya Kamati Maalum niliyoiunda kwenda North Mara kuchunguza kuvuja kwa kemikali za sumu toka mgodi ule.

Kwa kifupi chimbuko la shughuli hii mnalifahamu na taarifa hii nitaisambaza kwenu, lakini baada ya Kamati kurejea niliahidi mbele ya Bunge kwamba nitatoa taarifa ya awali

ya hayo ambayo waliyaona. Baada ya Kamati kutembelea maeneo yaliyoathirika ya Kata za Kemambo, Kibasuka na Matongo, pamoja na mgodi wa North Mara, Kamati ilishuhudia na kujionea mambo yafuatayo:-

(i) Kuwepo kwa vumbi, milipuko ya baruti na mawe yanayoruka *flying stones*, ambayo yanawasilisha afya za wananchi wanaoishi jirani na mgodi wa North Mara.

(ii) Uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na kutiririka kwa maji yenye kemikali ya sumu itokanayo na miamba kwenda kwenye vyanzo vya maji pamoja na vijito, mashamba na mto Tigite, ambao umesababisha mimea na uoto wa asili kukauka na hakuna dalili za viumbe hai kwenye mto huo na vijito hivyo.

(iii) Kurundikana kwa udongo, *stock tile* na udongo wa tope unaotiririsha maji yenye kemikali kwenda kwenye mashamba, vijito na vyanzo vya maji.

(iv) Kuvuja kwa bwawa linalohifadhi maji ya kemikali ya *Cyanide* inayohatarisha maisha ya binadam, mifugo na mazingira.

(v) Kuwepo zulia na vifaa vya kuzuia maji yenye kemikali za sumu yaani *lines* kwenye mabwawa yote ya kuhifadhi maji yenye kemikali.

(vi) Kuwepo kwa idadi ya watu wengi wenye magonjwa mbalimbali kama ya ngozi, upele na kupooza yanayosemekana kusababishwa kwa kutumia maji ya mto Tigite.

(vii) Kukiukwa vipengele vya mikataba, kati ya mwekezaji, wananchi na Serikali ambako kumesababisha mahusiano duni kati ya wananchi wa maeneo husika na mwekezaji *Barrick Gold Limited* ambapo imepelekea kuwepo kwa vitendo vya wizi na ubadhirifu wa mali za mgodi, malalamiko ya mauaji yanayofanywa na Jeshi la Polisi pamoja na walinzi wa mgodi na kuwepo kwa wizi wa *liners* na uharibifu na uchomaji moto wa magari na mitambo pia kujeruhi watumishi wa mgodi na ubomoaji huo.

Waheshimiwa Wabunge nimepokea taarifa ya awali ya Serikali iliyozama kwa kina katika masuala haya. Kutokana na hilo hayo yote mawili sasa kupokea taarifa ya awali ya Kamati Maalum niliyoiunda na taarifa ya Serikali, uamuzi wangu ni kama ifuatavyo;

Baada ya kupokea maoni hayo ya awali ya Kamati ya Wabunge waliotembelea mgodi wa North Mara, na tathmini ya Serikali ambazo zote zinahitaji uchambuzi wa kina, nawasilisha suala hili katika Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ili Kamati hiyo iunde Kamati ndogo kwa mujibu wa kanuni ya 114(18) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 kwa ajili ya kupitia taarifa zote sasa na kazi hiyo sasa waikamilishe na kutuletea katika Mkutano wa Kumi na Saba. Katika kuunda Kamati hiyo ndogo, naomba Mwenyekiti ashirikishe pia wajumbe wachache wa Kamati ya Nishati na Madini ili

waweze kufanya kazi kwa pamoja, huo ndiyo uamuzi wangu na kwa sasa suala la North Mara linakaa katika sura hiyo.

Lakini naisihi Serikali kwa yale mambo ambayo yanaweza kuwa na athari kubwa kwa wananchi na mifugo na mimea, basi tusisubiri mwezi Novemba, ni dhahiri kwamba harakati nyingine zifanyike ili kuwaokoa wananchi.

La pili, Waheshimiwa nimepokea malalamiko kutoka kampuni ya *TDI Consultancy* wakimlalamikia Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa CCM Kigoma Kusini kwa maneno makali sana, waliona yamewakashifu na kuwaharibia hata biashara zao. Maneno haya aliyatoa tarehe 21 Julai, 2009 na chini ya kanuni 71(1) wawekezaji hao wamelalamika kwamba wameonewa na Mheshimiwa Serukamba hakuwatendea haki. Kwa hiyo nayachukua malalamiko yao, na kuyapeleka kwenye Kamati ya Maadili ili yashughulikiwe kama ambavyo inapaswa.

Waheshimiwa Wabunge, nitoe tahadhari hasa kwa wale Wabunge ambao hawaiangalii vizuri hii kanuni 71. Kanuni hii inaruhusu mtu ambaye ukimponda sana ukadhani unamaliza hasira zako, mara nyingine yanaweza kurudi tena yakawa ni mambo magumu kwako.

Mengine, Waheshimiwa Wabunge tarehe 3 Agosti, 2009 yaani kesho kutwa, Mheshimiwa Rais mnamo majira ya asubuhi, nadhani saa nne atakuja kuzindua kauli mbiu ya KILIMO KWANZA, kwenye maonesho ya nane, Viwanja vya Nane Nane, barabara ya Dar es Salaam hapa Dodoma. Waheshimiwa Wabunge wote ambao watakuwa wapo na hususan wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, tafadhalini sana tuweze kushiriki asubuhi ya kesho kutwa, msiwe na haraka wale wote mtakaobaki hapa Katibu ataangalia namna mtakavyoishi hapa. Kwa hiyo, hilo lisiwe kikwazo. Katibu unasikia, nane nane, asubuhi kesho kutwa tarehe tatu.

Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto ameniomba nitangaze kwamba leo katika ukumbi Na. 227, wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, mkutane kwa kikao kifupi cha dharura mara baada ya kuahirishwa Bunge.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, pia anaomba mara baada ya kuahirishwa Bunge, wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii mkutane katika ukumbi nadhani utakuwa 231 baada ya kuahirisha Bunge.

Nami pia nawaita kwenye kikao wajumbe wote wa Tume ya Huduma za Bunge, tukutane tuna kazi kubwa sana mbele yetu, tumekwishapitisha, *CDF* sasa tunasonga mbele tutashughulikia masuala ya Bima ya Afya kwa Wabunge, Bima kwa maisha ya Wabunge na masuala ya mafao yao Wabunge wanapostaafu. Mimi nikiwa Spika naamini kabisa kuimarisha Bunge ni kuwaimarisha Wabunge, wasipokuwa na uhakika wa hali zao, huwezi kuwategemea wakawa wajasiri au wakafanya mambo yanayotegemewa. (*Makofi*)

Kwa hiyo tunakwenda mbele, tumemaliza *CDF* tunapambana na hayo matatu, najua kutakuwa na upinzani wa kawaida lakini tutaumaliza kama tulivyoumaliza ule wa *CDF*.  Kwa hiyo Tume ya Huduma mara baada ya kuahirisha Bunge tukutane Ukumbi wa Spika

Waheshimiwa Wabunge,  baada ya kusema hayo sasa..., kumbe taarifa hatujaipata na mimi nama-speed yangu bwana!  Katibu tutolee taarifa jinsi ilivyo.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limemaliza kuchambua shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano wa Kumi na Sita.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa.

**SPIKA:** Asante Katibu kwa taarifa hiyo.  Naomba Waheshimiwa Wabunge tutambue uwepo wa mgeni mashuhuri ambaye ni mama yetu Mama Tunu Pinda, yuko pale.  Kweli mshikamo huu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na mkewe Mama Tunu Pinda ni mshikamo ambao wengine mnatakiwa kuiga.  Maana yake naona wengine mambo yenu.., haya basi.  Sasa Kwa heshima na tahadhima namkaribisha Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kutoa hoja ya kuliahirisha Bunge.

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge lako Tukufu ambao ulianza tarehe 9 Juni 2009 hapa Dodoma.  Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuongoza, kutusimamia, kutulinda na kutuweka salama hadi siku ya leo tunapohitimisha Mkutano huu.  (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niungane nanyi tena Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Watanzania wote kutoa pole kwa kifo cha aliyekuwa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mwanazuoni Maarufu nchini na Afrika nzima, Profesa Haroub Othman ambaye alifariki Dunia tarehe 28 Juni, 2009, Kisiwani Zanzibar.  Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Spika huyu alikuwa ni mwalimu wangu aliyenifundisha Chuo Kikuu. (*Makofi*)

Vilevile, natoa pole kwa Watanzania wote kwa kifo cha aliyekuwa Kaimu Mufti wa Tanzania, Sheikh Suleiman Gorogosi aliyefariki kwa ajali ya gari Mkoani Lindi, tarehe 27 Juni, 2009.  Nitumie fursa  hii  pia  kutoa Salaam za Pole kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki  na  mali kutokana na ajali, maradhi na sababu nyingine mbalimbali wakati tukiendelea na Mkutano huu hapa Dodoma.  Ni hivi majuzi tu tarehe 26 Julai 2009 ambapo Taifa limepoteza Watu 28 na idadi imeongezeka kidogo kwa ajali ya basi la Abiria la Mohamed *Trans* iliyotokea Wilaya ya Korogwe, Mkoani Tanga. Ni dhahiri kuwa, wote waliopoteza maisha tuliwahitaji sana katika Maisha yetu na tuliwapenda, lakini Mwenyezi Mungu amewapenda zaidi na kukubali watutangulie mbele

ya haki. Naungana na ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu wote kumwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahala pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Biharamulo kupitia Chama Cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mdogo uliofanyika tarehe 5 Julai 2009. Kuchaguliwa kwake kunadhihirisha kwamba wananchi wana imani kubwa kwake na kwa Chama Cha Mapinduzi. Kurejeshwa kwa Jimbo la Biharamulo kwa Chama Cha Mapinduzi ni uthibitisho tosha kwamba Chama Cha Mapinduzi kina Sera zinazokubalika kwa wananchi na hakuna shaka kitafanya vizuri katika Uchaguzi ujao wa mwaka 2010. Navipongeza pia Vyama vyote vya Siasa vilivyoshiriki kwenye Uchaguzi huo ambao pamoja na kuonyesha ushindani wa hali ya juu pia uliifanya Tanzania kuudhihirishia ulimwengu kuwa imekomaa kwenye demokrasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano huu, Bunge lilifanya Uchaguzi wa Wajumbe katika Tume ya Huduma ya Bunge. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge Kidawa Khamid Salehe na Magdalena Hamisi Sakaya kwa kuchaguliwa kuwa Makamishna katika Tume hiyo ya Huduma za Bunge. Tuna matumaini kwamba kuwepo kwao kwenye Tume hiyo kutaiwezesha Tume kutoa uongozi utakaoliimarisha Bunge letu ili liweze kutekeleza majukumu yake kama inavyotarajiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, najisikia faraja na heshima kubwa kumpongeza Dakta Getrude Ibengwe Mongella, Mbunge wa Ukerewe kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano kama Rais wa Bunge la Afrika. Wote mtakubaliana nami kwamba katika kipindi hicho, Mheshimiwa Mongella amefanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa na hivyo kuweka historia ya nchi yetu katika kumbukumbu ambazo hazitafutika katika Historia ya Bunge la Afrika. Naungana nanyi nyote kumpongeza tena kwa heshima kubwa aliyoipatia nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge, Miswada, katika Mkutano huu wa Kumi na Sita, pamoja na kujadili Bajeti ya Serikali, Waheshimiwa Wabunge waliweza kujadili Miswada ifuatayo:

i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa Mwaka 2009 [*The Executive Agencies (Amendment) Bill, 2009*];

ii) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2009 [*The Finance Bill, 2009*];

iii) Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2009 [*The Appropriation Bill, 2009*];

iv) Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo wa Mwaka 2009 [*The Constituencies Development Catalyst Fund Bill, 2009*]; na

v) Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2009*].

Aidha, Miswada ifuatayo ilisomwa kwa mara ya kwanza :

i) Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 [*The National Security Council Bill, 2009*];

ii) Muswada wa Sheria ya Mazao ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko wa Mwaka 2009 [*The Cereal and Other Produce Bill, 2009*];

iii) Muswada wa Sheria ya kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali za Mazao wa Mwaka 2009 [*The Crops Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2009*];

iv) Muswada wa Sheria Mpya ya Korosho wa Mwaka 2009 [*The Cashewnut Industry Bill, 2009*];

v) Muswada wa Sheria ya Mtoto wa Mwaka 2009 [*The Law of the Child Bill, 2009*].

Mheshimiwa Spika, Kauli za Serikali, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu lilipokea Kauli Saba za Serikali zilizotoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali kutoka Serikalini. Kauli hizo ni pamoja na:

i) Kauli ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafiri wa Mazingira Vijijini;

ii) Kauli ya Waziri wa Miundombinu kuhusu Upangaji Barabara katika Hadhi Stahikili;

iii) Kauli ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu Mafua Makali ya Nguruwe;

iv) Kauli ya Waziri wa Nishati na Madini kuhusu Ubinafsishwaji wa Kampuni ya Mgodi wa Makaa ya Mawe - *Kiwira Coal Mines Limited;*

v) Kauli ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuhusu Uanzishaji wa Benki ya Wanawake Tanzania;

vi) Kauli ya Waziri wa Fedha na Uchumi kuhusu Majadiliano ya Mkataba wa Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Canada; na

vii) Kauli ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu Magunia ya Katani kwa ajili ya Kuhifadhia Mazao (*Mandatory Use of Sisal Bags*).

Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri waliotoa Kauli hizo za Serikali na kwa ufafanuzi mzuri.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia lilipokea Taarifa ya Utekelezaji kupitia Kamati mbalimbali za Bunge hili ambazo zilikuwa ni Kamati ambazo zimejadili na hatimaye kuwasilisha hapa taarifa zifuatazo:-

(a) Uendeshaji Usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania uliofanywa na Kampuni ya *RITES* ya India;

(b) Utendaji wa Kazi usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania International Container Terminal Services* (*TICTS*);

(c) Uuzwaji wa Nyumba za Serikali;

(d) Maazimio ya Bunge kuhusu Mchakato wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura Ulioipa Ushindi *Richmond Development Company LLC ya Houston, Texas* – Marekani Mwaka 2006; na

(e) Azimio la Bunge kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji na bei zake ambavyo Muda wake Kisheria Unaishia mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa Mbalimbali, Bunge lako Tukufu lilipokea Maamuzi ya Spika kuhusu hoja mbalimbali kama ifuatavyo:-

i) Hoja ya Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega ya kutaka iunde Kamati Teule ya Kuchunguza Wizara ya Miundombinu kuhusu kuingia Mikataba ya Ujenzi wa Barabara ambazo fedha zake zilikuwa hazijapitishwa na Bunge;

ii) Malalamiko ya Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba na Mheshimiwa Salum Saleh Londa, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni dhidi ya Kauli ya Mheshimiwa Halima James Mdee, aliyoitoa Bungeni tarehe 7 Agosti, 2008;

iii) Suala la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, lililojitokeza tarehe 12 Juni, 2009; na

iv) Ufafanuzi kuhusu madai ya kutumia Lugha ya kuudhi Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa maamuzi na ufafanuzi alioutoa ambao unaonyesha dhahiri kuwa Bunge hili linaongozwa kwa Kanuni na taratibu zinazolinda haki ya kila Mbunge katika kuchangia na kutoa maoni yake.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupokea Taarifa zilizowasilishwa na kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kujadili na hatimaye kupitisha Azimio pamoja na Miswada yote iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu katika kipindi cha Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maswali. Katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi ya kuuliza maswali 324 ya msingi pamoja na mengine mengi ya nyongeza. Aidha, katika kipindi cha kila Alhamisi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu, jumla ya maswali 60 yaliulizwa na 31 ya nyongeza. Nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa Maswali yao mazuri ya Papo kwa Papo na yale ya kawaida ambayo yameisaidia Serikali kutoa ufafanuzi wa Shughuli za Maendeleo kwa ajili ya Taifa letu. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri ambao walijibu kwa ufasaha maswali yote yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Nami naahidi kwamba Serikali itaendelea kujitahidi kujiandaa vizuri ili kuweza kutoa majibu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu bajeti ya Serikali na msukosuko wa uchumi na. bajeti ya Mwaka 2009/2010. Mkutano huu ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kuwasilisha, kujadili na hatimaye kupitisha Bajeti ya Serikali pamoja na Makadirio ya Fedha kwa Wizara, Mikoa na Taasisi mbalimbali kwa mwaka 2009/2010. Bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010 tuliyoipitisha ni ya jumla ya Shilingi Trilioni 9.5.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kwamba vipaumbele vyetu ni Elimu, Miundombinu, Afya, Kilimo, Maji na Nishati na Madini. Changamoto tuliyonayo ni kupanua wigo wa ukusanyaji mapato, kudhibiti matumizi na kutumia fedha hizi kwa shughuli zilizopangwa. Tayari Serikali imeanza kudhibiti matumizi ambayo siyo ya lazima, kwa mfano, Semina, Warsha, Makongamano, Mikutano, ununuzi wa magari, samani na baadhi ya posho. Maeneo yote ambayo tumeanza kuyasimamia tutaendelea kuyasisitiza.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii, kutoa wito kwa Watendaji Wakuu wa Wizara, Wakala na Idara zinazojitegemea, Mashirika na Taasisi za Umma, Mikoa na Halmashauri zote kuhakikisha tunasimamia vizuri ukusanyaji wa Mapato na kuwepo kwa usimamizi makini wa utekelezaji wa mipango ya Serikali na udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali. Hatua hii itawezesha kupiga hatua katika kufikia malengo mengi tuliyojiwekea. Aidha, nahimiza utaratibu wa kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu mapato na matumizi ya fedha za Serikali uzingatiwe katika ngazi zote. Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina wajibu wa kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu mapato na matumizi ya Serikali pamoja na michango ya wananchi. Uzoefu unaonyesha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zina tatizo la kukaa na fedha kwa muda mrefu kabla ya kuzitumia kwa matumizi yaliyopangwa. Hali hii haikubaliki kwa sababu inachelewesha kufikisha huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, naagiza taarifa za fedha zilizopo katika Akaunti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zitolewe kwenye kila Kikao cha Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msukosuko wa uchumi. Pamoja na kutenga fedha hizo, katika kipindi hiki tunapoelekea kwenye utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali tuliyoipitisha hapa, hatuna budi kufahamu kuwa dunia bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya msukosuko wa Fedha na Uchumi ambao haujatokea karibu miaka 60 iliyopita. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake aliyoitoa tarehe 10 Juni 2009, hapa

Dodoma, wakati alipozungumza na wananchi na Waheshimiwa Wabunge, alielezea kwa kina suala hili. Vilevile, alieleza kuwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zitaathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na msukosuko huo wa kifedha na kiuchumi, hasa kuanzia mwaka huu wa 2009. Mheshimiwa Rais pia alielezea kuhusu Mpango wa Serikali wa kuunusuru Uchumi wa Tanzania na athari za msukosuko wa fedha na uchumi duniani, ambao umeanza kutekelezwa kuanzia mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, msukosuko huo wa kiuchumi duniani, ingawa unasemekana ni wa mpito, ni dhahiri kuwa tusipojihadhari mapema, utaathiri zaidi uchumi wetu na hasa katika maeneo ambayo yapo nje ya uwezo wetu. Maeneo hayo ni pamoja na Sekta ya Utalii, kupungua kwa misaada na mikopo kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo, maeneo ya Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni na kushuka kwa bei ya bidhaa mbalimbali katika Soko la Dunia. Tayari Serikali imeanza kuchukua hatua za kibajeti kukabiliana na tatizo hili ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 20 zimeshatolewa kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili kusaidia kufidia bei ya zao la pamba. Hatua zingine zinaendelea kufuatiliwa ili kukabiliana na msukosuko wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa athari hizo ni pana, natoa wito kwa Wizara, Idara na Taasisi zote za Umma, Mikoa na Halmashauri kuzingatia yafuatayo:-

i) Kuhakikisha kuwa wanaandaa Mipango Kazi inayozingatia katika kukusanya Mapato na kubana Matumizi ya Serikali ili hata makusanyo yetu yakipungua kutokana na athari hizo, Serikali iweze kuendelea kutoa huduma zote muhimu kwa Wananchi;

ii) Mamlaka ya Mapato (*TRA*) wahakikishe wanaimarisha usimamizi katika makusanyo yote ya Kodi za Serikali na hasa kudhibiti wakwepa kodi. Aidha, wananchi wote washiriki katika kukataa kukwepa kodi ili kuisaidia *TRA* kukusanya mapato zaidi;

iii) Umakini zaidi unahitajika katika matumizi ya rasilimali tulizonazo. Matumizi ya fedha za Serikali yasiyo ya lazima katika kila ngazi yadhibitiwe. Semina, Warsha na Makongamano zitaendelea kusitishwa pamoja na Ununuzi wa Magari ya Kifahari. Tutadhibiti pia baadhi ya posho zisizo za lazima;

iv) Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu fedha zilizotengwa kwenye miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kulingana na kazi zilizopangwa na kuhakikisha kuwa zinaleta matokeo dhahiri kwa walengwa yaani *value for money*;

v) Kamati zilizoundwa katika kila Wizara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri zote kwa ajili ya kuratibu, kusimamia na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali zifanye kazi zake kama inavyopaswa na kuwasilisha taarifa zao kama maagizo yanavyowataka. Aidha, Halmashauri zinasisitizwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato yake ili kujijengea uwezo wa kujitegemea; na

vi) Kuongeza kasi ya kuondoa vikwazo vya Uwekezaji na Ukuaji wa Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, napenda kusisitiza kuwa Viongozi na Watendaji katika kila ngazi wanatakiwa kubuni mbinu mpya za kuchochea ukuaji wa uchumi ili athari za msukosuko wa kiuchumi zisiturudishe nyuma katika malengo tuliyojiwekea. Wakati huu wa msukosuko wa uchumi sio wakati muafaka wa kutekeleza majukumu yetu kwa utaratibu wa mazoea au lugha ya Kiingereza *business as usual*, bali ni wakati wa kubadilika na kuenda na kauli ya *business unusual*. Jambo kubwa linalohitajika hapa ni kwa wananchi kuunga mkono jitihada hizi za Serikali na kudhamiria kufanya kazi kwa bidii na maarifa kwa kila aliye na uwezo.

Aidha, kimkakati tuchukue hatua za ziada kuongeza uwekezaji kwa kuweka mazingira ya kuhimili ushindani zaidi. Kwa mfano, sio busara kwa wakati huu wa msukosuko wa uchumi kwa Viongozi kutumia lugha za kuwaogopesha Wawekezaji. Wote tumekubaliana kwamba, Sekta Binafsi ndiyo Injini ya Ukuaji wa Uchumi. Tutumie nafasi hiyo kuwavutia Wawekezaji kwa kuhakikisha Viongozi wa Serikali na Waheshimiwa Wabunge wote tunaongea lugha moja inayovutia Wawekezaji. Tunapoongea tusiwaogopeshe kuwekeza na kuwatafutia njia ya kutokea. Badala yake tuwape moyo wa kupenda nchi yetu na kuiona ni nchi nzuri ya kuwekeza mitaji yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi makini ya fedha. Pamoja na kuhimiza Uwekezaji, ni lazima tuchukue hatua za kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima. Katika mazingira tuliyonayo, Serikali na Vyombo vyake vyote, wote hatuna budi kuwa makini katika matumizi katika maeneo yote. Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zisimamie vizuri Watumishi wa maeneo yao ili watumie kikamilifu muda wa kawaida wa kazi kutekeleza majukumu yao. Watumishi wote wa maeneo ya kazi, kila mmoja afanye kazi kwa bidii zaidi na kutumia muda wa kazi kwa ufanisi badala ya kutaka kulipwa posho kila kazi anazozifanya. Kila mmoja ajitahidi kuwa mwadilifu ili rasilimali kidogo iliyopo iweze kutumika ipasavyo.

Nayasisitiza haya kwa sababu zipo taarifa zinazoonyesha kuwa hali sio shwari kwa matumizi ya fedha za Serikali. Mazoezi yaliyoendeshwa hivi karibuni kwa baadhi ya Halmashauri, baadhi ya Watumishi wanatumia fedha vibaya. Kazi ambazo zingeweza kutekelezwa kwa utaratibu wa kawaida wa kiofisi, sasa hazifanywi hadi posho itolewe. Haya hayawezi kuvumilika.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali ilituma Timu ya Wataalam ili kuhakiki madai ya Walimu. Matokeo ya uhakiki huo kwa kutumia mifano michache, umebainisha yafuatayo:-

(i) Wapo baadhi ya Watumishi ambao wanalipwa Mishahara miwili;

(ii) Yapo malipo yanayofanyika ambayo ni hewa, Watumishi hawapo;

iii) Zipo taarifa pia kwamba, hata wale tuliowatuma kwenda kuhakiki, nao wenyewe wameamua kujinufaisha. Baadhi ya Wakuu wa Shule wamebainisha kwamba, Timu iliyotumwa imewaomba waongeze fedha zinazodaiwa kwa makubaliano maalum. Kwa mfano, madai yaliyokuwa Shilingi milioni 40, wanataka ziandikwe Shilingi milioni 100. Hali hii kwanza ni aibu kwa watumishi wa Umma lakini ni kweli kabisa kwamba imejitokeza katika madai ya Wazabuni mbalimbali, madai ya Walimu na madai mengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kuvumilia mambo haya. Kutokana na hili, tumedhamiria kuchukua hatua zifuatazo:-

i) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha na Uchumi zitaandaa utaratibu ambao utawezesha uhakiki wa malipo ya mishahara kwa watumishi na ikibidi kutenga mwezi mmoja wa kulipa watumishi dirishani ili kubaini watumishi hewa;

ii) Fedha za malipo kwa ajili ya madai ya madeni ya Walimu zitapelekwa Mikoani na malipo yasimamiwe na Mikoa yenyewe kwa kulipa mtumishi mmoja mmoja badala ya watumishi kutoka Makao Makuu ya Wizara eti kwenda kuhakiki malipo hayo;

iii) Watumishi wote watakaobainika kulipwa mishahara miwili au kuchukua fedha wasizostahili, wote inaagizwa wafikishwe mbele ya vyombo vya sheria bila kuchelewa.

Ili kutekeleza haya, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali afanye ukaguzi wa kina hasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuona uhalali wa malipo yanayofanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kilimo Kwanza. Wakati wa kujadili Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2009/2010, pamoja na mambo mengine, nilizungumzia kwa kina dhana ya “Kilimo Kwanza”. Vilevile, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi ya kujadili kwa kina dhana hii wakati wa kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu, Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, Hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali katika hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kaulimbiu hii imetokana na Mkutano uliofanyika tarehe 2 na 3 Juni, 2009, Jijini Dar es Salaam chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Katika Mkutano huo tulikubaliana na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi kusukuma kwa kasi utekelezaji wa Programu ya *ASDP* ili kuleta Mapinduzi ya Kijani katika nchi yetu ambayo yatafanya kilimo kiwe cha kisasa, chenye Tija na kukifanya kiwe cha kibiashara. Tulikubaliana nia ya Serikali katika kutoa kipaumbele kwenye uendelezaji wa kusindika mazao ya kilimo na mifugo kwa kuhusisha Sekta Binafsi.

Vilevile, tumekubaliana kwamba, dhana ya “Kilimo Kwanza” iwe ni uwekezaji zaidi, siyo tu kupitia Bajeti ya Serikali, bali pia kupitia Uwekezaji wa Sekta Binafsi kwenye mashamba makubwa ya kilimo cha kibiashara. Tumekubaliana kwamba, Mapinduzi ya Kijani yanawezekana kwa kutumia maarifa na teknolojia za kisasa. Kwa maana hiyo, tunahitaji kujipanga vizuri kama Serikali na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutekeleza dhana hii. Lengo kubwa ni kuwawezesha wananchi wengi zaidi ikiwemo Sekta Binafsi kushiriki katika uzalishaji wa Sekta ya Kilimo. Ni dhahiri kuwa sekta mbalimbali kama vile Sekta za Kilimo, Miundombinu, Maji, Umeme, Usafirishaji na Mawasiliano zikishirikiana vizuri na wadau wengine hususan, Mabenki zinaweza kuchangia kasi ya kufanikisha azma hii.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumejiwekea vipaumbele mbalimbali katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010. Kwa mfano, Sekta ya Elimu imepewa kipaumbele kwa sababu bado tuna kazi kubwa ya kufanya kulingana na ukubwa wake na malengo mengi ambayo tulikwishaanza kuyatekeleza. Watoto wetu wengi wanatakiwa kuanza shule, wengi wanatakiwa kujiunga na Elimu ya Sekondari na tunatakiwa kujiandaa ili wapate nafasi ya Elimu ya Juu. Kwa maana hiyo, tunahitaji kuimarisha Miundombinu muhimu katika Elimu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, Maabara na kuwawezesha wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa njia ya mikopo. Vile vile, tunayo madeni mbalimbali yakiwemo, madeni ya Walimu, Wazabuni na Stahili za Wahadhiri katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Hata hivyo, ni vema ieleweke kuwa kwa kuimarisha elimu nchini, ni dhahiri matokeo yake yana faida nyingi zitakazopatikana kwenye kilimo. Tutapata wakulima bora, Maofisa Ugani bora na wafugaji bora na tutapata wavuvi bora.

Sekta ya Miundombinu nayo ina maeneo muhimu ambayo kwa ukubwa wake na aina ya shughuli zinazofanyika inaifanya sekta hii kuchukua asilimia kubwa ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka huu. Wote tumeshuhudia mjadala ndani ya Bunge hili, tena wenye hisia kali kuhusu ujenzi wa barabara katika maeneo yetu na hoja kwamba fedha zilizotengwa hazitoshelezi. Tumekubaliana kwamba, tunahitaji kutafuta fedha zaidi takriban Shilingi bilioni 45 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dodoma-Babati. Lakini vilevile zipo juhudi nyingine ambazo tunaendelea kuzifanya kupata mhisani ambaye anaweza kusaidia kujenga barabara hiyo moja kwa moja. Kwa maana hiyo, tunahitaji zaidi ya asilimia 11.5 ya bajeti iliyoelekezwa kwenye miundombinu.

Vilevile, Sekta ya Afya nayo pia tumejiridhisha kwamba ni sekta muhimu na shughuli zake kwa mwaka huu zinahitaji fedha sawa na Asilimia 10.1 ya Bajeti yote kwa shughuli zitakazofanyika mwaka 2009/2010. Lakini Sekta ya Miundombinu na Afya zote zinaimarisha na kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa sababu bila barabara nzuri usafirishaji wa mazao ya kilimo kwenda sehemu mbalimbali za nchini na nje ya nchi hautawezekana na bila kuwa na wananchi wenye afya nzuri nayo vilevile mambo mengine hayatafanyika na Taifa litakosa wakulima na wafugaji. Aidha, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko nayo ina mchango mkubwa sana katika kuendeleza Sekta ya Kilimo. Kwa mfano:-

i) Kuongeza upatikanaji na usambazaji wa Zana za Kilimo na pembejeo, hususan mbolea na madawa;

(ii) Kuendeleza usindikaji ili kuongeza thamani ya Mazao ya Kilimo, kupunguza upotevu baada ya kuvuna na kuongeza muda wa kuhifadhia mazao kabla ya kuuza kwa watu wengine (*shelf life*);

(iii) Kuendeleza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwenye Mazao ya Kilimo kama njia ya kukabiliana na mabadiliko ya bei za mazao;

(iv) Kuendeleza Kilimo cha Mkataba, hususan mbegu za mafuta;

(v) Kuimarisha upatikanaji wa Taarifa za Masoko ya Mazao na kuwaunganisha wakulima na masoko maalum; na

(vi) Kuendeleza miundombinu ya masoko ya mazao.

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo hasa msingi wa dhana hii ya “Kilimo Kwanza”. Kwa Lugha nyingine kila sekta ni lazima itekeleze majukumu kwa kuangalia namna jukumu hilo linavyosaidia kuendeleza Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhusiano wa Kilimo Kwanza na *ASDP*. Kama nilivyokwisha eleza hapo juu, sekta nyingine zote za Elimu, Miundombinu na Afya, lengo lake ni kusaidia kusukuma Kilimo. Ingawa ni kweli kuwa fedha zinaonekana kwenye Vitabu, kilimo kimetengewa asilimia 7.0, hali halisi inaonyesha kuwa kiwango kimefikia asilimia 11.24. Zipo fedha nyingine zilizopangwa na Serikali kupitia mpango wa kunusuru uchumi kwa mfano, kutoa Dhamana ya Serikali kufidia Vyama vya Ushirika vilivyokopeshwa, Makampuni yaliyopata hasara wakati wa kununua na kuuza Mazao ya Kilimo, Ruzuku ya Bei ya Pamba, Mkopo wa Matrekta kutoka India kwa ajili ya ununuzi wa matrekta. Kwa maana ya msisitizo wa nafasi ya kilimo, bajeti ya mwaka huu imetoa msukumo mkubwa kwa “Kilimo Kwanza”. Serikali itaendelea kuongeza na kuzionyesha fedha hizo kwenye Vitabu.

Mheshimiwa Spika, zipo hisia kwamba Kaulimbiu hii ya “Kilimo Kwanza” ni mbadala wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*), hisia ambazo zinaondoa ukweli wa kile tulichodhamiria na kukubaliana katika Mkutano wetu wa tarehe 2 hadi 3 Juni, 2009 kuhusu Mapinduzi ya Kijani katika Nchi yetu. Ni kweli kwamba, katika Mkutano ule tuliamua kukipa kipaumbele kilimo kwa mapana yake na kwamba mambo mengine yote yanaweza kusubiri, isipokuwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kusisitiza kwamba Kaulimbiu ya “Kilimo Kwanza” siyo Mradi au Programu mbadala wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*). *ASDP* ni Mpango wa Kutekeleza Malengo ya Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Mpango ambao una lengo la kukiwezesha kilimo kiwe cha kisasa, cha kibiashara, kilicho na tija na chenye kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali na kuchochea maendeleo ya sekta nyingine. Tunachofanya sasa ni kutumia

Kaulimbiu hii kuhamasisha kusukuma maendeleo ya kilimo nchini kwa vitendo ili yafikiwe kwa kasi zaidi. Programu ya *ASDP* itaendelea kuwa ndiyo Programu ya Kitaifa ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo na kwamba ndiyo Programu ya kuzisaidia sekta zingine kufanya sehemu zake ipasavyo.

Kwa tafsiri nyingine "Kilimo Kwanza" itasukuma kwa kasi zaidi utekelezaji wa Programu wa *ASDP*. Kila sekta ni lazima ielekeze mipango yake ifikie malengo ya "Kilimo Kwanza" kwa kuweka Vipaumbele vyake katika kuongeza tija katika Sekta ya Kilimo. Kutokana na umuhimu huu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameamua kuzindua Kaulimbiu hiyo siku tarehe 3 Agosti, 2009 wakati wa Wiki ya Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima – NANE NANE, Mjini Dodoma. Waheshimiwa Wabunge wote wanaalikwa katika shughuli hiyo muhimu kwa Taifa letu na hasa ile Kamati ambayo inahusika na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majumuisho ya Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nilieleza kwa kina uamuzi wa Serikali kuhusu dhana hii ya "Kilimo Kwanza" na nikatoa Nguzo Kumi na Amri kumi za "Kilimo Kwanza". Aidha, mafunzo ya Mawakala wa Pembejeo kwa maeneo mapya yameanza. Mafunzo hayo yatasaidia Mawakala kuanza kujiandaa kupeleka Vocha mapema Vijijini. Aidha, yapo maelekezo ya utekelezaji wa Kaulimbiu hii yakiainisha Nguzo Kumi na Amri Kumi za Kilimo ambayo yamekwishapelekwa kwa Wakuu wa Mikoa wote kuelezea jinsi ya kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Kaulimbiu hii.

Kwa upande mwingine tayari tumeanza kujiandaa kikamilifu kutekeleza Kaulimbiu hii. Ili kuwezesha mbolea kuwafikia wakulima kwa wakati, uchapishaji wa Vocha umekwishaanza na Vocha zilizochapwa zinatarajiwa kuanza kusambazwa kuanzia katikati ya Agosti, 2009. Usambazaji wa Vocha utahusu maeneo yafuatayo:-

i) Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Morogoro, Kigoma, Kilimanjaro, Arusha na Manyara (Wilaya zote);

ii) Mikoa ya Shinyanga (Wilaya za Kahama na Bukombe), Tabora (Wilaya za Urambo na Sikonge) na Mara (Wilaya za Serengeti na Tarime);

iii) Maeneo ya Umwagiliaji, Mikoa ya Singida (Wilaya za Singida na Manyoni), Dodoma (Wilaya za Bahi na Mpwapwa), Tanga (Wilaya za Lushoto, Korogwe na Muheza), Pwani (Wilaya ya Bagamoyo), Lindi (Wilaya ya Lindi), Mtwara (Wilaya ya Mtwara), Tabora (Wilaya ya Igunga) na Mara (Wilaya ya Bunda) kwenye maeneo yale ya umwagiliaji.

Ili kuhakikisha kwamba maeneo ambayo mvua zinaanza mapema Vocha zinawahi kufika, tayari Mikoa inayohusika imetakiwa kuainisha maeneo ya namna hiyo. Mathalan, Wilaya ya Rungwe wanaanza kupanda mwezi Septemba wakati Wilaya nyingine wanaanza Novemba. Lengo ni kuhakikisha kwamba vipaumbele vinawekwa kwanza kwenye Wilaya ambazo msimu wake unaanza mapema.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Usambazaji wa Pembejeo kwa Wakulima, tayari Serikali imeweka utaratibu mzuri na wa gharama nafuu wa kufikisha pembejeo kwa Wakulima. Tayari Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imekwishakutana na Makampuni ya Mbolea na Mbegu na kuyajulisha mahitaji ya Pembejeo kwa kila Mkoa na maeneo yatakayopata ruzuku ya pembejeo na kiasi ambacho kitapelekwa kwa kila aina ya pembejeo.

Wito wangu kwa Viongozi na Watendaji katika ngazi zote ni kuwaomba washiriki katika kuelimisha na kuhamasisha wakulima kuzingatia utekelezaji wa Kaulimbiu hii na Kanuni Bora za Kilimo ili tuweze kufikia azma yetu ya Mapinduzi ya Kijani. Kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunayo nafasi ya pekee katika maeneo tunayotoka ya kuchochea na kuleta Mapinduzi ya Kijani katika maeneo yetu. Hapa ndani ya Bunge tupo jumla ya Waheshimiwa Wabunge 323 Kikatiba ambao kwa pamoja tukiinuka na kwenda kwenye Majimbo yetu kuhimiza kilimo, matokeo yake nina hakika yatakuwa makubwa sana. Nawaomba tushirikiane na kuwa mfano kwa wananchi kwenye kuhimiza maendeleo ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa chakula. Kulingana na tathmini ya hali ya chakula iliyofanyika Mei na Juni, 2009; hali ya chakula msimu wa 2009/2010, siyo nzuri pamoja na matarajio ya mavuno mazuri katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Hali hii inatokana na Mikoa ya Mashariki na Kaskazini kukosa kabisa Mvua za Vuli na Masika. Mikoa 17 na Wilaya 61 zitakuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tabora, Tanga, Ruvuma, Morogoro na Pwani, mtashtuka nikitaja Morogoro lakini ni kweli kwamba yapo maeneo ambayo hayakupata mvua. Mikoa mingine ni Dodoma, Iringa, Shinyanga, Singida, Lindi, Mbeya, Mwanza, Mara na Mtwara.

Tathmini inaonyesha kuwa, uzalishaji wa nafaka unakadiriwa kufikia tani milioni 5.26, lakini mahitaji ni tani milioni 6.58 na hivyo kuwa na upungufu wa tani milioni 1.3. Huu ni upungufu mkubwa sana ambao haujawahi kutokea katika miaka ya karibuni. Aidha, bei ya mahindi katika soko la dunia bado iko juu sana zaidi ya Dola za Kimarekani 350 kwa tani ambayo ni takriban Sh. 500,000/= kwa tani.

Kwa kuzingatia hali hii, Serikali imeamua ifuatavyo:-

(i) Mpango wa kuhamisha Akiba (*Stock*) za mahindi kutoka Mikoa yenye ziada kupeleka maeneo yenye upungufu uendelee kwa kasi zaidi;

(ii) Fedha za kusafirisha na kununua mahindi pamoja na madeni ya chakula cha njaa, zitolewe zote mwezi wa Agosti, 2009, ili Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*SGR*) iwe na uwezo mkubwa wa kununua mahindi wakati wa mavuno. Fedha zinazohitajika ni Shilingi bilioni 19.6 zilizotengwa kununua chakula; na Shilingi bilioni 9.9 za madeni ya chakula cha njaa; na

(iii) Fedha za kutunisha Mfuko wa Maafa, Shilingi bilioni 10.0 zitolewe mwezi Agosti, 2009, Waziri wa Fedha ameshaelekezwa ni matumaini yangu kwamba jambo hili

litafanyika bila kuchelewa ili tusikose fursa hiyo na ili kazi ya kusambaza chakula cha njaa isikwame.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu hali hii ya upungufu wa chakula ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha za kununulia chakula chote kwa ajili ya Wakala wa Taifa wa Kuhifadhi Chakula zinapatikana katika Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2009/2010. Kinachohitajika sasa ni utekelezaji wa Mipango na hatua ambazo zinapendekezwa na Serikali kuchukuliwa ili kupunguza uhaba wa chakula. Wito wangu kwa wananchi wote ni kuzingatia maelekezo ya Serikali katika kutunza na kuhifadhi chakula. Katika maeneo yenye chakula cha kutosha, wananchi watunze chakula cha kuwatosha kwa msimu wote unaofuata. Aidha, kwa maeneo yenye Uhaba wa Chakula, wananchi wahakikishe kwamba chakula wanachopelekewa kama msaada kinatumika ipasavyo badala ya kukiuza tena kwa njia ya magendo. Wakuu wa Mikoa na Wilaya wasimamie zoezi hili na kuhakikisha chakula cha msaada hakiuzwi tena nje ya nchi. Pia wananchi wasichague chakula. Chakula cha mazao yasiyo ya nafaka kinapatikana kwa wingi na hatua zitachukuliwa kuongeza matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, nimeomba niliseme hili la kuhakikisha kwa kweli chakula hakitoroshwi kupelekwa nje kwa sababu mazingira tuliyonayo hivi sasa tusipokubali hali halisi tutaaibika kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi midogo ya Umwagiliaji. Njia moja ya kupambana na hali ya Ukame unaojitokeza mara kwa mara na kuleta tishio la njaa mbaya hapa nchini ni kuanzisha miradi midogo midogo ya umwagiliaji. Miradi hii inaweza kuwa sehemu ya mikakati ya Halmashauri katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*). Serikali sasa itaweka nguvu zaidi katika kupanua Kilimo cha Umwagiliaji. Kila Kiongozi kwa kushirikiana na Watendaji wa Wilaya wajikite zaidi kuwahamasisha wananchi kuibua Miradi hiyo Midogo Midogo ya Umwagiliaji ili iweze kuingizwa katika Programu ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*). Huu ni wajibu wa Viongozi na Watendaji wa kila Mkoa na Wilaya, tusiiachie Wizara peke yake.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo ina nafasi kubwa katika kujenga uchumi imara wa Taifa, hasa katika kuongeza kipato kwa Watanzania wanaotegemea mifugo na kutoa fursa za ajira pamoja na kuhifadhi rasilimali za Taifa. Kwa mfano, Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2008 imechangia asilimia 4.6 ya Pato la Taifa.

Upo ukweli kwamba, Sekta ya Kilimo ina uhusiano wa karibu sana na Sekta ya Mifugo. Katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*), vipengele vinavyohusu Sekta ya Mifugo ni kama vifuatavyo:-

(i) Huduma za Utafiti, Mafunzo na Ugani ikiwemo kuanzisha na kuendeleza mifugo yenye ukosefu wa tija, pamoja na kuandaa maelekezo ya uzalishaji bora wa ng’ombe wa nyama na maziwa; kuandaa majaribio na maelekezo sahihi ya chanjo kwa lengo la kudhibiti magonjwa ya mifugo; kuimarisha Vituo vya Kanda vya Utafiti wa

Mifugo na Idara ya Utafiti na Mafunzo na Kuboresha huduma za ugani kwa Wafugaji pamoja na kuhakiki watoa huduma za mifugo;

(ii) Kuboresha Masoko na kuendeleza Sekta Binafsi ikiwa ni pamoja na kuimarisha mashamba ya kuzalisha mifugo kwa kuyapatia zana na pembejeo; mbegu bora za malisho ya mifugo na kuchimba na kukarabati malambo ili kuipatia mifugo maji katika maeneo kame nchini;

(iii) Uzuiaji wa Milipuko ya Magonjwa ya Mifugo kwa kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa ya milipuko; kuwaendeleza Kitaaluma Watumishi na kuimarisha ushirikiano wa watoa huduma za mifugo wa Sekta ya Umma na Binafsi na kushiriki katika Vyama vya Kitaaluma; na

(iv) Utaratibu, Ufuatiliaji na Tathmini kwa kuandaa mkakati wa kuendeleza mifugo na kutoa elimu kwa Wadau kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo; kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali na kuandaa Sheria mpya za Sekta ya Mifugo na kuwezesha jamii za wafugaji kuandaa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) imetoa mwongozo wa utekelezaji wa vipengele vilivyoainishwa. Tatizo kubwa tunaloliona ni utekelezaji, hususan katika ngazi za Halmashauri hasa katika uibuaji wa Miradi ya Mifugo kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*). Wafugaji wanapaswa kuelimishwa zaidi kuhusu miradi hiyo, hususan kuibua miradi ya uenezaji, uzalishaji wenye tija katika mazao ya mifugo, uboreshaji ngozi, udhibiti wa magonjwa ya mifugo na uendelezaji malisho ili mifugo isihamehame kutafuta maji na malisho wakati wa ukame.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwa sasa, Sekta ya Mifugo pamoja na kwamba imepewa nafasi kwenye Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*), ni eneo ambalo halijionyeshi wazi kuweza kuliangalia na kulipa msukumo kama ambavyo Kilimo kinavyojionyesha. Serikali imeiagiza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuandaa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo, ili nayo iweze kujidhihirisha kwa wadau namna inavyoweza kujiendeleza. Hivyo, mikakati yake ya kuendeleza Sekta itabainishwa. Wizara itakamilisha zoezi hili mapema ili kuendeleza Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli wa mahusiano hayo na kama ilivyo kwa Kilimo, Serikali inadhamiria kujenga mazingira mazuri yatakayotoa fursa za kuongeza kipato na ajira kwa Wafugaji Wadogo, kufuga kibiashara na kuongeza ajira. Ili kufikia azma hii, malengo makuu ya kisera yatatekelezwa kama ifuatavyo:-

i) Kuendeleza Sekta ya Mifugo itakayokuwa na mwelekeo wa kibiashara, yenye ufanisi na itakayohimili ushindani wa Kimataifa;

ii) Kuibua mifumo bora ya uzalishaji wa Mifugo na mazao yake ili kuongeza Mifugo yenye tija miongoni mwa Wafugaji; na

iii) Kuhifadhi rasilimali za Mifugo na kuhuisha Taasisi zitakazosimamia maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Julai, 2009, nilikutana na kuzungumza na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika Mikoa yenye wafugaji wengi ya Mwanza, Mara, Tabora, Shinyanga, Dodoma, Singida na Manyara. Katika Mkutano huo, Waheshimiwa Wabunge walishauri na kupendekeza kwa nguvu kuwa ili tuweze kuleta mageuzi ya kweli katika Sekta ya Mifugo, ni lazima tuanze kwanza kwa kuyaelewa matatizo yanayowakabili wafugaji hawa na kujua ni kwa nini hawabadiliki na kufuga kibiashara. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wamependekeza na kushauri kama ifuatavyo:-

i) Tuanze kwa kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi, utakaotenga maeneo ya wafugaji na matumizi mengine;

ii) Pamoja na kuwa Sekta ya Mifugo inatekeleza majukumu yake kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *–ASDP*, kuna haja sasa kuandaliwa kwa Mipango Maalum kwa ajili ya Sekta ya Mifugo peke yake na kutafutiwa bajeti ya kutekeleza mipango hiyo ili kuongeza kasi ya Mapinduzi katika Sekta hii;

iii) Kuwaelimisha wafugaji na wananchi kwa ujumla kuelewa kuwa mifugo ni sawa na mazao mengine ya biashara, tena mazao ambayo tayari yapo wala huhitaji kuyalima au kuyatafutia umwagiliaji hata kidogo. Hivyo, kuwepo na mpango maalum utakaowawezesha wafugaji kuvuna mazao na kuuza katika masoko ili kuboresha maisha yao. Tuache tabia ya kuhamisha mifugo kwenda maeneo mengine; na

iv) Kutokana na wingi wa mifugo, kuwepo na Mkakati Maalum wa Kupunguza Idadi ya Mifugo iliyopo, hasa kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa Victoria na Kanda ya Kati. Vile vile kuwepo na Mpango wa Kujenga Viwanda vya Kusindika Nyama na Maziwa ili kuongeza thamani ya mazao yatokayo na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walioshiriki katika kikao hicho nilichokiitisha siku chache zilizopita. Ni kutokana na mapendekezo haya mazuri ya Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaandaa Mkutano ambao utatuwezesha kukubaliana Programu na Mikakati ya kuleta Mapinduzi katika Sekta ya Mifugo. Vile vile tulikubaliana kuwa tufanye Mkutano kama ule wa Kilimo uliofanyika mwezi Oktoba, 2008. Mkutano huu wa mifugo utashirikisha Viongozi, Watendaji Wakuu na Wataalam kutoka Mikoa ya Manyara, Mara, Shinyanga, Mwanza, Arusha, Dodoma, Tabora na Singida. Aidha, Mikoa ya Rukwa, Morogoro, Kagera, Mbeya, Pwani na Lindi nayo itashirikishwa. Mkutano huo utashirikisha wadau wote kutoka Mikoa, Halmashauri na Wawakilishi wa Wafugaji. Mikoa inatakiwa sasa iwasilishe mapendekezo yao kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ambayo ndiyo itaratibu maandalizi ya Mkutano huu mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi. Kama ilivyo kwa Mifugo, Samaki ni zao lingine ambalo lipo na kinachohitajika ni uvunaji tu. Nchi yetu inayo maeneo mengi yenye maji na raslimali ya uvuvi. Maeneo hayo ni pamoja na Maziwa Makubwa na Madogo, Mito, Malambo lakini kubwa ni Bahari hii ya Hindi. Wingi wa raslimali zilizopo katika maeneo haya una manufaa makubwa kwa jamii na uchumi kwa nchi hii.

Sekta ya Uvuvi inaajiri zaidi ya watu milioni nne (4,000,000) hapa nchini na ina umuhimu mkubwa kwani huwapatia wananchi lishe bora, ajira, kipato kwa mtu mmoja mmoja, mapato ya Serikali na fedha za kigeni zinazotokana na mauzo ya mazao ya Uvuvi nje ya nchi. Hata hivyo, mchango wa sekta hii bado ni mdogo sana, sasa hivi ndiyo kwanza ni asilimia moja na pointi mbili (1.2%) tu ya Pato la Taifa. Hivyo, tuna changamoto kubwa ya kuboresha sekta hii ili itoe mchango unaostahili katika uchumi wa Wavuvi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo changamoto kubwa ninayoiona katika Sekta ya Uvuvi ni namna ya kukabiliana na uvuvi haramu kwa upande mmoja, unaojitokeza na ambao umesababisha madhara makubwa ya kijamii, kiuchumi na kimazingira. Hali hii inatokana na matumizi ya nyavu zenye matundu madogo, matumizi ya nyavu aina ya kokoro, matumizi ya sumu na baruti katika uvuvi. Athari za uvuvi haramu ni upungufu wa samaki kama kitoweo na kama malighafi katika viwanda vya uchakataji wa mazao ya uvuvi. Kwa sasa, viwanda hivi hufanya kazi chini ya uwezo wake wa kuzalisha kutokana na kupungua kwa samaki hasa katika Ziwa Victoria na hivyo kulazimika kupunguza idadi ya wafanyakazi na hata kulazimika kurekebisha taratibu za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa Kilimo na Mifugo, kuna umuhimu sasa wa kuingiza Sekta ya Uvuvi katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*). Maeneo ambayo ni muhimu kuangaliwa ni pamoja na Viwanda vya Kusindika Samaki, Masoko, Utafiti, Zana za Uvuvi, na Maafisa Ugani ili kuweza kuwaelimisha Wavuvi. Kama tunavyoendelea na uhamasishaji katika Sekta ya Kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji na tunavyotaka kufanya kwenye Sekta ya Mifugo, ni lazima tufanye hivyo hivyo kwa Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla upo umuhimu wa kuimarisha Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kutokana na ukweli kwamba, Watanzania wengi wanaishi Vijijini na tegemeo lao kubwa ni Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya maisha yao. Vile vile Kilimo, Mifugo na Uvuvi ndiyo chanzo cha malighafi ya Viwanda vyetu nchini na ni chanzo muhimu cha chakula cha Watanzania. Sekta hizi huzalisha mazao ambayo husindikwa na kuuzwa nchi za nje na kutuingizia fedha za kigeni. Hivyo, sekta hizi ni silaha muhimu sana katika kupambana na umasikini nchini. Serikali itaweka nguvu zaidi katika kuziendeleza sekta hizi tatu ili kuwaondolea wananchi umasikini. Matarajio yetu ni kwamba juhudi hizi zitaleta mabadiliko makubwa katika uzalishaji na uendelezaji wa sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Tatizo linalotoa changamoto kubwa kwa dunia nzima kwa sasa ni kasi ya mabadiliko ya tabia nchi. Katika hali ya kawaida, tatizo hili linaweza kuonekana dogo na

litakalomalizika hivi karibuni, lakini ukweli ni kwamba, sio la kawaida. Ni tatizo kubwa ambalo linahitaji kueleweka vizuri mpaka kwenye ngazi za kaya zetu.

Mheshimiwa Spika, suala hili la mabadiliko ya tabia nchi inabidi liangaliwe kwa umakini sana. Tunahitaji Elimu na Tabia Nchi ishuke katika ngazi za nchini ili wananchi waelewe vizuri chanzo chake, kwani itawasaidia kujiandaa na kufanya maamuzi sahihi ya shughuli zao za uzalishaji hasa kilimo kwa kulima mazao mbadala yanayoendana na hali ya hewa iliyopo na kwa wafugaji kubadilika na kupunguza mifugo.

Yapo maeneo mengine kwa mfano ukataji miti hovyo, uchomaji moto nyasi na misitu na kilimo kisichozingatia utaalam na kisicho endelevu, haya yanasababisha mabadiliko ya tabia nchi. Vile vile, wingi wa mifugo katika sehemu moja, uvuvi haramu na uzalishaji wa gesi mbalimbali kutoka viwandani vyote hivi vinachangia katika tatizo kubwa la mabadiliko ya tabia nchi na kuharibu Vyanzo vya Maji, Ardhi, Mazalia ya Viumbe hai na hivyo kuharibu Hewa ya *Ozon* kunakosababisha ongezeko la joto duniani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu athari za kemikali kwa mazingira na viumbe hai. Kemikali ni nyenzo muhimu katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali katika Viwanda na Migodi. Migodi hasa ya Dhahabu hutumia Kemikali za *Cyanide* na Zebaki (*Mercury*) katika uvunaji wa dhahabu katika mchanganyiko wa udongo na madini yake, kutokana na mchanganyiko wa hewa na unyevunyevu juu ya ardhi, madini huweza kutengeneza kemikali zenye madhara makubwa kwa binadamu na mazingira. Vilevile viwanda hutumia kemikali mbalimbali katika uzalishaji wa bidhaa. Majitaka yanayotokana na uzalishaji Viwandani na Migodini mara nyingi hubeba kemikali hizi na ni hatari iwapo yataachwa kuingia katika mazingira bila kusafishwa.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa wenye Viwanda na Migodi. Ili kuzuia ajali zinazotokana na Kemikali, upo utaratibu uliowekwa kisheria katika usafirishaji wa Kemikali zitokanazo na shughuli za migodi na uzalishaji wa viwandani. Wawekezaji kama vile wenye Viwanda au Migodi wana wajibu wa:-

i) Kusajili shughuli zao na kufuata maelekezo yanayotolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira;

ii) Kufanya Tathmini ya Athari ya Mazingira (TAM);

iii) Kufanya ufuatiliaji na uperembaji wa mradi na uhakiki; na

iv) Kuzingatia na kutekeleza Sheria ya Mazingira na Sheria nyingine zinazolenga katika kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa, pale ambapo utaratibu huu haifuatwi kunaweza kuleta madhara kwa watu na viumbe hai, naomba nitoe wito kwa wenye viwanda na mgodi kuzingatia taratibu hizi zote ili kuepusha madhara ya kemikali kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kufanyakazi kwa nguvu zote kuhakikisha tunalinda maisha ya binadamu, wanyama pamoja na viumbe hai vingine,

madhara ambayo yanasababishwa ama na uzembe, kutokujali au kupuuza uzingatiaji wa Sheria zile zinazolinda mazingira yetu, tutachukua hatua kali dhidi ya mgodi au kiwanda chochote kitakachodhihirika kwamba, kwa makusudi ama kwa uzembe kimeacha kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wajibu wa kutunza mazingira. Sheria ya Mazingira, Sura ya 191 ya Mwaka 2004, ilianzisha Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) na kulipa nguvu kusimamia na kuhifadhi mazingira.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, jukumu la Msingi la Baraza la Mazingira ni kusimamia masuala yote ya Mazingira Nchini na kuhakikisha kwamba, Mazingira yanatumiwa kwa njia endelevu. Aidha, Sura ya 191 Vifungu Na. 172 na 173 vya Sheria ya Mazingira vimeeleza wazi kwamba, kila raia wa Tanzania anao uhuru wa kujua taarifa za Mazingira ikiwemo mtiririsho kwenye vyanzo vya maji, hewa na uhifadhi wa taka hatarishi. Vile vile, Sheria inamtaka kila mwananchi kuwajibika na kutunza mazingira. Swali ninalojiuliza kila siku ni kwamba, kama Sheria tunazo, vyombo vya kusimamia mazingira tunavyo na wataalam wapo, sasa tatizo liko wapi? Kwa hiyo, nadhani hapa tatizo tulilonalo ni changamoto kwa Wataalam na jamii kwa ujumla kwamba, ni lazima sasa kila mmoja azijue sheria hizi, ajue taratibu zake na adhamirie kuzisimamia na kuzitekeleza kwa dhati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ulinzi na Usalama. Tarehe 30 Juni, 2009 nilipata nafasi ya kutembelea maeneo yaliyotokea mapigano katika Wilaya za Tarime na Rorya ambako jumla ya watu 31 waliuawa, nyumba 400 zilichomwa moto na watu 3000 walikosa makazi. Ziara hii ilinisaidia kuwapa pole waathirika, kuongea nao kujaribu kujua chanzo cha mapigano haya na hatua za kuchukua. Vile vile, katika ziara hiyo nilibaini kwamba, kimsingi hakuna uhasama kati ya Mluo na Mkurya. Inawezekana kwamba, vita vile ni kati ya raia wema na majambazi ambao wanakuja kufanya wizi wa mifugo. Ilibainika pia kwamba, maeneo yale hayana Ulinzi wa kutosha. Nashawishika kukubali kwamba, kama tukidhamiria tunaweza kulipatia ufumbuzi tatizo hili, kinachotakiwa ni kulishughulikia tatizo hili kisayansi na kitaalam zaidi na kushirikisha jamii yenyewe kwa kiasi kinachowezekana.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kwamba hatua ya kuanzia ni kubadilisha mfumo wa Ulinzi katika maeneo haya ya Tarime na Rorya na kuyapatia hadhi ya Mkoa wa Kipolisi, kazi ambayo tayari imekwishaanza kutekelezwa. Vile vile Serikali imefanya utaratibu wa kupeleka chakula cha msaada kwa familia zilizoathirika na kupoteza mali zao. Mipango mingine ya muda mrefu, kwa mfano, kuanzisha Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa katika maeneo haya inafanyiwa kazi. Wito wangu kwa wananchi wa Tarime na Rorya, ni kuongeza ushirikiano na Vyombo vya Dola, kudumisha dhana ya Ulinzi Shirikishi na kuimarisha Ulinzi wa Jadi ili kuwabaini mapema wanaosababisha wizi na kisha mapigano katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kama Waheshimiwa Wabunge mnavyofahamu mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi wa Viongozi wa Mamlaka

za Serikali za Mitaa katika ngazi ya Vitongoji, Vijiji na Mitaa. Uchaguzi huu utafanyika tarehe 25 Oktoba, 2009 kwa kuzingatia masharti ya Sheria za Serikali za Mitaa na Kanuni za Uchaguzi ambazo zimetungwa baada ya kushauriana na wadau mbalimbali, wakiwemo Viongozi wa Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu. Katika Uchaguzi huo wananchi watatakiwa kuwachagua Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji na Wajumbe wa Serikali za Vijiji na Kamati za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari ratiba ya uchaguzi huo, ikiwa ni pamoja na utaratibu utakaotumika imekwishatangazwa katika Vyombo vya Habari ili kutoa nafasi kwa wananchi kuelewa utaratibu huo na masharti muhimu ya kuzingatia wakati wa uchaguzi. Miongoni mwa masharti muhimu ya kuzingatia katika uchaguzi huo ni haya:-

i) Wapiga kura watatakiwa kujiandikisha katika Rejista Maalum ya Wapiga kura itakayoandaliwa siku Ishirini na Moja (21) kabla ya siku ya Uchaguzi;

ii) Uchaguzi utafanyika katika ngazi ya Kitongoji na Mitaa sehemu ya faragha na hakutakuwa na Mikutano ya Uchaguzi katika ngazi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji; na

iii) Wagombea wote wa nafasi mbalimbali za uchaguzi watatakiwa wawe Wanachama na wadhaminiwe na Chama cha Siasa chenye Usajili wa Kudumu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kutoa rai kwa wananchi wote wenye sifa stahiki kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kupitia Vyama vyao. Aidha, nawaomba kujiandikisha katika Daftari Maalum kwa ajili ya Uchaguzi huu na pia kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura, ili kutumia haki yao Kikatiba kuchagua Viongozi bora kwa maendeleo ya nchi yetu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tutumie kipindi hiki hadi siku ya uchaguzi kwa kuwahamasisha wananchi kushiriki kwa amani na utulivu katika uchaguzi huo ambao ni haki ya kila mmoja Kikatiba. Kwetu sisi sote tuliomo humu Bungeni, nina hakika tunajua umuhimu wa uchaguzi huu kwamba, ni kipimo muhimu sana katika uchaguzi wa mwaka 2010. Kwa hiyo, wote tushirikiane tutoe elimu ya kutosha ili kila mwananchi ashiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kabla ya kuhitimisha hoja yangu napenda nisisitize maeneo machache yafuatayo;

Kwanza: Tunayo changamoto ya kuongeza juhudi za kukusanya Mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi na kutumia vizuri pesa inayokusanywa. Tutumie bajeti ya mwaka huu iwe mfano wa kuigwa kwa kupanga na kutumia vizuri rasilimali tulizonazo;

Pili: Tunayo nafasi ya kutumia kilimo katika kubadili maisha ya Mtanzania. ‘Kilimo Kwanza’ ndiyo Kaulimbiu yetu ambayo ni kichocheo katika kusukuma yale yaliyomo katika Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo yaani *ASDP* kwa vitendo. Nasisitiza kwamba, Kaulimbiu ya ‘Kilimo Kwanza’ siyo mbadala wa *ASDP*. Tuitumie

Kaulimbiu hii kusukuma shughuli zilizoanishwa katika Mkakati huu wa kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa kasi zaidi;

Tatu: Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi zinategemeana kwa kiasi kikubwa sana. Watanzania wengi wanategemea matumizi ya mazao ya Sekta hizi kama chakula, lakini vilevile kama silaha ya kupambana na umaskini. Tushirikiane na Serikali kuziendeleza Sekta hizi ili kuondoa umasikini kwa wananchi wetu.

Nne: Suala la Mabadiliko ya Tabia Nchi linazungumzwa katika ngazi za juu Serikalini tu. Kuna haja sasa ya kulipa uzito mkubwa zaidi katika ngazi za chini kwa njia ya kutoa elimu zaidi ili wananchi walifahamu vizuri. Hatuhitaji Makongamano na Warsha za kitaalam kwa hili kwani mabadiliko ya hali ya hewa yanaonekana dhahiri katika maeneo mengi. Tushirikiane kuweka msisitizo kwa wananchi waelewe dhana nzima ya mabadiliko ya Tabia Nchi na athari zake na kwamba nao wanayo nafasi na wajibu kuzuia uharibifu wa mazingira.

Tano: Tunalo tatizo la Watumishi wasio waaminifu katika matumizi ya fedha na muda wa kazi. Watumishi wote hawana budi kuwa makini katika matumizi ya muda wa kazi wa kawaida katika kutekeleza majukumu yao. Kila Meneja ajitahidi kuwa Mwadilifu ili rasilimali kidogo iliyopo iweze kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Nikushukuru kwanza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kutuongoza vizuri kulingana na Kanuni zetu za Bunge. Vilevile, niwashukuru Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho; Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid, Mbunge wa Kwamtipura kwa kuongoza vizuri baadhi ya vikao vya Bunge wakati wa Mkutano huu.

Niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu ya dhati kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Niwashukuru Watumishi na Wataalam wote wa Serikali waliosaidia kujibu Maswali na Hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza hapa wakati wa Mkutano huu. Vile vile, nawashukuru Waandishi wa Vyombo vya Habari kwa kuwapatia Wananchi habari kuhusu Majadiliano yaliyokuwa yanaendelea hapa Bungeni.

Napenda kuwashukuru sana madereva wote ambao wamekuwa makini katika kazi ya kuwaendesha Viongozi wote, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Wataalam kutoka sehemu mbalimbali nchini na kuwawezesha kufika hapa Dodoma kuhudhuria Mkutano huu wa Kumi na Sita. Vilevile, nawashukuru Wananchi wa Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Dk. James Alex Msekela, kwa ukarimu wao kwa muda wote tuliokaa hapa. Navishukuru pia Vyombo vya Ulinzi na Usalama ambavyo vimehakikisha muda wote tumekaa kwa amani na utulivu mkubwa. Mwisho namshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa huduma nzuri zilizowezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwa Mkutano huu bila matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunahitimisha Mkutano huu leo, yako mambo mengi yaliyojitokeza wakati wa majadiliano ya taarifa mbalimbali za Wenyeviti. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, sisi tumeyapokea yote yaliyojitokeza katika mjadala wa leo na tunaahidi kwamba, tutayafanyia kazi kwa nguvu zetu zote na kuhakikisha kwamba, Bunge lijalo tunaweza kuwasilisha taarifa ambayo itawaridhisha Wabunge, lakini kubwa Watanzania kwa ujumla. Naomba vile vile nishukuru sana kwamba, katika michango iliyojitokeza wengi mmeendelea kukiri uadilifu na umahiri mkubwa wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, katika kuliongoza Taifa letu. Nawashukuru sana kwa jambo hili, na naomba mwendelee kuheshimu Taifa hili kama ambavyo tumekuwa tukifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Richmond limechangiwa kwa hisia nyingi tofauti. Lakini nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Spika na Wabunge wote kwamba, hili ni jambo letu sisi wote na ni wajibu wetu sisi wote kuendelea kulizungumza mpaka tutakapolifikisha mwisho. Naomba niwashukuru sana kwamba, katika michango hii kuhusiana na Richmond wengi mmesema kwa dhati kabisa kwamba, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kamwe alikuwa hahusiki na jambo hili, jambo ambalo nawashukuru sana na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atawaongezea kila jema ili mwendelee kuongoza Bunge hili kwa namna ambayo ni ya busara na hekima zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana kwa yote mliyoyasema juu ya Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri wake. Najua ni kazi nzito ambayo tumekabidhiwa na Bunge lako pamoja na Taifa kwa ujumla, lakini tutajitahidi kwa kadri tukavyoweza kufanya kazi zetu kwa uadilifu mkubwa na kwa mategemeo na matarajio ya Watanzania wote. Nakubaliana na Mheshimiwa Shibuda kwamba, huyu baba wa kufikia atajitahidi kadri itakavyowezekana kutekeleza majukumu iwezekanavyo. (*Makofi*/*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie basi kwa kumwomba Mwenyezi Mungu awatangulie ninyi wote, awalinde na awaongoze katika safari za kurejea Majimboni. Aidha, Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani unatarajiwa kuanza katika kipindi cha takribani mwezi mmoja ujao. Naomba nitumie nafasi hii kuwatakia Waislamu wote Mfungo mwema kwa kila atakayeamua kufanya Ibada hiyo ya pekee katika maisha ya kila mwenye kuamini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi Tarehe 27 Okotoba, 2009, Siku ya Jumanne, Saa Tatu (3:00) Asubuhi litakapokutana katika Ukumbi huu, hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa niaba ya sisi Wabunge wote nami naongeza sauti yangu kwa shukrani zote ulizozitoa kwa makundi mbalimbali na hususan Wabunge wote wa Bunge hili na kwa niaba ya Wabunge tunawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ushirikiano mkubwa katika kujibu maswali na kufanya utafiti. Yote yametusaidia sana!

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji nina tangazo moja tu kwamba, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, nayo ikutane baada ya kuahirisha Bunge katika Ukumbi, hapa wametaja Na. 227 ambao tayari kuna Kamati nyingine, lakini nadhani wakifika hapo wataweza kusikilizana.

**WIMBO WA TAIFA**

*Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa*

*(Saa 07.55 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku yaJumanne,*
*Tarehe 27 Oktoba, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*